

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Hamsini na Moja – Tarehe 15 Juni, 2021**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza na maswali. Swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, litaulizwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi, Mbunge wa Moshi.

Na. 420

**Barabara ya Bomang’ombe – Kikafu Chini – Shing’oro  
– Shing’oro Mferejini – Makoa**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI K.n.y. MHE.  
SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa Barabara ya Bomang’ombe – Rudugai – Chekimaji – Kikafu chini – Kawayu – Mijengweni – Shing’oro Mferejini hadi Makoa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Bomang’ombe – Rudugai – Chekimaji – Kikafu Chini – Kawaya – Mijengweni hadi Shing’oro Mferejini hadi Makao zimesajiliwa kwa majina ya Bomang’ombe – Kikafu Chini na ina urefu wa kilomita 26.53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Shing’oro – Mijengweni hadi Makoa yenye urefu wa kilomita 12.7 na Barabara ya Mferejini – Makoa yenye urefu wa kilomita 21 ni barabara muhimu katika Halmashauri ya Hai na zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini wa Wilaya ya Hai. Serikali inatambua kuwa barabara hizi ni miongoni mwa barabara zilizoahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami katika ahadi za Rais na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza ahadi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuzifanyia matengenezo barabara hizo ili kuhakikisha zinapitika katika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, *TARURA* Halmashauri ya Hai iliidhinishwa shilingi milioni 72 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Bomang’ombe – Kikafu Chini kipande chenye urefu wa kilomita 14 kwa shilingi milioni 35 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Shing’oro – Mijengweni kipande chenye urefu wa kilomita 4 na sShilingi milioni 67.5 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Mferejini – Makoa kipande chenye urefu wa kilomita 6.4 ambapo matengenezo ya barabara hizo yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, *TARURA* Halmashauri ya Hai imetengewa

jumla ya shilingi milioni 628.2 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Bomang'ombe – Kikafu Chini kipande chenye urefu wa kilomita 10 na boksi kalvati moja la Shing'oro – Mijengweni kipande chenye urefu wa kilomita 8 na ujenzi wa barabara ya Mferejini – Makoa kwa kiwango cha changarawe kwa kilomita 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi na kutekeleza ahadi za Rais za ujenzi wa barabara za lami katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri ya Hai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Patrick.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Ndugu yetu pia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza nauliza kwa kuwa, tayari barabara ya Mferejini – Narumu – *Takri* – Lyamungo hadi Makoa imeshatengewa shilingi milioni 500 kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa hivi kuongeza pesa mwaka huu wa fedha, ili hiyo barabara ikamilike kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swali la pili, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa *International School* kwa Raphaeli, Umbwe, inayounganisha na hii Barabara ya Mheshimiwa Mafuwe kule Lyamungo kwa kiwango cha lami? Ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa hii barabara inayoishia pale Mto Sere?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameeleza, kwanza ametambua kwamba, Serikali tumepeleka fedha milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya lami. Na kikubwa ambacho ameomba tu ni kwamba, je, Serikali ni namna gani tutaongeza fedha kwa ajili ya barabara hiyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, moja, tuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama yetu Samia Hassan Suluhu kwa kutoa fedha milioni 500 kwa majimbo yote nchini kwa ajili ya barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili kwenye jambo hili tuombe Bunge lako tukufu mpitishie bajeti kuu, ili yale mapendekezo yaliyoletwa na Wizara ya Fedha ya kuongezea *TARURA* fedha katika kile chanzo cha shilingi 100 iweze kupita maana tutapata fedha. Na hizi fedha tutakazopata maana yake tutakwenda kuongeza barabara katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo hili ejeo ambalo mmeliainisha hapo. Kwa hiyo, ombi letu kwenu mpitishie bajeti kuu na sisi tutafanyia kazi maombi yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyaleta kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ameeleza hii Barabara ya *International School* kupitia Umbwe na hayo maeneo ambayo ameyaainisha ambayo yako katika jimbo lake:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge hivi ninavyozungumza kazi nzuri ambayo ulikuja Ofisini kwetu na ukatuomba tumeanza kwanza kujenga mifereji katika barabara hiyo na itakavyokamilika maana yake tutaipandisha hadhi kwa kuongezea viwango vile ambavyo vinastahili. Kwa hiyo, ndio kazi ambayo tumedhamiria kuifanya na tutaifanya kwa wakati wote, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond nimekuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninakubaliana na aliyosema Naibu Waziri:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hizi ziko kwenye tambarare ya Kilimanjaro na mvua zote zinazonyesha mlimani zinashuka chini na kufagia changarawe yote iliyowekwa na *TARURA*. Na kwa kuwa, Barabara ya kutoka Hai kwenda Rundugai inaunganisha Barabara ya *TPC* ambayo ni ya lami.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kabisa kuanza barabara hiyo kwa lami kuliko kila wakati kumalizia hela za Serikali kwenye changarawe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Kilimanjaro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameeleza *concern* njema kabisa yenye nia njema. Niseme kwamba, tumelipokea ombi lako tutakwenda kufanya tathmini, ili tuingize katika mipango inayofuatia ya kuhakikisha tunaiondoa hiyo adha. Sio kila wakati tu hizi barabara zetu zikawa zinaondolewa na mvua kutokana na ile changamoto ya udongo au kifusi kwa hiyo, tunachokitaka sisi ni kuhakikisha kwamba, hizi barabara zinatengenezwa katika kiwango ambacho muda wote zitakuwa zinapitika.

Kwa hiyo, nilipokee hilo na tutaliingiza katika mpango, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa auklize swali lake.

Na. 421

## Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Lami Bagamoyo

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa barabara ya lami yenye urefu wa Kilomita tano ndani ya Mji wa Bagamoyo itatekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza ahadi ya Rais ya ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 5 iliyotolewa katika mwaka wa fedha 2015 ambapo hadi mwaka 2019/2020 barabara zenye urefu wa kilomita 2.36 zimejengwa kwa gharama ya shilingi bilioni 2.37. Barabara hizo zinajumuisha Barabara ya Stendi ya Kongowe – Kwa Chambo kilomita 0.6, Mgonera – Forodhani kilomita 0.63, Rubeya kilomita 0.7 na Soko la Uhindini kilomita 0.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 375 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bomani kipande chenye urefu wa kilomita 0.4 kwa kiwango cha lami. Tayari Mkandarasi ameshapatikana na yupo kwenye maandalizi ya kuanza kazi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 375 kwa ajili ya ujenzi wa Barabara ya Kapala kwa kiwango cha lami yenye urefu wa kilomita 0.45.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muharami.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara hizi ahadi yake ni ya muda mrefu na zimetengewa kiasi kidogo sana cha pesa. Na tuna barabara nyingi sana ambazo katika Mji wa Bagamoyo zinahitaji kupata huduma ya lami, mfano.

Je, ni lini Serikali itachukulia umuhimu Barabara ya Makofia – Mlandizi kwa sababu ni barabara muhimu sana ambayo inapita katika chanzo cha maji ambayo wanakunywa watu wa Dar-es-Salaam pamoja na pwani ambapo panaitwa bomu. Ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami hii njia ili kunusuru magari yanayonasa kupeleka dawa wananchi waweze kunusurika afya zao katika mikoa hii?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameanisha hapa, moja kwamba hizi barabara imekuwa ni ahadi ya muda mrefu na fedha inayotengwa ni ndogo, lakini pili ameanisha Barabara ya Kofia – Mlandizi ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wake wa Jimbo la Bagamoyo kwamba, ni lini sasa Serikali tutatenga fedha:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama nilivyojibu katika majibu ya awali kwamba, moja ya wajibu wetu sisi ni kupokea mapendekezo yanayoletwa na Wabunge, lakini la pili ni kuhakikisha kwamba, zile ahadi zote ambazo viongozi wetu wakuu walizitoa zinatekelezwa. Na tutaendelea kuzitekeleza kwa kadiri ya upatiakanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana katika jibu langu la msingi nikasema niwaombe Wabunge wote wapitishie Bajeti Kuu ya Serikali ili kile chanzo kilichokuwa kimetengwa zile fedha maana yake zitaongeza kuna kitu tutakwenda kukifanya. Na haya maombi mnayoleta maana yake tutayatekeleza. Hakuna barabara yoyote inaweza kutekelezeka bila kuwa na fedha. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge muweze kufanya hivyo, ili tuweze kufanya kazi nzuri ya kuwasaidia wananchi wetu. Kwa hiyo, tunayapokea hayo tutayafanyia tathmini na tutayaweka katika mipango yetu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, nimekuona swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa ahadi ya barabara hizi imetolewa pia kwenye Jimbo la Kibaha Vijijini kwenye Mji wa Mlandizi na tayari kuna barabara ya kilometa moja imeanza kutekelezwa na miezi sita sasa hajalipwa chochote. Je, Serikali haioni ni muda sahihi sasa kumaliza ile fedha ili mkandarasi amalizie ili hata ile kazi ambayo ameshaanza kufanya isiharibike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara zote ambazo wakandarasi wako *site* zitaendelea kulipwa fedha ili ziendeleo kukamilika, ikiwemo hii barabara ambayo umeitaja hapa.

Kwa hiyo, haitakwama kwa sababu ninaamini kabisa kwamba, sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kupitia *TARURA* tunapitia zile *certificates* ambazo wakandarasi wanazileta

kwetu na tunazitolea fedha. Kwa hiyo, na hili tumelisikia na nikuhakikishie kwamba, itaisha kwa wakati kama ambavyo iliahidiwa na viongozi wetu wakuu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 422

### **Sera ya Afya ya Kuwa na Kituo cha Afya Kila Kata**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutekeleza Sera ya Afya ya kuwa na Kituo cha Afya kwa kila Kata ili kupunguza vifo vya Mama na Mtoto?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Afya ya kuwa na Zahanati kwa kila Kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata kwa awamu ambapo kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 hadi 2020/2021 Serikali imejenga Zahanati 1,281, Vituo vya Afya 488 na Hospitali za Halmashauri 102. Mpango huu umewezesha kuongeza Vituo vya Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa vyenye uwezo wa kutoa huduma za dharula za upasuaji kutoka Vituo 115 Disemba 2015 hadi Vituo 352 Juni 2021 na hivyo kuchangia katika kupunguza vifo vya mama wajawazito na Watoto. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali itaendelea na ujenzi wa vituo vya afya 121 na kiasi cha shilingi billioni

27.75 kimetengwa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma 768 ya zahanati kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha za ujenzi wa vituo vya afya kwa awamu. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa Naibu Waziri amejibu hapa kwamba, ni Sera ya Serikali kwamba kuwe na zahanati kwa kila kijiji, lakini pia, kituo cha afya kwa kila kata. Wilaya ya Kyerwa yenye kata 24 ina zahanati tatu, yenye vijiji 99 ina zahanati 23. Ningependa kujua je, kwa wilaya ya Kyerwa hiyo sera inatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni mkakati gani Serikali ilionao kuhakikisha wananchi wa Kyerwa nao wananufaika na Sera ya Serikali ya kuwa na huduma ya afya kila kijiji, kila kata? Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge. Kama ambavyo nimejibu katika maswali ya msingi kwamba, Serikali katika kipindi cha miaka mitano imejenga zahanati zaidi ya 1,200 vituo vya afya zaidi ya 488 na hospitali za halmashauri zairi ya 102, lakini mkakati huu unaendelea kutekelezwa na Halmashauri hii ya Kyerwa ni miongoni mwa halmashauri ambazo zitapewa kipaumbele kuhakikisha vijiji vyake na kata zinapata vituo vya afya ili kusogeza huduma za afya kwa wananchi. Kwa hiyo, naomba

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, awamu zinazofuata tutaendelea kuongeza kasi, lakini pia kuipa kipaumbele halmashauri ya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili. Mkakati wa Serikali ni huo wa kuhakikisha kwamba, sasa kila kijiji, lakini pia kila kata na kila halmashauri inapata vituo vya huduma za afya, ili kusogeza huduma kwa wananchi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo, nimekuona.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi na niipongeze Serikali kwa juhudi madhubuti za kuboresha ujenzi wa vituo vya afya, zahanati pamoja na hospitali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Misenyi ni wilaya ambayo ina kata 20, lakini mpaka sasa inavyo vituo vya afya viwili. Sasa ni lini zamu ya Wilaya ya Misenyi itafikiwa angalao kuongezewa vituo vya afya kwa juhudi kubwa ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo hili la Nkenge na Halmashauri ya Misenyi kwa ujumla wake Serikali imeweka kipaumbele cha kuhakikisha inafanya tathmini ya maeneo ambayo yatapelele kipaumbele cha kuanza kujenga zahanati, lakini pia vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali katika

mwaka ujao wa fedha imetenga kujenga vituo vya afya 121, lakini katika miaka mingine inayofuata ya fedha pia, tutahakikisha tumeweka kipaumbele cha kujenga vituo vya afya kwa hivyo, Jimbo hili la Nkenge na Halmashauri ya Misenyi pia, ni moja ya halmashauri ambazo zitapewa kipaumbele. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 423

### **Mradi wa Kusambaza Umeme – Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Mradi wa kusambaza umeme katika Jimbo la Kibaha Mjini unakwenda kwa kusuasua:-

Je, ni lini Mradi huo utakamilika ili Wananchi wa Kibaha Mjini waondokane na adha ya umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kusambaza umeme kwa Wilaya ya Kibaha Mjini (*Peri-Urban*) ulianza mwezi Novemba, 2019. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayonufaika na mradi huu ni pamoja na Pangani, Maili Moja, Picha ya Ndege na Sofu. Gharama ya Mradi ni shilingi bilioni 18.56.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa.

**MHE. SILYVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa sababu kwa kweli kwa kipindi kifupi imefanya kazi nzuri na hasa ilivyoondoa mkanganyo wa ulipaji wa kufungiwa umeme kwa wananchi ili tunalishukuru sana Serikali yetu imefanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kibaha bado tuna matatizo makubwa ya kusambaziwa umeme kwa wananchi na hususani katika mitaa ya Viziwaziwa kwa maana ya Sagale Magengeni, Sagale kambini lakini Muheza pamoja na maeneo mengine ya Misugusugu kwa maana ya Zogohale na Miomboni pia vilevile Madina hadi Kiembeni toka 2016 baadhi ya wananchi bado hawajapata umeme.

Je, ni lini sasa wananchi hawa watawekewa umeme ili waondokane na adha ya kukosa umeme katika Mji wa Kibaha?

Swali la pili, toka mwaka 2014 wananchi wengi wa Jimbo la Kibaha mjini walisimamishiwa maendeleo katika maeneo yao ambayo kunategemewa kupita mradi wa umeme wa msongo wa *Kilowatt* 400 kutoka Kinyerezi kuelekea Chalinze wasifanye lolote ingawa hadi leo bado wengine wanaendelea hata kutozwa kodi za ardhi.

Je, ni lini wananchi hawa watapata fidia zao ili waweze kufanya maendeleo maeneo mengine na kuondokana na adha hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Byabato.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Koka Mbunge wa Kibaha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya maeneo ya Mji wetu wa Kibaha hayajapata umeme lakini tayari Serikali imejitahidi kupeleka umeme katika hayo maeneo machache ambayo ni jitihada ya Mheshimiwa Mbunge katika kufanya ufuatiliaji wa kina kuhakikisha maeneo yote yanapata umeme. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote ya Kibaha yataendelea kupelekewa umeme kupitia mradi wetu wa *Peri-Urban* na tayari Mkandarasi huyo ameshaongezewa *scope* ya kazi kwa hiyo maeneo yote ya Ziwaziwa na mengine ambayo yametajwa na Mheshimiwa Mbunge yote yatafikiwa na umeme kadri tunavyozidi kuendelea mbele kwasababau ni jukumu la *TANESCO* na *REA* na Serikali kuendelea kupeleka umeme kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, ni kweli kwamba kuna maeneo ambayo yalitwaliwa na Serikali kwa nia ya kupitisha mradi wa Msongo wa *kilovolti* 400 kusafirisha umeme na sasa utakuwa unasafirishwa kutoka Chalinze kuelekea Kinyelezi kwa sababu uzalishaji mkubwa unafanyika katika maeneo ya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imetoa fedha kwa *TANESCO* takribani Billioni 29.6 na kuanzia Julai, Mosi fidia zitaanza kulipwa kwa wananchi wa maeneo ya Chalinze, maeneo ya Kibaha na maeneo ya Kinyerezi kwa ajili ya kupisha mradi huo uanze kujengwa mara moja.

**MWENYEKITI:** Sasa swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Vijijini.

Na. 424

### **Kufikisha Umeme wa Msongo Mkubwa-Katavi**

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kasi ya kufikisha umeme wa msongo mkubwa katika Mkoa wa Katavi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme wa gridi ya Taifa kwa msongo wa kilovolti 132 yenye urefu wa kilometa 381 kutoka Tabora hadi Katavi na ujenzi wa vituo vitatu vya kupoza umeme vya msongo wa kilovolti 132 kwenda 133 vya Ipole, Inyonga na Mpanda. Ujenzi wa majengo ya vituo vya kupooza umeme vya Ipole na Inyonga pamoja na uzio umekamilika kwa takribani asilimia 90. Mradi unatarajia kukamilika ifikapo Agosti, 2023, gharama ya mradi ni Shilingi Bilioni 64.9

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaendelea na utaratibu wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga kupitia Mpanda hadi Kigoma takribani kilometa 1,232. Kazi inayofanyika kwa sasa ni kukamilisha taratibu za kupata Mtaalamu Mshauri wa kuandaa nyaraka za kumpata Mkandarasi wa kuanza ujenzi wa mradi. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza Novemba, 2022 na kukamilika mwezi Oktoba, 2024. Gharama ya mradi ni Shilingi Bilioni 470.42.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ilivyo katika eneo la mradi kuna hali ya kusuasua, nilichokuwa naomba nafahamu uhakiki wa uwezo wa mtengenezaji kwa maana ya *due-diligence* jambo hili bado halijafanyika sambamba na utiaji

saini mikabata, nilikuwa naiomba Serikali inihakikishie ni lini suala hili litafanyika ili kuharakisha mradi huu? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kapufi wa Mpanda kama ifuatavyo, kama tulivyosema katika swali la msingi ni kwamba tayari ujenzi umeanza kwenye maeneo hayo na vituo vya kupoozea umeme tayari vimetengenezwa na majengo yake yamekamilika kwa asilimia 90, ni kweli kwamba uhakiki wa uwezo wa Mkandarasi wa kututengenezea vile vifaa vya ndani ya kile chumba cha kupoozea umeme vikiwemo *generator, transform* na vitu kama hivyo *broker* na *breakers* nyingine haujafanyika vizuri kwasababu ya tatizo kubwa ambalo liliwapata wenzetu ambao wanaweze kututengenezea vifaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni vigumu kwetu sisi kutuma wataalam wetu kwenda kwenye hizo nchi ambazo zinao watengenezaji wa vifaa hivi vikubwa kwenda kuhakiki uwezo wa watengenezaji hao. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ufuatiliaji wake sisi kwetu ni faraja na tunaelekea kukamilisha kwa sababu tayari sasa nchi ambazo zinatengeneza vifaa hivi zimeanza kuruhusu watu mbalimbali kwenda kufanya shughuli mbalimbali kwenye nchi zao baada ya janga la Korona kupungua kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajiandaa kutuma wataalam wetu kwenda kuhakiki kama wale tuliowapa kazi wana uwezo wa kutengeneza hizo mashine tunazojiomba na baada ya hapo mikataba itasainiwa kama tulivyosema kwenye jibu la Msingi kwamba 2023 mradi huu utakuwa umekamilika na grid ya Taifa itafika Mpanda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mradi wa *REA-I* na *REA-II* katika Wilaya ya Kyela Vijiji vya Lupaso Ndondwa na Mabuga mpaka sasa hawajapata umeme.

Je, nini jitihada za Serikali kuhakikisha tunapata umeme maeneo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo fupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakaganda Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli yapo baadhi ya maeneo ambayo *REA I* na *REA II* ilikuwa haijakamillisha, kulikuwa na changamoto mbalimbali ambazo sasa tumezitaifutia mkakati maalum wa kuzimaliza na tunahakikisha kwamba inapoelekea 2022 tunapomaliza *REA III round II* na vile viporo vyote vya nyuma tutakuwa tumevimaliza, yalikuwepo matatizo ya Wakandarasi kushindwa kumaliza kazi kwa sababu ya changamoto mbalimbali lakini sasa tatizo hilo tumelitibu na tutahakikisha kwamba kila mwananchi anapata umeme katika maeneo yote ambayo yamepitiwa na mradi kulingana na *scope* ilivyokuwa kufikia 2022 kama ambavyo tumesema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa David Kihenzile swali fupi la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili la hali ya Mufindi linafanana pia na hapa mtangulizi amezungumza lakini tofauti ni kwamba asilimia 70 ya nguzo katika nchi hii zinatoka pale kwenye Jimbo letu, sasa ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye maeneo ambayo ni ya giza pamoja na kwamba nguzo zinatoka pale, *especial* maeneo la Idete, Maduma pamoja na Idunda na vijiji vya Kisasa na maeneo mengine

ambayo hayana umeme kabisa na wanashuhudia nguzo zikipita kila siku mbele yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kihenzile Mbunge wa Mufindi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunakiri kuna maeneo bado hayana umeme mpaka sasa, Mufindi ni eneo mojawapo ambalo mkandarasi wa *REA III round II* tayari amepatikana *MS Services* na tayari ameenda kufanya *survey* kwenye maeneo husika, tunamhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utuatiliaji wake ambao amekuwa akiufanya mara kwa mara utazaa matunda na tutapeleka umeme katika vijiji vyote alivyovisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hilo lazima lipewe kipaumbele na heshima kwa sababu ndiyo linalisha na maeneo mengine yanayotumia nguzo za miti, kwa hiyo kweli katika hali ya kawaida siyo kitu cha kufurahisha kuona unatoa bidhaa halafu wewe haunufaiki nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya mwaka 2022 kukamilika tutakuwa tayari tumefikisha umeme katika maeneo yote ambayo hayana umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Mpakate Mbunge wa Tunduru Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 425

### **Hitaji la Umeme wa REA- Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza: -

Jimbo la Tunduru Kusini lina Vijiji sita kati ya 65 vyenye umeme.

(a) Je, ni lini REA Awamu ya Tatu utaanza?

(b) Je, ni lini umeme wa ujazilizi wa maeneo ambayo bado umeme haujafika hasa Vitongoji vya Vijiji vya Azimio, Chiwana, Umoja, Mkandu, Mbesa, Airport, Namasalau, Tuwemacho, Ligoma, Mchuruka na Makoteni vitapatwa umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme wa REA Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili ulianza mwezi Machi, 2021. Mradi huu utakamilika ifikapo mwezi Desemba, 2022. Katika jimbo la Tunduru Kusini Vijiji vyote vilivyobaki vitapelekwa umeme kupitia mradi huu wa REA-III unaoendelea kupitia Kampuni Mbili za Wakandarasi *M/S JV Guangdong Jianneng Electric Power Engineering CO. LTD* na *White City International Contractors LTD*. Gharama ya Mradi ni shilingi bilioni 27.25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usambazaji wa umeme wa ujazilizi katika vijiji vya Jimbo la Tunduru Kusini vikiwemo vitongoji vya Vijiji vya Azimio, Chimwana, Umoja Mkandu, Mbesa, Airport, Namasalau, Tuwemacho, Ligoma, Mchuruka na Makoteni utaanza mwezi Septemba, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2022.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru Serikali kwa kupeleka mkandarasi amesharipoti tarehe 11 Mwezi huu. Kwa kuwa Serikali inaenda kutekeleza mradi huu katika vijiji vyote vya Jimbo la Tunduru Kusini na Tunduru kwa ujumla na tatizo la Umeme Tunduru kukatika katika ni jambo la kawaida.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga *substation* pale Tunduru Mjini ili kutoa huduma hii kwa vijiji vyote kwa sawasawa? (*Makofi*)

Swali la pili, kwa kuwa *REA* imeanza kutekelezwa katika vijiji vyote vilivyopo Jimbo la Tunduru Kusini pamoja na vijiji vya Azimio, Semeni, Angalia Je, Serikali sasa haioni kuna haja sasa ya kuweza kutoa tamko la kuweza kuisaidia *TANESCO* kwa asilimia 100 ili waweze kutoka huduma hiyo kwa shilingi 27,000?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Daimu Mpakate Mbunge wa Tunduru kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu hoja ya kupeleka *substation* tuichukue tukaifanyie mkakati na upembuzi yakinifu na kuona kama ujenzi wa *substation* peke yake ndio utasaidia kutokatika kwa umeme katika maeneo hayo au njia nyingine inaweza ikaboresha kwa sababu pengine kama umeme unaofika ni mkubwa wa kutosha maana yake tunatakiwa kuboresha miundombinu badala ya kujenga *substation*. Tunalichukua tutaenda kulifanyia kazi na tutaweza kufikisha huduma nzuri kabisa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili tayari Serikali imeshatoa maagizo na maelekezo ya kuunganisha umeme kwa wateja wote kwa shilingi 27,000, katika bajeti iliyowasilishwa na Wizara ya Nishati kwa niaba ya Serikali ilisemwa hapa wazi na Mheshimiwa Waziri kwamba maeneo yote itakuwa ni shilingi 27,000 isipokuwa Dar es Salaam City

*Centre.* Tayari wenzetu wa TANESCO wametoa *circular* kwa Meneja wa Wilaya na wa Mkoa kuhakikisha kwamba agizo hilo linatekelezwa na tunafahamu linaendelea kutekelezwa, lakini pale Waheshimiwa Wabunge ambapo bado mnaona changamoto basi tuwasiliane ili tuweze kuchukua hatua kwa sababu mambo mengine yanahitaji kusimamiwa kwa ajili ya manufaa ya wananchi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu nimekuona.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Mkoa wa Simiyu una vijiji 470 na vijiji vilivyopata umeme ni 332 vimeshapata umeme vijiji vilivyobaki ni 138.

Je, ni lini Serikali itakamilisha kupeleka umeme katika vijiji vilivyobaki. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Simiyu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema ni kweli kwamba kuna maeneo bado hayajapata umeme katika vijiji takribani kama 1,500 nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hivyo vijiji 132 ambavyo bado havijapata umeme kwa Mkoa wa Simiyu na vyenyeve vitapelekewa umeme kabla ya mwezi Desemba 2022 kwa sababu tayari mkandarasi tumempata na tunaamini amesharipoti *site* yupo katika hatua za kwanza za kufanya *survey* kuhakiki kwamba vijiji vimechukuliwa na baada ya hapo kazi itafanyika kwa muda uliopangwa na kukamilisha umeme kufikia Desemba 2022. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Byabato Naibu Waziri wa Nishati kwa majibu mafupi. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa

Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake. (*Makofi*)

Na. 426

### **Tatizo la Mawasiliano ya Simu – Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, ni lini Kata 16 zisizo na mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Urambo zitapatiwa mawasiliano ya simu na kuwaondolea wananchi adha ya kutokuwa na mawasiliano kwa muda mrefu?

Je, ni kwa nini kuna maeneo yenye minara ya mawasiliano ya simu lakini kuna matatizo ya mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Urambo lina jumla ya Kata 18 ambapo Kata zote zina huduma ya mawasiliano isipokuwa vijiji baadhi katika Kata Tisa za Kiloleni, Itundu, Imalamakoye, Ugalla, Vumilia, Nsondo na Uyogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Utundu na Ukondamoyo zitafikishiwa huduma za mawasiliano na kampuni ya simu ya *Vodacom* ifikapo Oktoba, 2021, Kata za Nsondo na Uyogo zitafikishiwa huduma za mawasiliano na kampuni ya *Airtel* ifikapo Oktoba, 2021, Kata ya Vumilia itafikishiwa huduma za mawasiliano kupitia kampuni ya simu ya *Halotel* ifikapo Septemba, 2021 pamoja na Kata ya Ugalla

itakayofikishiwa huduma na kampuni ya simu ya *TTCL* ifikapo Septemba, 2021. Aidha Kata za Kiloleni na Imalamakoye zitaingizwa kwenye miradi ya mfuko itakayotekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu mbalimbali zinazoweza kusababisha kukosekana huduma ya mawasiliano kwenye maeneo yenye minara ya simu ikiwa ni pamoja na hali ya kijiografia ya eneo husika kama vile uwepo wa milima, mabonde na uoto wa asili wenye miti..

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge punguzeni sauti tusikilize majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba sauti zimezidi punguzeni. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabonde, uoto wa asili wenye miti mirefu ambayo huzuia huduma za mawasiliano. Hali ya kukosekana kwa nishati ya umeme wa uhakika pia inaweza kusababisha minara kushindwa kutoa huduma za mawasiliano. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake lakini bado ningepomba kwa kuwa maisha ya sasa yanategemea sana matumizi ya simu na wahusika wanaathirika kwa kiasi kikubwa naomba niyataje maeneo hasa ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua haraka iwezekanavyo, Kata ya Itundu, hasa Katuli, Ilani, Kiloleni, Mwinyi, Kalembela, Jumbe na Kikwete Kata ya Muungano ni Muungano yenyewe, Magulungu, Isenda, Utenge na Kangeme, Kata ya Usisya ni Usisya Kati, Mabundulu, Katungulu na Majengo. Kata ya Uyogo ni Uyogo yenyewe, Igembesabo, Kasela, Igunguli na Mirambo, Kata ya Ugala ni Ugala yenyewe Izengamatogile na Isogwa, Songambebe, Mlangale na Ukwanga na Kata ya Kapilula ni

Kata yote, naomba lini wanapatiwa mawasiliano watu wa Urambo. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Injinia Andrea Kundo majibu ya swali hili la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya wananchi wa Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli alichokiongea Mheshimiwa Mbunge ni kweli kabisa, kwasababu tayari tarehe 16 Machi 2021 nilifanya ziara katika Jimbo lake la Urambo, na kweli nikagundua kuna maeneo ambayo bado yana changamoto ya mawasiliano. Lakini katika maeneo ambayo tuligundua yana changamoto ya mawasiliano, tulitoa maelekezo ili tathmini ifanyike na kuhakikisha kwamba wananchi wa Urambo hawapitwi mbali na huduma ya mawasiliano kwa ajili ya kujiletea maendeleo kupitia mtandao wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka, nimekuona.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jimbo la Tabora Mjini lina kata 29 na vijiji 41, na katika vijiji hivyo vingi havina mawasiliano ya simu na vijiji vingine vipo karibu kabisa, kilomita mbili tu kutoka mjini lakini bado ni vigumu kupata mawasiliano; mathalani kata ya Itetemya. Ninaomba kuuliza;

Je, ni lini Serikali itatufanyia mpango wa kuongeza angalau minara ili mawasiliano yaweze kuwa mazuri? ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Andrea Kundo majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya mawasiliano ni takriban nchi nzima ina changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ambazo zinatokana na teknolojia iliyowekwa katika eneo husika, lakini pia mnara uliowekwa pale inategemea kwamba uliwekwa katika wakati upi, kwamba iawezekana kulikuwa na *population* ya watu wachache na sasa wameongezeka sasa mnara unaweza ukazidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu kabisa kwamba kuna maeneo ambayo kutokana na sababu za kijiografia unakuta kwamba katika kata moja mawasiliano yapo katika vijiji sita lakini Kijiji kimoja kinakuwa kinakosa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kupitia Wizara yetu imeanza kufanya utafiti wa kujiridhisha ili tuweze kupata teknolojia ambayo tutakuwa tunafikisha huduma ya mawasiliano katika zile *sports* ambapo unakuta kwamba ni Kijiji kimoja tu ambacho kimekosa mawasiliano lakini tufikishe kwa teknolojia ambayo ni nafuu na yenye gharama nafuu. Waheshimiwa Wabunge pia tuweze kusaidiana kuhakikisha kwamba tunawaelewesha wananchi wetu kujua kwamba mawasiliano yatafika kwasababu bahati nzuri mmetusaidia kupitisha bajeti ambayo itatufikishia mawasiliano katika vijiji vyetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Andrea Kundo, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang sasa aulize swali lake.

Na. 427

## Ujenzi wa Barabara ya Katesh - Hydrom

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Katesh – Hydrom kwa kiwango cha lami ili kuwarahisishia wananchi kupata huduma za afya katika Hospitali ya Hydrom pamoja na usafirishaji wa mazao hasa ngano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Katesh – Hydrom yenye urefu wa kilometa 67 ni sehemu ya barabara ya mchepuo wa Mbuga ya Serengeti (*Serengeti Southern Bypass*) ambayo inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu wa Barabara ya Mchepuo ya Mbuga ya Serengeti (*Serengeti Southern Bypass*) yenye urefu wa kilometa 575.6 inayojumuisha barabara ya Karatu – Hydrom – Lalago hadi Maswa yenye kilometa 446.6, Katesh – Hydrom yenye kilometa 67 na Kolandoto – Lalago yenye kilometa 62 inatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Ujerumani. Upembuzi yakinifu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, mwaka huu 2021. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Katesh – Hydrom utaanza pindi usanifu wa kina utakapokamilika na kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Samweli Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa Serikali imesema upembuzi yakinifu wa barabara ya Katesh – Hydrom unakamilika Juni, yaani mwezi huu; na kwasababu mfumo wa sasa ni wa kusanifu na kujenga. Je, baada ya mwezi wa sita ambapo upembuzi utakamilika Serikali iko tayari kuanza ujenzi mara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye barabara hiyo kuna maeneo mawili korofi moja ni daraja ambalo lipo Njia Panda ya Dawar kwenye hiyo barabara ya kwenda Hydrom, lakini lingine ni ule Mlima Chavda ambao unakwaza usafiri na usafirishaji kwa kata za Bassodesh, Garawja, Hirbadaw, Getanuwas, Bassotu, Murbadau, Dawar yenyewe na Mogitu na mara nyingi wananchi wamekuwa wakipoteza maisha yao na kupoteza mali.

Je, Serikali itakuwa iko tayari sasa kuweka lami wakati tukitarajia ujenzi uanze kwenye eneo la Mlima Chavda na kujenga daraja imara pale kwenye ule mto uliopo kwenye njia panda ya Dawar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Samwel Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna aina mbili, ya usanifu na kujenga ama kusanifu halafu baadaye kujenga. Kwa kuwa tayari tunafanya upembuzi yakinifu, itategemea na upatikanaji wa fedha kama utaruhusu tufanye utaratibu wa kusanifu na kujenga. Lakini kama fedha itakuwa haipo, kwa

maana ya bajeti ya mwaka tunaoanza kutekeleza baada ya kukamilisha upembuzi yakinifu tutafanya usanifu wa kina ili barabara hiyo sasa iwe tayari kwa ajili ya kuanza kwa ujenzi wa kiwango cha lami kwa hela hiyo ya mfadhili kutoka benki ya Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu daraja na maeneo korofi tayari tulishatoa taarifa kwa mameneja wote barabara zote ambazo zina maeneo korofi waweze kuyaaanisha ili tuweze kuyafanyia mkakati wa kuyatengeneza si tu kwa barabara hii ya Hydrom – Katesh bali ni pamoja na barabara zote ili tuweze kuyatengeneza, hata ikiwezekana kuweka lami nyepesi ili yaweze kupitika kwa kiwango chote. Kuhusu madaraja wataalamu wako barabarani wakiwa wanaangalia uharibifu wa madaraja hayo yote na kuweza kuyatengeneza ili baada ya kipindi hiki cha mvua kukatika basi barabara zote ziweze kupitika bila kuleta bugudha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yustina halafu Mheshimiwa Cecil.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Dareda, Bashnet na Dongobesh, kwa kuwa barabara hii inaunganisha wilaya mbili wilaya ya Mbulu na Babati lakini vile vile itaunganisha halmashauri mbili ambazo zinahamia makao mapya halmashauri ya wilaya ya Mbulu inayohamia Dongobesh na halmashauri ya wilaya ya Babati ambayo sasa inahamia Dareda? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Yustina Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo. Barabara ya Dongobesh Dareda ni barabara muhimu ambayo tayari Serikali

imeshakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hivyo Serikali kwa sasa inatafuta fedha ili barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mara fedha itakapopatikana kama ambavyo imeainishwa basi katika mpango huu wa miaka mitano ni kati ya barabara ambazo ziko kwenye mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, *Engineer* Godfrey Msongwe, Mheshimiwa Mwambe nilikuita.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakazi wa Mtwara, Lindi pamoja na Ruvuma tunalazimika kufika Dar es Salaam kabla ya kuja Dodoma ambako ndiko Makao Makuu ya nchi. Lakini kimsingi kuna barabara inayoanzia Songea barabara nyingine inaanzia Masasi, Nachingwea, Liwale, Lupilo inakuja kutokea Morogoro, Ifakara, Malinyi ili kuweza kufika Dodoma kirahisi badala ya kutulazimisha tufike kwanza Dar es Salaam ndipo tuje Dodoma.

Sasa swali langu kwa Serikali kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa watu wa mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma ili tuweze kufika kirahisi Makao Makuu ya nchi ambako ni Dodoma, ni lini itatengenezwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil Mwambe, Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara anayoitaja ni barabara kuu; siyo barabara ya mkoa, ni barabara kuu, ambayo kama nimemuelewa ni hii barabara ambayo inaoanzia Lumecha, Londo, Kilosa kwa Mpepo, Malinyi, Ifakara hadi Mikumi ambayo nadhani inaunganisha mikoa ya Mtwara, Lindi na Songea kuja Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii iko kwenye mpango, na kama ameangalia bajeti tayari, na baadhi ya maeneo kuanzia tumejenga Daraja lile la Magufuli pale Mto Kilombero lakini pia kuna kipande cha lami ambacho kinajengwa kati ya Kidatu kuja Ifakara, na sasa ipo kwenye mpango kwa ajili ya kuendelea na barabara kuanzia Lupilo kwenda huku Kilosa kwa Mpepo hadi kuunganisha huku Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa tu ni fedha kupatikana halafu tukamilishe hiyo barabara kuu ambayo kwa kweli imekuwa ni hitaji kubwa sana kwa wananchi na Wabunge wa mikoa ya kusini ambayo ni ya Ruvuma, Mtwara, Lindi na Morogoro yenyewe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana *Engineer* Godfrey Msongwe kwa majibu mazuri hayo. Waheshimiwa Wabunge muda siyo rafiki tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Seif Hamis Gulamali Mbunge wa Manonga sasa aulizwe swali lake.

Na. 428

### **Hitaji la Maji ya Ziwa Victoria – Manonga**

**MHE. SEIF K. GULAMALI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya Makamu wa Rais ya kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Tarafa ya Simbo na Manonga katika Jimbo la Manonga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Maryprisca, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali, Mbunge wa Manonga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria, ambapo hadi sasa Vijiji vya Ziba, Igumila, Ibologero, Itibula, Mwalamo, Ngulu, Mwabubele, Nyandekwa, Itale na Usongo vilivyoko katika Tarafa ya Manonga, vimefikiwa na huduma ya maji kupitia mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kuanzia mwezi Aprili, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022, utekelezaji wa miradi ya maji utaendelea endapo mradi wa Maji toka Ziwa Victoria utatekelezwa na utanufaisha vijiji vya Ulaya, Nkinga na Barazani vilivyopo katika Tarafa ya Simbo na vijiji vya Imalilo, Ngulu, Igumila, Ndembezi, Itulashilanga, Njia Panda, Mwanzelwa vilivyopo Tarafa ya Manonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zitakazofanyika ni ulazaji wa bomba takribani kilometa 50, kujenga Matenki matano ya kuhifadha maji katika vijiji vya Igulu (lita 50,000), Ndembezi (lita 100,000), Ulaya (lita 50,000), Kitangili (lita 60,000) na Nkinga (lita 300,000) na kujenga vituo 60 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa mradi huu utaboresha hali ya upatikanaji wa maji katika Tarafa ya Simbo na Manonga kufika asilimia 85.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Seif Gulamali

**MHE. SEIF K. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka kumbukumbu vizuri naomba kurekebisha kidogo vijiji vya Ulaya, Nkinga na Barazani, kwamba viko Tarafa ya Manonga na si Tarafa ya Simbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza, kwasababu ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na sasa ndiyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni lini Serikali itapeleka maji ya Ziwa Victoria katika Tarafa ya Simbo hasa Makao Makuu ya Tarafa ya Simbo na Tarafa ya Manonga, hasa Makao Makuu ya Tarafa pale Choma cha Nkola kwa kuwa maeneo hayo yana idadi kubwa ya wananchi wanahitaji huduma hii ya maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Seif Gulamali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti Tarafa hizi mbili, ya Simbo na Manonga zote zipo katika mpango mkakati wa kukamilisha utekelezaji wa kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria. Mwaka ujao wa fedha wa 2021/2022 kadiri tutakavyopata fedha tutafikia maeneo hayo yote muhimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, nimekuona nyuma kule.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza napenda kuipa shukrani Serikali yangu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jinsi inavyofanya kazi zake katika Wizara hii ya Maji, inatekeleza kwa hali na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sasa hivi ni mkazi wa Dodoma nakaa maeneo ya Mkalama. Eneo lile la Mkalama maji yapo mengi sana lakini mabomba yanakuwa yanapasuka sana maji yanatoka na hovyoy. Mimi mwenyewe binafsi nakuwa nahisi huruma. Kwa hiyo nimwambie Mheshimiwa Waziri, kama Serikali imeliona suala hili kule sehemu ya Mkalama basi ifanye kazi zake kwenda kuyaziba yale mabomba ili maji yasitoke hovyoy. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Mheshimiwa Naibu Waziri naona jambo hili linawagusa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa hiyo tunaomba majibu hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipende kupokea pongezi kwa namna ambavyo ameridhishwa na utekelezaji wetu. Sasa kuhusiana na tatizo la maji kumwagika baada ya mabomba kupasuka maeneo ya Mkalama nipende kusema kwamba Meneja wa Maji Mkoa wa Dodoma *Engineer* Aron anafanya kazi usiku na mchana. Lengo ni kuona anakwenda kufanyia kazi mapungufu yote haya yanayoendelea kujitokeza. Siyo tu eneo la Mkalama hata wale wenzetu wanaotoka llazo taarifa za matatizo ya maji pale tunazo na tunazifanyia kazi. Tayari tumempa mtu kazi ya kuweza ku-*supply* mabomba.

Kwa hiyo mabomba haya yakifika, tunatarajia wiki hii yatafika, tunakuja kufanya ukarabati na marekebisho maeneo yote ambayo yana matatizo ya kupasuka na kumwaga maji mitaani.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryprisca, Naibu Waziri wa Maji. Tunamalizia Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga Mbunge wa Ludewa sasa aulize swali lake.

Na. 429

### **Kuanza kwa Mradi wa Liganga na Mchuchuma na Wananchi Kulipwa Fidia**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

(a) Je, ni lini wananchi wa Ludewa ambao maeneo yao yamechukuliwa na Serikali kwa muda mrefu kwa ajili ya

ujenzi wa mradi wa Liganga na Mchuchuma watalipwa fidia?

(b) Je, ni lini Mradi wa Liganga na Mchuchuma utaanza kufanya kazi ili kuinua uchumi wa Mkoa wa Njombe na Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi unganishi wa madini ya chuma na makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma uliopo katika Wilaya ya Ludewa, Mkoani Njombe ni Mradi wa Kimkakati na upo katika hatua za awali za utekelezaji. Mradi huu unategemea kutekelezwa kwa ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa - *NDC* ambalo litakuwa na 20% na Kampuni ya Sichuan Hongda (*Group*) Kampuni hii ya China yenye 80% baada ya majadiliano kuhusiana na baadhi ya vipengele katika mkataba wa utekelezaji mradi huu kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ili kuanza utekelezaji wa mradi, mwekezaji aliomba vivutio ambavyo vimeshindwa kutolewa na Serikali kwa sababu vinakinzana na Sheria mpya Na. 6 na 7 za mwaka 2017 ambazo ni *Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Renegotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hadi sasa, majadiliano na mwekezaji huyu yanaendelea ikiwemo suala la ulipaji wa fidia kwa maeneo yote ya mradi yaliyoathaminiwa. Utekelezaji wa mradi huo utaanza mara baada ya kukamilika kwa majadiliano hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; wananchi wa Ludewa wangependa kufahamu kwa kuwa wamesubiria fidia hizi kwa muda mrefu. Je, kwa nini Serikali isitenganishe majadiliano na mwekezaji na suala la fidia ili wananchi wa Jimbo la Ludewa waweze kulipwa fidia mapema?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ningependa kufahamu ni lini Serikali itanza kutoa elimu ya kuandaa wananchi wanaoathirika na miradi ili waweze kunufaika na miradi hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Jimbo la Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mradi huu fidia kwa wananchi iliyothaminiwa jumla ya bilioni 11.037 katika majadiliano au katika mkataba ambao tuliingia na kampuni hii *Situan Honda* ilikuwa yeye kama mwekezaji atakuwa na wajibu wa kulipa fidia eneo hilo ambalo atakuwa analitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema baada ya majadiliano na mwekezaji huyu tutaangalia sasa kama tutafikia muafaka maana yake yeye atakubaliana kulipa fidia, lakini utekelezaji wa mradi huu lazima uanze mwaka 2021/2022, aidha tumekubaliana na mwekezaji huyu au hatujakubaliana lakini mradi huu lazima uanze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameshaeleza na ni utekelezaji ambao unaenda kufanyika katika mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la elimu katika eneo hili, ni kweli Serikali imekuwa ikiweka fedha kwa ajili ya kuelimisha wananchi namna ambavyo watashiriki katika ujenzi wa mradi huu kwa maana ya *local content* kwamba wao watafanya nini au watashiriki vipi katika mradi huu mkubwa wa Mchuchuma na Liganga. Kwa hiyo fedha zinatengwa kila mwaka na elimu inaendelea kutolewa kwamba sasa mradi huu ukianza naamini ...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti mnaongea kwa sauti kubwa, ili tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba sasa tutakapoanza kutekeleza mradi huu, elimu zaidi itatolewa ili wananchi wa eneo hili waweze kushiriki katika utekelezaji wa mradi huu kikamilifu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kuendelea kuzungumzia mradi wa Mchuchuma na Linganga kwenye Bunge letu bila utekelezaji dhabiti ni aibu, ni wa muda mrefu tangu enzi ya akinamama Mary Nagu wakiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu unasuasua kwa sababu mwekezaji hana mtaji wa kutosha, ndiyo maana ameshindwa kulipa fidia. Kwa nini Serikali inamkumbatia huyu mwekezaji, kwa nini isiachane naye kama mama Samia anataka mradi huu uendelee, ikamtafuta mwekezaji mwingine na Serikali ikawekeza vya kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza. Nimemwona Mheshimiwa Waziri Profesa, karibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nijibu swali nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi umechukua muda mrefu lakini lazima tukubaliane kwamba mwekezaji huyu *Situan* alikuwa na mkataba na Serikali kupitia *NDC*. Kwa hiyo mkataba wake lazima uhitimishwe kisheria, tukienda papara tutapata matatizo. Hata hivyo, nimpe taarifa kwamba leo hii wanakaa na tunaamini ndani ya mwezi huu mazungumzo yatakamilika. Baada ya hapo tuatajua ama twende naye au tuachane kisheria twende kwa mwekezaji mwingine, lakini tumesema kabisa kwamba kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais mradi huu lazima uanze ndani ya mwaka ujao wa fedha.

**MWENYEKIKTI:** Ahsante sana Profesa Kilila Mkumbo, Waziri wa Viwanda na Biashara kwa majibu hayo sahihi.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umeisha sasa tunaingia kwenye matangazo. Tunaanza na matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa.

Kuna wageni 12 wa Mheshimiwa Spika, ambao ni wachungaji na wake zao kutoka Jimboni kwake Kongwa wakiongozwa na Mchungaji Wilson Chigoji. Karibuni sana katika Bunge letu wageni wetu ambao ni Wachungaji na wake wake zao. (*Makofi*)

Sasa tunaenda kwa wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kuna wageni 25 wa Mheshimiwa Omari Kipanga, Mbunge Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni Wanajumuiya wa *JAI* Jamii ya *Tul Akhlaquul-Islaam* wakiongozwa na ndugu Yahaya Masao. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naambiwa Jumuiya ya *JAI* wako hapa Dodoma kwa ajili ya kuchangia damu tarehe 29 na 30 Mei na walikuwa Wilaya ya Mafia kwa huduma ya afya na wanaomba ushirikiano na Waheshimiwa Wabunge katika

haya majimbo yao. Karibuni sana kutoka JAI kwa ajili ya uchangiaji wa damu salama. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Engineer Kundo Mathew, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutoka Bariadi, Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na Ndugu Kondra Malyuta. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa *Engineer* Kundo.

Wageni 10 ni wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoka Kampuni ya *DOTTERA*, ya Washington, Marekani. Wakiongozwa na Ndg. Catherine Kahabi, Karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ali Mohamed, ambao ni Viongozi wa CCM kutoka Zanzibar Ndugu Mussa Kasim na Ndugu Ruth Panhe. Karibuni katika Bunge letu wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, Naibu Waziri wa Maji, ambao ni familia yake kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na Ndugu Winfrida Kinawilo. Karibuni wageni wa Naibu Waziri wetu. *(Makofi)*

Wageni 34 wa Mheshimiwa Tarimba Abbas, ambao ni Sekretariati ya CCM na Viongozi wa Kata 10 kutoka Jimbo la Kionondoni wakiongozwa na Katibu wa UWT Wilaya Ndugu Zahara Abdallah. Karibuni sana wageni wetu kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wa wanne ni wa Mheshimiwa Tunza Malapo, ambao ni watoto wake kutoka Mkoani Mtwara, wakiongozwa na Ndugu Kauthar Mbwana. Karibuni watoto wetu. *(Makofi)*

Wageni 25 ni wa Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wakiongozwa na Ndugu Kisaka Spemba. Karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wanne ni wa Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ambao ni familia yake kutoka Kongowe Mkoani Pwani wakiongozwa na Ndugu Gian Jimmy. Karibuni watoto wetu. *(Makofi)*

Wageni 46 ni wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalya. Karibuni sana wageni wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni saba ni wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja, ambao ni familia yake wakiongozwa na Ndugu Halima Sungi. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni watano ni wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka kutoka Taasisi ya Wanaweza ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Flora Mvungi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne ni wa Mheshimiwa Venant Protus, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na mke wake Ndugu Elizabeth Manase. Karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni watatu ni wa Mheshimiwa Zahor Mohammed ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, mke wake Ndugu Fatma Ally, watoto wake Ndugu Ilham Mohammed na Ndugu Haitham Mohammed. Karibuni sana Mke wa Mheshimiwa Zahor na wanawe. *(Makofi)*

Wageni wawili ni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Restuta Marwa na Ndugu Anusiata Komba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano ni wa Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mke wake Ndugu Levina Kikoyo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni 42 ni wa Mheshimiwa Dkt Rita Kabati, ambao ni Kwaya ya Usharika wa Mlandege, Mkoani Iringa wakiongozwa na Mchungaji Yusuph Mnyawani. Karibuni sana wanakwaya wetu kutoka Iringa. *(Makofi)*

Wageni sita ni wa Mheshimiwa Mussa Mussa wakiongozwa na ndugu Machano Ali. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Mussa. *(Makofi)*

Wageni watatu ni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi, ambao ni ndugu zake Ndugu Nusra Rashid, Ndugu Baliatu Rashid na Ndugu Zakia Yusuph. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili ni wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Ndugu Faraja Mbawala na Ndugu Rose Ngoliga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni wa Mheshimiwa Dennis Londo, ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dodoma, Ndugu Rosemary Mbele. Karibu sana ndugu Rosemary Mbele. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Mswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria ...

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Spika,

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa subiri wamalizie kusoma kidogo.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria itakayotoza au kubadili baadhi ya Kodi, Ushuru Tozo na Ada mbalimbali, Kufanya Marekebisho kwenye Sheria**

**mbalimbali zinazohusu Ukusanyaji na Usimamizi wa  
Mapato ya Umma (A Bill for an Act to Impose and Alter  
Certain Taxes, Duties, Levy's Fees and to Amend Certain  
Written Laws Relating to the Collection and  
Management of Public Revenues)**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nassor Amar, nimekuona, Mwongozo.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni 49(2) inayosema, niisome?

**MWENYEKITI:** Isome.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa; *"(1) Wakati swali linalohusika litakapofikiwa katika orodha ya shughuli, Spika atamwita Mbunge mwenye swali hilo au kama hayupo, Spika atamwita Mbunge mwingine yeyote aulize swali hilo kwa niaba ya Mbunge mwenye swali.*

*(2) Mbunge atakayelitwa atasimama na kuuliza swali, pamoja na masahihisho (kama yapo), kwa kutamka maneno yafuatayo bila ya kuongeza jambo lingine lolote..."*

Muuliza swali atasema, naomba swali langu namba fulani sasa lijibiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, naona Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kuwa tunaongeza masuala ya nyongeza mfano, nasema sasa swali langu namba fulani kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyangh'wale. Hili suala linazidi kuendelea, je, liko kwenye kanuni na kama liko kwenye kanuni, kanuni hii ilitungwa lini? Kwa sababu hapa ni kwamba ni mwisho useme swali namba fulani lipate majibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassor Amar, mwongozo wako uko sahihi na kanuni ndiyo inavyosema, kwamba haitakiwi kuongezwa neno lolote baada ya kusema Mheshimiwa Spika, sasa naomba namba fulani lipatiwe majibu. Hivyo ndivyo inavyotakiwa kwa mujibu wa utaratibu na kanuni na haijaongezwa mahali popote kanuni nyingine. *(Makofi)*

Ni kama ambavyo wenzangu ambao wanakuja kwenye kiti wanasema, tunaendelea kuvumiliana lakini itafika wakati kutakuwa uvumilivu huo haupo, tutakwenda kwa mujibu wa kanuni. Ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu. Tuendeleo.

**NDG: RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa Kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza majadiliano yetu au tunaendelea na majadiliano yetu na nitawataja watu wanne wa mwanzo ambao wataanza kuchangia. Tutaanza na Mheshimiwa Munde Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Mussa Sima, ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia Bajeti ya Serikali. Nimeisoma vizuri bajeti hii, jambo moja ambalo naweza kuwaambia Watanzania pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba Tanzania tuna bahati kubwa sana. Tumepata Rais msikivu amesikia vilio vya Wabunge, amekaa

na Mawaziri wake, vitu vyao vingi wametuwekea kwenye bajeti yetu, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mawaziri, nimpongeze Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kaka yangu Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake kaka yangu Masauni, kwa kweli wamekuwa ni wasikivu na wanyenyekevu. Wamechukua mambo yetu humu Bungeni wameenda kukaa na Amiri Jeshi Mkuu, Rais mwanamke mwenye kuandika historia ya kwanza Tanzania kwamba ni Rais mwanamke na kuleta bajeti nzuri ambayo mimi mwenyewe ikiwa ni bajeti yangu ya 11 toka nikiwa Mbunge nimeiona ni bajeti ya kipekee, nawapongeza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii imepanua wigo wa kodi, lakini imetuletea kodi za kisayansi, kodi ambazo haziumizi moja kwa moja mwananchi, kodi ambazo mwananchi anazilipa bila kuzisikia. Yote hii ni dhamira ya Rais wetu mwanamke ya kuleta mageuzi ya maendeleo ndani ya nchi yetu ya Tanzania. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi isiyolipa kodi, dunia nzima tunalipa kodi ila inategemea ni kodi za aina gani ambazo wananchi wako watazimudu. Nitoe mfano kama kodi iliyoandikwa kwenye bajeti yetu ya *property tax*, nimesikia kuna watu wanaiongelea kodi hii, wakisema kwamba kodi hii italeta mkanganyiko baina ya mwenye nyumba na mpangaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina watalaam, nyumba zetu zina hati za nyumba, kwa mfano nyumba imeandikwa Munde ndiyo mwenye nyumba, kwa hiyo watalaam hawa wataenda kufanya katika zile LUKU kama kuna LUKU tatu au nne, wataangalia nyumba hii hati ya nyumba ni ya nani, kama ni ya Munde *house rent* ya huyo *property tax rent* itafidiwa kwenye LUKU ya mwenye nyumba. Kwa hiyo niwatoe wasiwasi Watanzania pamoja na

Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wanadhania kwamba huu ni mkanganyiko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kama ikitokea kwa bahati mbaya mpangaji amekatwa *property tax rent* risiti itaandikwa kuna *property tax rent* ya Sh.3000 au Sh.2000, siku wana-*renew* mkataba wao wataiweka mezani kwamba nilichangia LUKU Sh.20,000, kwa hiyo wakati una-*renew* mkataba nitakatwa hiyo 20,000 kwenye mkataba wangu. Kwa hiyo niwaombe Watanzania na Waheshimiwa Wabunge tuzipokee kodi za kisayansi za Amiri Jeshi Mkuu mama yetu Samia Suluhu, hazitamuumiza mwananchi, unakatwa elfu moja moja, hutaisikia kama kuna kodi, lakini Serikali itakusanya mapato mengi na hatimaye kutekeleza yale mambo yote tuliyokuwa tunayataka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji trilioni 36 ili kutekeleza mambo yetu. Ni lazima tulipe kodi Watanzania, hatuwezi kuwa na nchi ambayo hailipi kodi, lakini kodi hizi ni nzuri na za kisayansi. Tuache *propaganda* ya kuzalisha maneno kwamba ukiamka asubuhi simu yako inakatwa Sh.200, simu yako inakatwa shilingi 50 siyo kweli, ukiweka *voucher*, ukiweka muda wa maongezo wapo watakaokatwa shilingi 10 ambayo kwa mwezi ni shilingi 300 kwa kuweka muda wa wapo watakaokatwa shilingi 20 ambayo kwa mwezi ni Sh.600 kwa kuweka muda wa maongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale watumiaji wakubwa wa juu wanaotumia shilingi 100,000 mpaka shilingi 200,000 labda Wakuu wa Taasisi ndiyo watakatwa shilingi 200 kwa siku watakayoweka muda wa maongezi. Akiweka muda shilingi 800 tu. Kwa hiyo jamani kodi hii haina tatizo twendeni tukalipe kodi, tukahamasishe Watanzania, Mheshimiwa Rais apate pesa aweze kuleta maendeleo kwenye nchi yetu, twendeni tukamuunge mkono Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amejipambanua kwamba yeye ni Rais mpenda haki na mimi nawathibitishia Watanzania na Wabunge, Mheshimiwa Rais

ni mpenda haki, mimi najua Mheshimiwa Rais ni mpenda haki. Pia amekuwa na *slogan* zake, anapenda kusema kwamba kazi iendelee na zege hailali, twendeni tukakusanye kodi, Mheshimiwa Rais afanye kazi iendelee na zege hailali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Amiri Jeshi msikivu, mchapakazi, mwanamama wa kwanza Tanzania, naamini ndani ya miaka yake kumi ya uongozi wake wa urais mpaka 2030 atakuwa kafanya kazi kubwa na ataacha *legacy* kubwa ya maendeleo kwa jinsi hapa alivyotunyeshwa ukusanyaji wake wa kodi, najua pesa zitapatikana na malengo yake yatakwenda kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema bajeti hii ni ya wananchi na bajeti hii imegusa watu, Mheshimiwa Rais ameenda kugusa watu wa chini kabisa kama bodaboda, walikuwa wanalalamika muda wote bodaboda, wanalalamika wapunguziwe faini muda wote, lakini Mheshimiwa Rais Samia ameenda kuwapunguzia kodi bodaboda wetu, faini kutoka shilingi 30,000 mpaka shilingi 10,000 kwa kweli vijana hawa walikuwa wanaumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesikia kilio cha muda mrefu cha Madiwani wetu kulipwa na *central government* posho zao. Leo tunaenda kuwalipa Madiwani wetu kutokea *central government*. Malipo kwa Serikali za Mitaa, mimi Madiwani wangu wamekaa miezi sita hawajalipwa posho zao, naamini sasa watakuwa wanapata kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tupate uhuru, hakuna awamu iliyowahi kulipa posho ya madaraka ya Mtendaji wa Kata na Katibu Tarafa, ni awamu hii ya Rais mwanamke Mheshimiwa Mama Samia Suluhu. Nani kama mama?

**MBUGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu ndio wanaosimamia maendeleo yetu,

wanasimamia utekelezaji wa ilani kule chini, Mheshimiwa Rais amewaona na ninaamini kazi itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais ameenda kumaliza kero ya ukamilishaji wa maboma ambayo ilikuwa inakera kwenye majimbo yetu. Tuliwahamasisha wananchi wakajenga maboma, lakini yalikuwa yamebakia wazi na wakaona kama nguvu zao zimekwenda bure. Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu amekwenda kumaliza kero ya maboma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amekwenda kuandika historia kwa kujenga shule za watoto wa kike za mabweni kila mkoa, tena za sayansi ili kupata wanasayansi wazuri wanawake. Vile vile Mheshimiwa Rais ametuwekea pesa za *TARURA*. Ameongeza Mfuko wa *TARURA* kwa shilingi mia mia kwenye lita ya mafuta ili tutokane na kero kubwa ya barabara kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikia kuna Mbunge mmoja analalamika kwamba tukipandishwa shilingi 100 vitu vitapanda bei. Hivi kero ya barabara inayoua magari yetu, inayoshindwa kusafirisha na shilingi 100, kipi bora? Tuache kuwa walalamishi. Naipongeza sana Wizara ya Fedha, nampongeza sana Waziri aliyepo madarakani na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri, lakini Mheshimiwa Mama Samia Suluhu amefanya mambo mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, namwomba sana, watakapokuwa wanakusanya hizi fedha, hizi fedha ni kwa ajili ya maendeleo. Tunaomba azi-*ringfence* ziwe kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania, zisiwe kwa ajili ya kulipana posho. Kazi maalum shilingi milioni 400 kwenye pesa hizi za kodi ya Watanzania.

Namuomba sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake ya Fedha, pesa hizi wazipeleke zikafanye kazi ya kuwakomboa Watanzania kama Mheshimiwa Rais Samia alivyodhamiria na siyo kwa ajili ya kulipana posho kwa kazi maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri sana na Naibu Waziri wasimamie hilo kwa watendaji wao. Pamoja na Katibu Mkuu kama yupo humu, hizi sio pesa za posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena na tena Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu, kwa kweli...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Munde bado dakika zako.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa suala zima la *TARURA*. *TARURA* kulikuwa na kero kubwa. Waheshimiwa Wabunge humu walikuwa wanalalamika wakisema *TARURA*, lakini ilikuwa haina fedha za kuweza kufanya kazi kukidhi mahitaji yaliyopo kwenye majimbo yetu.

Hata hivyo, kwa maono makubwa ya Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara yake ya fedha nikimaanisha Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii, wameliona hili, wameamua kuongeza pesa kwa ajili ya kuongezea mfuko huu. Wameanza kwa kupeleka shilingi milioni 500 kila jimbo hili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niwahakikishie Watanzania, tumepata Rais mzoefu, mchapakazi, tunakwenda kufanya kazi kwa bidii, tunakwenda kuandika historia, mpaka ikifika mwaka 2030 ambapo Mheshimiwa Mama Samia anakabidhi kijiti, ninaamini atakuwa ameacha *legacy* kubwa sana ndani ya nchi ya Tanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde. Tunaendelea na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Mussa Sima wajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Naomba nikiri kwamba leo ninasimama kwa unyenyekevu mkubwa kuliko siku zote nilizosimama hapa Bungeni kuchangia bajeti. Kwa nini? Mnaijua sababu. Imeletwa bajeti ya kipekee kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni kipindi changu cha tano, sijawahi kuona bajeti ya sura hii. Hii ni bajeti ambayo ni ya kipee, ni bajeti ambayo imekwenda kugusa Watanzania wote. Hii ni bajeti ya kwanza ya mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Mama Samia ni mama mwenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikwambie kitu kimoja. Mimi ninayeongea hapa ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, ngoja nisimame vizuri; ninayoongea siyo maneno yangu, haya leo nimetumwa na wananchi wa Same Mashariki. Wameniambia nije hapa Bungeni, utanisaidia nipige magoti kidogo niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nimshukuru Mama yetu Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu. Kwa nini? Jamani, sisi tangu tumeanza Bunge hili, kila Mbunge anayesimama, anazungumza *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeizungumza *TARURA* miaka mingi, jamani *TARURA* iongezewe pesa, kila Mbunge amezungumza. Sasa tabia ya akina mama iko hivi, mnisikilize vizuri. Akina mama, hata kama ana homa, amelala kitandani, mtoto akilia, mama ananyanyuka. Anamwangalia mtoto, kwa nini analia? Wabunge mmelia sana. Mama ana kazi nyingi, lakini amenyanyuka. Ana kazi nyingi sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumelalamika sana na barabara za vijijini. Mimi ni mhanga wa kwanza ambaye barabara zinanitesa, kumbukeni hotuba zangu kabla ya bajeti kuanza. Maana yake mtoto analia, ana njaa saa saba iko mbali ya chakula cha mchana, hapa katikati unamwambia kula hiki kidogo. Bajeti inaanza Julai, mama akasema jamani nimewasikieni Wabunge na ugomvi wa *TARURA*, embu chukueni shilingi milioni 500 hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaambie kitu kimoja. Jambo alilofanya mama Samia Hassan, limegusa sana wananchi. Kwangu wamefanya sherehe siku tatu kwa sababu ya barabara. Sasa naomba niwaambie kitu kimoja, mama amefanya upande wake, ametoa kila Jimbo shilingi milioni 500. Waheshimiwa Wabunge, Bunge linakwisha tarehe 30, nendeni majimboni mkazisimamie shilingi milioni 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa onyo kwa Mameneja wa *TARURA* Wilaya, hizi shilingi milioni 500 isipotee hata shilingi moja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kabisa! *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Waheshimiwa Wabunge, kasimameni imara. Kwa nini nasema hivyo? Ili tuone kitu mama alichofanya, kionekane kizima kizima, lakini mkiziachia zikidokolewa, mtakuwa mnamuumiza aliyezileta hizi pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wamenituma nisema hayo. Kwa kweli kwa ajili ya wananchi wangu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu tunaomba upumzike sasa. Wananchi sasa umewachanganya. Wananchi wamechanganyikiwa na mapenzi yaliyoota ni makubwa sana.

Tunaomba mwendo huu mlionza Serikali ya Awamu ya Sita, mwende nayo mpaka mama amalize awamu zake zote mbili. Tunawasihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa unyenyekevu mkubwa, hili la shilingi milioni 500 Waheshimiwa Wabunge tafadhali, baada ya tarehe 30 hizi safari zenu za Dubai, sijui India, sijui wapi, hapana. Majimboni, tukazisimamie hizi shilingi milioni 500. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wale ambao hawana matatizo ya barabara hawachanganyikiwi. Naomba niwaulize, tangu tumeanza Bunge hili, kuna hotuba nimesimama nisiongee barabara?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna. Kero kubwa ni barabara kwenye jimbo langu. Mama yetu amekwenda akagusa wananchi wangu kwenye mioyo. Furaha iliyoko Same Mashariki haijapata kutokea. Sasa naomba nirudi kwa Serikali niwashauri kitu kimoja. Tusichukulie mambo kiutani utani. *Let us work!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kuhusu kukusanya mapato. Ni kweli mnakusanya, lakini tunaposafiri kwenda nchi za wenzetu, tujifunze. Mimi nilikwenda China kabla hawajafunga China. Nikienda China nakaa kama siku 5, 6 au 10. Siwezi kuzunguka China mwenyewe, lazima nizunguke na mkalimani. Nikafika mahali nikawakuta wazee wanauza mahindi. Nikamwambia yule mkalimani, ngoja ninunue mhindi hapa. Akanichukulia mhindi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Nilipopewa ule mhindi, nikaula, nikaupenda. Nimepokea ule mhindi, nimeuweka mdomoni, nikamwona yule mzee anayeniuzia, anaandika kitu kwenye simu yake. Nikamwuliza yule mkalimani, anafanya nini? Akasema analipa kodi. Yaani pesa niliyolipa, tayari analipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kuna pesa nyingi sana tunaziacha. Tafuteni njia ya kukusanya pesa.

Huyu Mchina, mzee mtu mzima, akaja mtu wa pili mimi nimesimama pale, akanunua mhindi. Mzee anatoa mhindi, anaandika. Anakusanya, lakini anakusanya kodi kwa furaha, tena ana raha. Jitahidini mkatoe elimu kwa wananchi, walipe kodi bila ya shuruti. Waone raha kulipa kodi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuna jambo kidogo naomba nizungumze tofauti. Hili suala la kulipa kodi kwenye majengo rudini mkaliangalie vizuri Mheshimiwa Waziri. Huko mitaani tusidanganyane, kuna mkanganyiko. Kinachohitajika ni kwamba Waziri mkaliangalie vizuri hili jambo mliweke vizuri kwa wananchi lieleweke, wananchi wawe na raha. Hatupendi bajeti hii ya kwanza ya Mheshimiwa Mama Samia Hassan Suluhu iwe na maneno maneno huko nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika, Mheshimiwa Mwigulu nakuheshimu, ukaangalie vizuri, utakapofunga hapa ukijumuisha, Watanzania wakuelewe kwamba hii kodi anayekwenda kulipa ni nani; kati ya mwenye nyumba na mpangaji? Iwe *straight* inaeleweka, lakini tusiseme kwamba imekuwa rahisi, hapana. Sisi kazi yetu ni kuwashauri nyie. Mitaani hii kidogo imeleta mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninapiga magoti tena, nimetumwa na wale wananchi wa Same Mashariki, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. tunaendelea na Mheshimiwa Edward Olelekaita, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Sima na Eng. Stella Manyanya, wajandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Leo sauti yangu siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama walivyosema Wabunge wengine, kweli bajeti hii ni ya wananchi. Kwa hiyo, pongezi za kwanza ziende kwa

Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na za pili ziende kwa Waziri wa Fedha, mzee wa wananchi. Unajua timu ya wananchi lazima pia upende wananchi, si ndiyo bwana! Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia rafiki yangu Naibu Waziri. Hii timu imejipanga vizuri sana. Zaidi nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Bunge na Makamu Mwenyekiti na timu yote ya bajeti. Hii bajeti tunayoisifia bila shaka imepita kwenye mikono mingi sana kuanzia kwa Kamati ya Bunge, wataalam na timu nzima ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu, mimi naichukulia Wizara ya Fedha kama ndiyo *financiers*, ni kama benki hivi. Kwa hiyo, lazima *m-scrutinize* miradi yote inayoletwa, halafu mwangalie ile ambayo ina tija. Wakati mwingine nikiangalia watafiti, ningefurahi sana kama Wizara hii ingekuwa na *thinktanks* wa nchi hii wote wawekwe kwenye Wizara ya Fedha. Kwa sababu kila kitu *at the end* kinakuja kwenu; ili kuangalia baadhi ya miradi mingine na kujua kwamba baada ya miaka mitano ijayo tutaweza kutekeleza ilani ambayo tumeinadi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, pesa hizi za Watendaji Kata, Maafisa Tarafa, zimefurahisha sana wananchi kule majimboni, *big up!* Hata hivyo wakati niko kwenye shughuli za mwenge, akaninong'oneza Mtendaji wa Kata, akaniambia, waambie watukumbuke na pikipiki pia na sisi kama walivyofanya kwa Maafisa Tarafa. Hii itasaidia sana. Ni ujumbe tunawapa. Vile vile kupunguza faini kwa boda boda imewafurahisha sana wananchi, *big up!* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine nataka niweke sawa hapa. Kuna Waheshimiwa Wabunge wamekuwa kila wakisimama hapa, wanasema walipa kodi ni milioni mbili na nusu mpaka milioni tatu kati ya milioni 60, *is not true*. Shilingi milioni 60 unajua ni pamoja na Watoto! Sasa *is a bit unfair* kusema walipa kodi ni milioni mbili au milioni tatu eti kwa milioni 60 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *data* zetu zinasema, watu asilimia 68 ya *population* ya nchi hii hawalipi kodi kwa sababu ni *below age* na wengine ni wastaafu. Kwa hiyo, wakati mnasema wanaolipa kodi, *I think is good to be fair*; tunaongelea watu kama milioni 20 hivi, lakini ni kweli kama ni watu milioni mbili au milioni tatu wanalipa, tujitahidi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita taarifa. Mheshimiwa Esther matiko.

### T A A R I F A

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba ni juzi tu tulipewa semina na wataalam na hata akipitia zile *power point* walisema wanaolipa kodi ni chini ya 5% *of the population*. Sasa *population* ina-include na watoto wadogo hata waliozaliwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa tu hiyo taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa taarifa nyingine za kuambiwa na wewe unaangalia. Si ndiyo bwana! Kwa sababu na sisi ni wataalam, watoto hawawezi kulipa kodi, wale waliostaafu hawawezi kulipa kodi. Sasa mimi nasema, kwa wale Waheshimiwa Wabunge wanaosema asilimia ya watu wanaolipa kodi ni milioni mbili kati ya milioni 60, *this is what I want to correct*. Mimi sizungumzii ile 5% waliyosema hawalipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu tena, hili Bunge tumeshazungumza hapa, tukasema hili Bunge baada ya miaka mitano, tunataka tujulikane kwamba ni Bunge la wakulima, wafugaji na wavuvi, kwa sababu asilimia 65 ya

Watanzania wako huko. Mimi ninachoomba, kwa bajeti zijazo tujipange. Asilimia 10 ya mapato yetu tuwekeze kwenye kilimo. Natarajia huko mbele, tufanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Ilani ya Chama cha Mapinduzi tunafurahi sana mmeongeza hela kwenye *TARURA*, *big up!* Nasi wengine tumeshafanya hata mikutano na tumeshakubaliana hiyo hela inaenda wapi? Kwa kweli tutasimamia ili hizi pesa zisipotee. Vile vile Ilani ya Chama cha Mapinduzi huko mbele huko tulishakubaliana, tukasema ukurasa wa 71 wa Ilani hii na naomba ninukuu: “kufanya mrejeo wa mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara kati ya *TANROAD* na *TARURA*.” Ili tupate pesa nyingi kwa *TARURA* ni lazima tu-*revisit* hii *formula* ambayo tulikubaliana isiwe 30 kwa 70 tena, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane kwa bajeti nyingine zijazo huko; na kwa kuwa ni *commitment* iko kwa kwenye ilani, tusema ni asilimia kama ni 50 kwa 50 ama 60 hata iende *TARURA* na *TANROADS* kwa sababu tulishakubaliana hivyo. Hii itaongeza chanzo kikubwa kwa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamezungumza kuhusu tozo za utalii. Mheshimiwa Waziri, wenzetu jirani hapa baada ya *Covid* wao wametengeneza kitu kinaitwa *Covid-19 and Tourism in Kenya; Impact, Measures Taken, Recovery and Pathways*. Yaani wanaangalia baada ya janga hili, tukakwama, kwa sababu ni kweli hii *Covid-19* imepeleka hii sekta ya *tourism down to its knees*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, walitakiwa – na ninyi sasa muangalie *from that eye* – na hiyo *document* nitakuletea, wataalam wetu waangalie ili na ninyi muweze kutengeneza *a stimulus package, recovery package*, ili huko mbeleni tuweze kunufaika. Kwa sababu ni kweli imepeleka chini zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine; tumezungumza hapa sana kuhusu mambo ya umwagiliaji.

Na tunajua ni kweli ardhi tunayo, mvua tunapata; tusipowekeza kwenye umwagiliaji hatutaweza kumkwamua mkulima. Tuwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu bajeti hizi, nilikuwa naangalia Wizara ya Mifugo kwa mujibu wa ilani wanatakiwa wajenge mabwawa karibu 95, lakini kwa sababu ya uchache wa bajeti yao, wamepewa mabwawa matano tu. Sasa kwa miaka mitano tukiendelea na *trend* hii, baada ya miaka mitano tutakuwa tumetengeneza mabwawa 20, na tuli-*commit* kama 400 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati mwingine tunapotengeneza *plans* hizi tujaribu kuangalia. *In fact*, nilishasema wakati mwingine, na ninarudia, labda Wizara ya Fedha iangalie ilani hii *projects* zote zilizoko kwenye ilani, tufanye tathmini tujue *in terms of figures, how much projects* zote ambazo tumesema tutafanya baada ya miaka mitano tuzungumze *in terms of money* ili kila mwaka tujue kabisa tukipata bajeti hii ikaenda kwenye barabara tutaweza baada ya miaka mitano kufanya vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nilikuwa naangalia hapa kilometa za barabara kwa miaka mitano ni karibu 8,000. Sasa tusipotengeneza bajeti ya kujibu hizi 8,000 kila baada ya mwaka mmoja, tutajikuta baada ya miaka mitano tutashindwa kufanya barabara zote ambazo tumekubaliana. Lakini tuki-*cost* ilani yetu vizuri itatuongoza, itatoa mwongozo mzuri sana huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni kweli ni ya wananchi. Na hotuba ya mama Samia Suluhu Hassan mimi nawashauri sana Mawaziri muisome vizuri sana ile. Kuna miradi kabisa anataja anasema huu ndio moyo wangu – iko kwenye hotuba yake. Ni vizuri tujielekeze huko ili kiu ya mama yetu kwa Watanzania ikapate kupata suluhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja nyingine fupi sana nataka nizungumze. Imejitokeza huko mbele kuna mkanganyiko fulani; Wizara ya Ardhi wanawapa kijiji hati,

TAMISEMI wanatambua, lakini anakuja bingwa mwingine kule kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii anaanza kuwavuruga wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *concept* ya Serikali moja anayozungumza mama yetu; msipeleke *confusion* kule kwa wananchi. Ninyi mkutane humu, mnyongane wenyewe kule maofisini halafu muelewane kabla hamjaenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita, tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Sima; Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya na Mheshimiwa Anthony Mavunde wajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, mama yetu Samia Suluhu, kwa bajeti nzuri hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze kaka yangu, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, pamoja na Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Fedha, bila kuwasahau Kamati. Nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Wanakamati wote, kwa kweli wametuonesha mwanga ni wapi tunapaswa kupita kushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya bajeti hii yanatupa fursa sisi kuchangia na kuweza kuishauri vizuri Serikali. Naomba nianze na eneo la uzalishaji wa mafuta ya kula. Tarehe 13, juzi, Waziri Mkuu alikuwa mgeni rasmi pale Singida kwa wadau wa alizeti; tumefanya mkutano mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri Mkuu; mkutano ulikuwa na tija na umeleta mafanikio makubwa sana. Yapo mapendekezo zaidi ya 16 ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyatoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nijikite kwenye bajeti hapa. Serikali imeongeza ushuru wa forodha kwenye mafuta ghafi asilimia 25 yanayoingia, lakini kwenye mafuta masafi (*semi-refined and refined*) asilimia 35; ni jambo jema sana, niipongeze sana Serikali kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukumbuke huku nyuma tumekuwa tukiongeza tangu bajeti ya 2016 mpaka sasa tumeendelea kuongeza. Yawezekana lipo tatizo. Kwa nini tunaendelea kuongeza asilimia ya ushuru, kutoza ushuru wa forodha wakati huku tunajua kabisa soko la mafuta ya chakula linaendelea kudidimia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri eneo hili vizuri kidogo; yawezekana kule mafuta yanapotoka wenzetu kwenye nchi zao wanapata ruzuku ya uzalishaji na wanazalisha kwa wingi, kwa hiyo kadri tutakavyokuwa tunaweka tozo hii ama kuongeza kodi hii, inawezekana ikawa haisaidii, hata tukiweka asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike; cha kwanza, tunapoangalia *market price* inayotoka kule sisi kwetu huku inatupa changamoto. Lakini jambo la pili kwenye eneo hili, sisi lazima tu-*regulate* bei ya mafuta nchini kwetu. Na tayari tunaye *regulator* ambaye ametuonesha anafanya kazi vizuri; *EWURA* wamefanya kazi nzuri kwenye eneo la maji na kwenye eneo la mafuta ya petroli na mafuta ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati sasa tumpe na jukumu hili la mafuta ya kula ili aweze ku-*regulate market price* kwenye nchi yetu. Tunaweza tukatatua tatizo kubwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye viwanda vyetu nchini. Mwaka

1997 mpaka 2013 kulikuwa na *zero-rated*. Maana yake walikuwa hawalipi hii VAT asilimia 18. Tukaanzia hapo sasa wanalipa asilimia 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayojitokeza hapa ni kwamba mwekezaji ambaye ana *turnover* ya milioni 100 anaondolewa ile VAT ya asilimia 18. Maana yake unampa fursa yule mtu ya kujipangia bei ya kununua mbegu, na bei ya kuuza mafuta. Utawaua wenye viwanda wengine wadogo ambao hawana *turnover* hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niishauri Serikali hapa; kama tumeamua kuboresha kuhakikisha hawa wazalishaji wa mafuta ya alizeti au na mafuta mengine tuondoe VAT ya asilimia 18 kwa wawekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda nishauri sana; wawekezaji wote wa viwanda hawana mashamba darasa. Wawe na mashamba darasa, lakini wawe na mikataba na wakulima wanaozalisha mbegu ya alizeti ili kuwapa fursa wakulima hawa katika uzalishaji wao, uwe ni uzalishaji wenye tija, awe anajua kabisa anaweza kupata soko wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na Sheria ya Kilimo, hapa hatuna Sheria ya Kilimo, tuna sera. Sheria ya Kilimo inatusaidia sisi ku-*control* ardhi yetu ile, inatusaidia sisi kupima udongo kwamba uzalishaji ufanyike, unapimwa, tunaweza ku-*control* eneo hili. Sasa uzalishaji wa mafuta ya alizeti unaweza kuwa na tija kubwa sana tukizingatia maeneo hayo ambayo nimeshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limejitokeza ni Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki Sura 306. Hili ni jambo jema sana, lakini nataka nishauri kidogo hapa, kwamba kutakuwa na tozo ya shilingi kumi mpaka shilingi 10,000; jambo jema. Lakini wanaotowa ni akina nani? Maana yake wanaotumia simu wote, leo ukiangalia wajasiriamali wadogo wote; mama ntilie, machinga na

wengine wote, wanatumia simu kwa ajili ya kuendesha biashara zao. Na simu ndiyo zimekuwa mtaji mkubwa wa kuhakikisha wanahifadhi fedha zao. Leo wakiona kuna ongezeko lingine maana yake wataacha sasa kutumia simu, watakuwa wanatembea na fedha mfukoni, wengine watajaa kwenye mabenki, itakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri, la kwanza, tuweke kiwango maalum cha watu ambao wanatumia miamala hii waweze kutoa tozo hii. Kama ni shilingi 300,000 au ni 500,000, kiwango maalum waanzie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, iko fedha ambayo tunapewa tunagawiwa sisi kila mwisho wa mwezi kutoka kwenye makampuni ya simu, unashukia tu mwisho wa mwezi umepata gawio hili. Gawio hili ukikusanya uka-*accumulate* fedha zote linakaribia bilioni 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isichukue hizi fedha ambazo ni gawio linalotoka kwenye makampuni iweze kuingiza ku-*cover* hili *gap* ambalo wanalitungumzia bilioni 39, badala ya kuwa tu tunapewa fedha ambazo sisi hatujui zinatoka wapi, hata mchanganuo wake hatujui. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo ninapenda sana nilishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida Mjini pale tunayo Hospitali ya Rufaa. Ile Hospitali ya Rufaa inaendelea na ujenzi. Na ujenzi wake tayari fedha ambazo zinatakiwa kwenda kukamilisha ujenzi hazijaenda mpaka leo, zaidi ya bilioni 3.5. Na Serikali imepanga fedha za dawa, na kule kuna fedha zaidi ya milioni 700 ambazo zimeingia kwenye Mfuko wa Hazina, zinatakiwa zirudi katika uendeshaji ili wananchi waweze kupata dawa na ujenzi uweze kuendelea; mpaka sasa fedha hizo hazijaweza kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri; umefika wakati, tunahitaji fedha hizi ziende, lakini tunahitaji hizi fedha pia za ujenzi ziendeleo ili Singida Mjini tuweze kutumia majengo ya Hospitali ya Mkoa wa Singida ambayo inahamia kwenda Hospitali ya Rufaa

iliyoko Mandewa, yale majengo ya hospitali ya wilaya tupunguze gharama ya uendeshaji katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji katika miji 28; hili ni jambo ambalo tunahitaji lifanyike haraka sana. Lakini maji haya siku zote tuna-*deal* na *water supply*, lakini *water resource* hakuna. Hatuangalii vyanzo vya maji, sisi tunaangalia kusambaza maji tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unatupangia fedha za kutosha, zaidi ya bilioni 33. Nataka niishauri Serikali; sisi tunahitaji Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria uweze kufika kwa wakati. Hii ndiyo itakuwa *sustainability* ya upatikanaji wa maji kwenye maeneo yetu, badala ya kuwa tuna-*drill* maji ambayo hatujui yapo au hayapo na unaingiza fedha nyingi ambazo tunatupotezea mapato mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna posho hapa wamepewa watendaji wa kata. Lakini naomba sana tufikirie zaidi kuhusu wenyeviti wa vijiji na wenyeviti wa mtaa. Na hawa wala huhitaji Serikali Kuu itoe fedha, Serikali Kuu inatakiwa kutoa mwongozo kwenye *Local Government*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri zetu zitenge bajeti kwenye mapato yao ya ndani na kwa kiwango ambacho wanakubaliana. Kama ni shilingi 50,000 basi 50,000 kwa kila mwenyekiti wa kijiji ama mwenyekiti wa mtaa. Hili jambo litatoa fursa kwa hawa watendaji walioko chini kufanya kazi yao vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiunga mkono sana bajeti hii na niwatakie kila la heri katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja tu.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Madiwani; sisi manispaa tumeingia kwenye akaunti siku nyingi, suala la kuingia kwenye akaunti *is not an issue*. *Issue* ni kuongeza posho. Waziri atusaidie, atuongezee posho. Hata ukiongeza kalaki moja kwa kila Diwani utakuwa umetusaidia, ndio wanaosimamia shughuli zote hizi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mussa Sima. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya; Mheshimiwa Anthony Mavunde na Mheshimiwa Bonnah Kamoli wajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Taifa letu. Taifa la Tanzania limeendelea kuwa imara wakati wote. Lakini tunamshukuru zaidi kwa sababu Mwenyezi Mungu ameendelea kutupa viongozi wazuri toka kipindi cha Uhuru mpaka sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema ahsante sana Mwenyezi Mungu kwa sababu pia hata sisi waja wake tumeamua kumtumainia. Na wanasema uchaji wa Mungu ni baraka kuliko vyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo furaha sana baada ya kuona kwamba tulikuwa na kiongozi shupavu, jemedari, marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Lakini Mungu alimuonesha kumchagua mtu wa kuwa mgombea mwenza wake ambaye pengine Mwenyezi Mungu alifunga tu kauli ile ya kumwambia kwamba huyu ndio atakayekurithi, lakini alihakikisha anapata mtu ambaye ni mwenye maadili, mwaminifu, mchapakazi, mshauri sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivyo, hata ilipofikia kwenye kubadilisha uongozi, hajapata nafasi kwamba eti aende kozi ya kumfundisha kuwa Rais; kuna mahali amefundishwa jamani? Hakuna. Ameendelea kuchukua kasi ileile, ameendelea kuchukua uthubutu uleule, ameendelea kututia moyo na kuonesha kwamba Taifa liko katika misingi ileile. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, alivyoingia madarakani amejipambanua wazi akasema suala la rushwa silitaki, na sitaki kusikia... shetani na ushindwe! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandiko pia tunaambiwa kwamba rushwa ni udhalimu na utafutwa mbali, bali uaminifu utakaa hata milele. Ndiyo maana rushwa ameikataa toka asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niseme kwamba, alisema, sitaki mapato ambayo ni ya dhuluma. Na maandiko pia yanaungana na hilo, yanasema kwamba mapato ya mwovu – maana yake ukifanya dhuluma ni mwovu – yatakauka kama mto, na kama ngurumo penye mvua inayopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo yote napenda tu kuunganisha hali halisi ya viongozi wetu walivyo wanyofu, na hasa huyu sasa tuliyenaye, naye amekwenda katika mstari huohuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu amesifiwa kwa mambo mengi, lakini mimi napenda sana ile misemo yake, naifuatilia, mara kwa mara anafundisha kwa mifano na kwa misemo. Kuna wakati aliwahi kusema kazi lazima iendelee. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi iendelee. Lakini mimi naongezea iendelee na nani, na mama Samia Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuishia hapo, akasema kuwe na upepo kusiwe na upepo, jahazi lazima likafike.

Jamani mambo si haya, jahazi linakwenda kufika. Kwa hiyo, baada ya kutafakari haya nimejirejesha pia katika malengo endelevu ya maendeleo ambayo tunatarajia tuondoe umaskini kufikia 2030. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba bado kuna tofauti kubwa sana ya kimaendeleo kati ya watu walioko mjini na walioko vijijini. Ukifuatilia unakuta kwamba hata hali ya umeme bado vijijini ilikuwa iko chini, sasa hivi ndiyo tunakwenda kumaliza. Lakini hali ya maji bado ni changamoto kubwa, hasa katika maeneo ya vijijini; hali ya barabara na miundombinu mingine ni hivyo hivyo. Kwa hiyo bajeti hii inalenga kwenda kusawazisha hizi changamoto ambazo zinafanya hali ya vijijini iwe ni ngumu zaidi kuliko hali ya mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna akinamama wako kule vijijini hawajawahi kuona kituo cha afya au kujifungulia hospitali. Bajeti hii inakwenda kuondoa hayo yote; inakwenda kupunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuipongeza sana, napenda kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango, lakini pamoja na timu yake yote. Siyo rahisi kumtaja mmojammoja, lakini nawapongeza, wamekuja na bajeti iliyotulia moyo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni tofauti na wadau wengine walivyokuwa wanashauri, wanasema akiingia kiongozi mpya inabidi na yeye aache *legacy*yake, kwa hiyo, aache yale ya mwanzo yaliyotangulia aanze ya kwake, matokeo yake kunakuwa hakuna uendelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bajeti hii imejiweka wazi namna gani itakwenda kumaliza ile miradi yetu mikubwa ya kimkakati ambayo ilianzishwa na hawa majemedari wawili; jemedari wetu marehemu, na jemedari mama yetu, Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan. Na kwa misingi hiyo niseme tu kwamba hilo ndilo ambalo tunalihitaji Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala ambalo tulifanya kubwa katika kipindi hiki ni uthubutu wa hii miradi mikubwa ambayo ilikuwa inawezeshwa na fedha yetu ya ndani. Kwa misingi hiyo uthubutu ule umeendelea ambao sasa tunajipangia malengo mengine ya kuhakikisha kwamba miundombinu mingine inapatikana kwa kuhakikisha kwamba kila mwananchi anachangia katika kupata fedha hizo; hatuna mjomba, hatuna shangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hatuwezi kuendelea kuusifia umaskini au sisi kufurahia kuitwa maskini kwa sababu eti kuna mtu yuko pale pembeni atatuchangia sisi fedha zake. Lazima sasa tuondoke na tujue kwamba sisi tunao wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba tunapata fedha kwa ajili ya kuhudumia maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo hilo tunazo fursa. Fursa ninayoiendea sasa ni ya Soko Huru la Afrika ambalo tayari Tanzania tumeshasaini mkataba wake, bado kuridhia. Na ninaamini pengine Wizara husika ya Wizara ya Viwanda na Biashara mtajitahidi kufanyia kazi suala hili ili huu mkataba tuiridhie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala hili sasa linapojitokeza, niwaombe Watanzania, kuna mambo hatuwezi kuyakimbia. Ni lazima na sisi tujiweke katika mpango na mstari wa kuhakikisha hiyo fursa tunaitumia vipi. Hata kama sisi hatutataka lakini wenzetu watakuja kutumia fursa zilizopo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutawakaribisha wawekezaji kuwekeza hapa nchini basi watawekeza pembeni ya nchi yetu na sisi tutakuwa soko lao, watu wanataarifa kiasi gani kuhusiana na suala hili, mambo gani ambayo yanaweza kuwa ni vikwazo kwa hawa wananchi kuweza kushiriki kwenda katika nchi nyingine kutafuta masoko na kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu tukiwawezesha wanawake wakapata elimu ya kutosha, wanawake najua

wao siyo waoga wanauwezo wa kwenda nchi yoyote ile wakafanya biashara na ndiyo maana hata Mheshimiwa Rais amesema katika sehemu anayotaka kufanya ni kuhakikisha kwamba anawezesha wanawake kiuchumi katika kupitia majukwaa mbalimbali ya kwenye mikoa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe kwa sababu hawa wanawake ni kundi kubwa ni jeshi kubwa na lina uwezo huo na wanawake hatuogopi hata tukiamua kuolewa nchi yeyote tunaenda kuolewa huko na tunajenga mataifa huko. Kwa hiyo, hata biashara ukitaka biashara za nje zifunguke ni pale tutakapowezesha makundi haya ya wanawake. Tukifanya hivyo kweli tunaweza kufanya biashara yaani katika soko la Afrika, lakini pia tutaweza kupata maendeleo tunayo yahitaji kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. Tunaendelea na Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mheshimiwa Bonnah Kamoli, na baadae Mheshimiwa Ahmed Yahya, ajiandae.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii nami kipekee kabisa kuipongeza Serikali chini ya Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo wamekuja na bajeti inayogusa maisha na maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii kwa kiwango kikubwa kabisa imeweka mkazo mkubwa kwenye maji, barabara, na naamini kabisa wananchi wangu wa kule Mkoyo, Ntyuka, Michese *TARURA* wakiongezewa fedha hapa maana yake watakwenda kuwagusa pia na wao kwenye utatuzi wa changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba nijikite katika maeneo makubwa matatu tu, na ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu na *Engineer* Masauni, Katibu Mkuu Tutuba na Ndugu Alphayo Kidata Kamishna Mkuu wa *TRA* ninyi wanne nimewataja kwa majina mnao uwezo wa kuacha historia katika nchi yetu, mnao uwezo wa kuifanya nchi hii ipige hatua kwenda mbele, kama tu tutafuatilia ushauri wa Wabunge na kuufanyia kazi hasa katika maeneo ambayo nitayasema hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuamini sana, Mheshimiwa Naibu Waziri nakuamini sana, mnayo nafasi kubwa ya kuacha *legacy* kwenye nchi yetu. Uchumi wa nchi yetu, maendeleo ya nchi yetu yapo mikononi mwenu ni ninyi sasa muamue kuipeleka nchi hii mbele na kwa umri wenu naamini kabisa mnayo nguvu ya kutosha kulipeleka gurudumu hili mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri la kwanza ambalo nataka nianze nalo Sera ya Fedha – *fiscal policy*, Mheshimiwa Waziri lazima mipango yetu na mikakati tuliyojiwekea iendane sawa na sera zetu zinavyosema. Ilani ya Uchaguzi ya CCM inasema kuhusu ajira milioni nane, Mheshimiwa Waziri ajira milioni nane hizi zinatokea mikononi mwenu kupitia kanuni, kupitia sera na sheria katika usimamizi wa masuala ya fedha. Hakuna uchawi mwingine wowote isipokuwa hapo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuangalie namna nzuri ya kukuza uwekezaji na kuvutia wawekezaji waje nchini, hiyo ndiyo itakuwa namna nzuri zaidi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye kupatikana ajira hizo milioni nane kwa sababu ajira hizi zitatokana na kazi kubwa ambazo zitafanywa na wawekezaji wa kuja kuwekeza hapa nchini. Mheshimiwa Waziri vipo vitu ambavyo lazima tviangalie kwa haraka na kuvifanyia kazi mapema sana, lazima tuondoe tozo na kodi zote ambazo zinawatisha wawekezaji. Zipo kodi, zipo tozo ambazo ukiziondoa leo *impact* yake siyo kubwa sana na ikaathiri mapato ya nchi, lakini ukiziondoa zina mchango mkubwa kuwavutia watu,

watu wakiona makodi yamejazana wanakimbia na zipo kodi ambazo hazina mchango mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikuombe tuipitie tena sera yetu ya fedha tuziondoe kodi hizi. Kwa mfano, kwenye sekta ya utalii, Mheshimiwa Waziri hatuna haja tena ya kuendelea kuongeza tozo, wenzetu wote washindani wetu hakuna mtu kaongeza tozo. Kenya na Rwanda na nchi zingine ambazo zipo karibu nasi wanafikiri kupunguza sisi Mheshimiwa Waziri tunaongeza hii haiwezi kutusaidia ongezeko la tozo hasa katika *park fees, land base rent* itatuletea changamoto kubwa sana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri uliangelie eneo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia nashauri na kupendekeza tufanye mabadiliko ya *corporate tax*, Mheshimiwa Waziri hivi sasa kodi ya makampuni ni asilimia 30 ya mapato yanayotozwa kodi, Mheshimiwa Waziri ukiangalia Kenya ni asilimia 30, Rwanda asilimia 30, Uganda asilimia 30 nchi nyingi za Afrika ni asilimia 30, Mheshimiwa Waziri kwa nini Tanzania leo tusiishushe kodi ya makampuni kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 25 ili kuanza kuwavutia watu wengi zaidi kuja kuwekeza Tanzania, hatupotezi kitu Mheshimiwa Waziri kwa sababu hata ukiiacha mwisho wa siku haumpati mtu anayekuja nchini, umebaki na asilimia 30, lakini ukiipunguza unawavutia wengi na ile *deficit* utaipata kutoka kwenye *pay as you earn, tax* ambayo italipwa na kodi zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nashauri pia sheria itungwe kuhusiana na masuala *corporate tax* kwamba mwekezaji yeyote atakayekuja kuwekeza Tanzania akiwekeza Dar es Salaam na Pwani atozwe asilimia 25, akitoka nje ya Pwani na Dar es Salaam ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi atozwe asilimia 12.5 ili watu waende Mbinga, watu waende Njombe, watu waende Ifakara na maeneo mengine, vinginevyo viwanda vitajaa Dar es Salaam tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mheshimiwa Waziri ukienda Ghana, Ghana amefanikiwa kupitia hivi. Ghana wanayp programu inaitwa *one district, one factory* kila wilaya na kiwanda chake, wametoza asilimia 12.5 ya *corporate tax* ndiyo dunia inapoelekea huko Mheshimiwa Waziri, nikuombe Mheshimiwa naamini hili unaliweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikupe mfano mwingine rahisi sana, tukiweka asilimia 25 utawavutia wawekezaji kwa nini aende Kenya kwenye asilimia 30, kwa nini aende Uganda, kwa nini aende Rwanda atakuja Tanzania na kwetu tutakuwa na manufaa makubwa sana. Mheshimiwa Waziri hivi sasa kwa Ulaya nchi ya *Ireland* ndiyo nchi ambayo inatoza *corporate tax* asilimia ya chini sana, asilimia 12.5, hivi sasa *Facebook* makao yake makuu wamepeleka *Ireland* kwa sababu tu wamevutiwa na *corporate tax*, nakuomba sana hili eneo uliangalie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunao uwezo wa kufanya jambo kubwa sana na mimi nakuamini sana Mheshimiwa kwa sababu yapo mabadiliko yaliyofanyika hapa, tumeona yalifanyika mabadiliko ya kodi hapa, tulishusha *corporate tax* katika viwanda vinavyoanzishwa vipya vya masuala ya madawa na ngozi mpaka asilimia 20, lakini viwanda vya kuanzisha vya kuunda magari mpaka asilimia 10 kwa nini hili pia lisiwezekane Mheshimiwa Waziri naomba uliangalie hilo na ninaamini kabisa lipo ndani ya uwezo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili naomba sasa tutunge sera ya kuchukua michango ya kuchukua *remittance* kutoka katika *diaspora*. Mheshimiwa Waziri wapo Watanzania wenzetu wapo nje ya nchi ambao wana uwezo wa kuchangia maendeleo ya nchi yetu tusiziachie hizi fedha Mheshimiwa Waziri. Kwa hivi sasa kuna takribani Watanzania 1,300,000 wapo nje ya Tanzania. Mheshimiwa Waziri hawa wana uwezo wakawa wana mchango mkubwa kwenye nchi yetu na maendeleo yetu, niwaombe Serikali mtunge sera maalum ya kusaidia

kuwawezesha hawa *diaspora* kuchangia nchi yao. Mheshimiwa Waziri ukienda Nigeria, Nigeria mwaka 2018/2019 *diaspora* wa Nigeria wamechangia dola bilioni 25 katika uchumi wa maendeleo ya nchi yao ambayo ni sawasawa na asilimia 83 ya bajeti ya *Federal Government of Nigeria*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Kenya *diaspora* wanachangia dola bilioni 2.2, Tanzania ni dola milioni 430. Mheshimiwa Waziri tuwajengee miundombinu rafiki waweze kuchangia katika nchi yetu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho....

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Lugangira.

## T A A R I F A

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge Anthony Mavunde kwamba Kenya wameweka mazingira wezeshi zaidi kwa *diaspora* wetu wa Tanzania kuwekeza kwa hiyo hivi sasa *diaspora* wa Tanzania wanawekeza Kenya kuliko wanavyowekeza hapa Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anthony Mavunde taarifa hiyo unaipokea.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na nimuombe Mheshimiwa Waziri aliangalie hili ili tuweze kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu riba. Mheshimiwa Waziri jana Mheshimiwa Rais katoa maelekezo pale Mwanza maana yake najua maneno yake ni maelekezo juu ya riba, kaeni na *BOT* tunawatesa watanzania kwa riba kubwa, riba ya Tanzania ni kubwa sana,

asilimia 21, asilimia 22, nani anaweza akakopa akaweza kufanya biashara hapa Tanzania kwa asilimia hizi. Mheshimiwa Waziri kaeni na *BOT* nendeni mkaangalie hati fungani, mkakae huko asilimia kule zishuke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tuna *CRB - Credit Reference Bureau* hivi mimi nikikopa mwaka wa kwanza nimelipa, mwaka wa pili nimelipa mabenki tofauti, tofauti hivi kwa nini nikijakukopa kwa mara ya nne riba yangu iwe ile ile tena huku mmeshaona kuwa mimi ni mlipaji mzuri? Mheshimiwa Waziri hili naomba mlifanyie kazi kwa sababu vinginevyo hata makampuni yetu hayawezi kukua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kushindana na mchina anayetoka China kuja kuwekeza Tanzania anayelipa riba ya asilimia 4 *vis-a-vis* riba asilimia 21, Watanzania hawataweza kuwa washindani kwenye soko lolote la kibiashara na hasa kwenye ujenzi. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana kaeni na *BOT*, tafuteni namna bora ya kupunguza riba, riba yetu ni kubwa inawaumiza sana watanzania na hasa wafanyakazi wa Serikali, hasa Walimu ukiwaangalia, walimu wengi sana makochi yao na *TV* zao zipo kwenye taasisi za fedha. Anakopa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anthony kuna taarifa huku. Taarifa Mheshimiwa Munde, nenda kwenye *mic* sasa.

## TAARIFA

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kuhusu suala zima la riba hasa kwa vijana wetu wa bodaboda, Mama lische ambao wanakopa *Brac, Pride* zile taasisi ndogondogo wanapata riba mpaka ya asilimia 30, kwa hiyo jambo hili ni jema tuwaombe *BOT* wahakikishe wanashusha riba kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Rais.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anthony Mavunde.

**MHE. ANTHONY P. MAVUNDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili ni muda muafaka sasa Serikali muone namna nzuri ya kuweza kurekebisha hili vinginevyo tunawatesa sana wafanyabiashara wa Tanzania, tunawatesa sana Watanzania kwa sababu wengi wana changamoto nyingi. Wakienda kuchukua mkopo mwisho wa siku mikopo yenyewe hii hailipiki, lakini vilevile hata wakienda kuchukua mikopo hii kama *issue* kubwa ni ya *risk* ambayo na mabenki wanaiogopa zipo namna, wapo watalaam wengi wa uchumi, yupo hata Dkt. Kimei hapa na watalaam wengine kaeni nao wawashauri vizuri namna ya kuweza kufanya, mimi naamini haya mambo yanawezekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwenye riba huku. Naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anthony Mavunde. Tunaendelea na Mheshimiwa Bonnah Kamoli, baadaye Mheshimiwa Ahmed Yahya na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake ambayo imekuja inaleta matumaini kwa wananchi, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu wake kwa sababu hii kazi wanaiweza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa milioni 500 kwa kila Jimbo kwa ajili ya barabara zetu na mimi nimekuwa nikichangia hapa siku zote sisi ambao tunatoka Mkoa wa Dar es Salaam au na Mikoja mingine ambayo inafanya biashara au inatumia sana miundombinu, tunamshukuru sana

kwa sababu ndiyo kitu kikubwa ambacho tunakipigania.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka niongelee mradi wa *DMDP* na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mwigulu pamoja na Mheshimiwa Umy tumesha wafuata sana kuhusiana na mradi wa *DMDP*. Mradi wa *DMDP* kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni muhimu sana na hata Mheshimiwa Waziri alivyoongea kwenye bajeti yake kwamba wapo kwenye mazungumzo tulitaka tujue haya mazungumzo yataisha lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kama unavyojua baada ya Bunge hapa Wabunge wote tunaenda kufanya mikutano na wananchi wetu na maswali ambayo tutakayoulizwa ni maswali ya barabara na tuna ahadi ya kama Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam, mradi wa *DMDP* pamoja na Bonde la Mto Msimbazi. Wakati tukiwa kwenye kampeni tulihidi kwamba tutakapomaliza kampeni Bonde la Mto wa Msimbazi litaanza kutengenezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tukaahidi kwamba mradi wa *DMDP Phase II* utanza na tayari wananchi wameshaanza kuuliza na tumekaa hapa Mheshimiwa Waziri miezi mitatu tukijadili maendeleo ya wananchi, tukirudi kule inabidi twende tukawaambie, hatuwezi kwenda kuwaambia kwamba Mheshimiwa Waziri katika kusoma bajeti yake amesoma mradi wa *DMDP* utakuwepo *Phase II*, utakuwepo lini? mwaka gani wa fedha unanza? na utanza lini? ili tuweze kujua tuweze kuwaambia wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu huu mradi siyo kwamba tu upo Dar es Salaam, Dar es Salaam tunaita *DMDP*, lakini sehemu nyingine wanaita *TACTIC* kwa hiyo huu mradi upo Miji 45 nani miradi ya muhimu sana, sana Mheshimiwa Waziri tunaomba hayo maongezi ambayo yanaendelea sasa hivi yaweze kumalizika haraka ili hii miradi iweze kuanza, itatusaidia sana wananchi wa Dar es Salaam na ukizingatia Mkoa wa Dar es Salaam kama nilivyosema hapa nilisimama wakati wa bajeti ya *TAMISEMI* nikasema hatuhitaji mbolea,

hatuhitaji sijui stakabadhi ghalani, sijui vitu gani, sisi tunachohitaji ni barabara na maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo unaolipatia mapato makubwa Taifa letu, kwa hiyo ni Mkoa ambao unatakiwa kulelewa, kuangaliwa, kutengenezewa miundombinu mizuri ambayo wananchi au wawekezaji waweze kuwekeza vizuri wakiona mazingira ni mazuri pamoja na miundombinu yetu ni mizuri tutaweza kupata wawekezaji waje kuwekeza katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini kwa sasa hivi Mkoa ule haufai kabisa, barabara ni mbovu kwa sababu hata *master plan* ya Dar es Salaam ni mbovu, sasa hivi mvua ikinyesha saa moja mvua ikinyesha Dar es Salaam, kwa sababu hata stendi ya mwendokasi wamejenga kwenye mto, kwa hiyo mvua inavyonyesha tu inabidi kwanza yale mabasi ya mwendokasi wayaondoe yaani mji wote unasimama kwa mvua ya saa moja Mji unasimama kwa siku nzima hakuna biashara inayofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisimama hapa siku zote nikisema Mkoa wa Dar es Salaam tunahitaji sana miundombinu kwa sababu hiyo na sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkoa wa Dar es Salaam mvua yaani inanyesha kila siku na watalaam wetu mvua ikianza kunyesha...

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Ridhiwani.

## TAARIFA

**MHE. RIDHIWANI J. M. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mchangiaji kwamba hilo jambo lilishajadiliwa humu ndani arudi kwenye *Hansard* za mwaka 2014 kama sikosei mchango mzuri wa Waziri kipindi kile Mheshimiwa *Professor Anna Tibajiuka* unaweza kumuelezea nini ambacho kilipangwa katika mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa naipokea, lakini mpango wenyewe ulikamilika? Haujakamilika kwa hiyo mimi ninachoongea hapa huu mpango ukamilike, kama ni suala la kujadili hata mimi hapa katika miaka yangu mitano nimeongea sana kuhusu *master plan* ya Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam sasa hivi ndiyo inatuingizia mapato, ndiyo inatuingizia uchumi, yaani kila kitu kinafanyika Dar es Salaam, hakuna mtu anayeingia kutoka nchi tofauti bila kupita Dar es Salaam, lakini Dar es Salaam yenyewe ukifika tu pale *airport* ambayo ipo Kipawa, barabara yake ni mbovu, ukija kama ninavyokwambia hayo mabasi ya mwendokasi kama mgeni anakuja siku mvua inanyesha magari yenyewe yamepaki kwa sababu hata huyo mtu ambaye alienda kujenga hiyo stendi akajenga kwenye Bonde la Mto Msimbazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ndiyo maana tunasema kwamba watu wa Dar es Salaam tunaomba sana ili uchumi wetu uweze kukua ni lazima muilee Dar es Salaam nani lazima muitengenezee mazingira mazuri ili barabara zake ziweze kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zingine, kwa mfano kama kwenye Jimbo la Segerea, unakuta barabara ya kilometa tano inajengwa kwa miaka mitano. Sasa hapo utaona kweli kuna uchumi gani hapo. Mtu anachukua mzigo wake bandarini mpaka kuufikisha Chalinze masaa 10. Kwa hiyo hayo yote yanaifanya Serikali iweze kupoteza uchumi. Kwa hiyo kama wataweza kutengeneza hiyo miundombinu basi inaweza kuwapatia uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nilikuwa nataka niongee ni kuhusiana na kauli ya Mheshimiwa Rais Mama Samia. Mama Samia katika mikutano yake au *events* zake ambazo alizifanya aliongea kwamba, Manispaa ambazo zinakusanya mapato mengi au mapato kwa wingi

inabidi ziangalie barabara zake, yaani pesa zibaki kwa ajili ya kutengeneza barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kauli hii tangu Mheshimiwa Rais amesema, tunaomba basi Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuongea uende waraka wa Mkurugenzi. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais amesema, lakini tunataka tujue, ni asilimia ngapi ndiyo itabaki kwa ajili ya barabara, ili Madiwani waweze kujua ni jinsi ya kuweza kufanya mipango yao, wakakaa kwa ajili ya *ku-budget* fedha hizo za barabara, kwa sababu tangu tumelisema hapa halijafanyiwa kazi. Kwa hiyo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri pamoja na *DMDP* na hili ni mambo muhimu kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuliongelea ni kuhusiana na *diaspora*. Ili kukuza diplomasia ya uchumi, ni lazima hawa *diaspora* tuwaingize kwenye bajeti zetu. Tuwatengenezee mazingira mazuri ili waweze kuja kuwekeza. Kwa sababu hawa watu wako nje na wana uwezo wa kukutana na watu wengi kule kwa ajili ya kuja kuwekeza huku, lakini tatizo huku mazingira sio mazuri. Nilikuwa nashauri dawati la uwekezaji wawe na *special package* ya hawa watu wa *diaspora* ili waweze kuja kuwekeza kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea hapa kwenye Wizara ya Mambo ya Nje, tukasema, kwamba hawa watu pamoja na kwamba wako kule bado ni Watanzania; na kule wanafanya shughuli nyingi ambazo sisi wanaweza wakaja huku Tanzania na wakatuingizia mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu Serikali mnatafuta fedha na mnatafuta uchumi lazima hawa watu waingie, yaani muwatengenezee mazingira waje kuwekeza. Kwasababu, kwa sasa hawa watu wanataka kuja lakini hawawezi kuja kutokana na mazingira kutokuwa mazuri. Kwa hiyo nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Uwekezaji kwamba litengenezwe dawati *special* kwa ajili ya watu wa *diaspora*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nililokuwa nataka... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda umeisha, Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Ahmed Yahya, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Adamson Mwakasaka na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, wajiandae.

**MHE. AHMED YAHYA ABDULWAKIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii asubuhi ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali, ambayo mimi ninaiita bajeti mkombozi na ufunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwanza inafurahisha mno, kwamba bajeti hii ina malengo mazuri ya kututoa hapa tulipo na kwenda katika hatua nyingine, hili ni jambo la kupongezwa. Vijana wetu, Mawaziri wote, Naibu Waziri pamoja na timu yote imefanya kazi kubwa sana kuandaa bajeti hii ambayo leo mmetuletea mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza uchumi lazima kuwe na vichocheo vya uchumi ambavyo vitaufanya uchumi ule ustawi na uendeleo. Dalili zinaonesha kwamba katika kipindi kifupi tu cha mama yetu Pato la Taifa limekuwa na mama yetu ameweza kujiamini kwa kutoa fedha nyingi katika miradi mikubwa ya uchumi, ambayo italetu ufufuaji wa uchumi mzuri zaidi katika siku za usoni, hongera sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi *na-declare interest* kama ni mfanyabiashara na muwekezaji, na kwa bahati niliwahi kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwenye sekta ya biashara, viwanda na kilimo. Ni ukweli usio wazi, na niko tayari hata na Naibu Waziri kwenda kuangalia ripoti ya fedha ya urari wa biashara baina ya Bara na Zanzibar kuwa ni mbovu mno! mbovu mno! Na niko tayari wowote kwenda, kwamba asilimia 75 ya biashara iliyokuwa ikifanywa baina ya Bara, imepungua mpaka asilimia 15 na imeweza kuathiri bajeti ya SMZ kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, hiyo iko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndugu yangu tunapendana sana, Mheshimiwa Naibu Waziri tunaweza tukaenda tukaangalia namna hali ilivyoathiri biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa nini basi, Tanzania Bara *wana-influence* kubwa ya kuuza bidhaa kwetu Zanzibar; kwa mfano mbao, nondo, maji, *cement* na biashara nyingine zozote; hiyo ni *free* na hiyo ni *free trade markets*. Nchi ndogo kama yetu, ya Zanzibar yenye *population* ya watu 1,500,000 tu, sisi ukitaka tusitake tunategemea soko la Tanzania Bara. Na ukiangalia kwa upevu niliokuwa nao kwamba, hata miaka 100 nyuma, Zanzibar ilikuwa inategemea biashara (*trade*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii bajeti iliyokuja ya kuondoa ondoa vikwazo vidogo vidogo tumeifurahia na tunaipongeza. Lakini la msingi, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri naomba na hapa kidogo unitolee macho. Umefika wakati kwa makusudi na kwa malengo mazuri, iundwe tume ya fedha ya pamoja, jambo ambalo mama nalo amelisisitiza hilo. Hii yote itaondoa minong'ono midogo midogo baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, na unalijua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi mimi kwa jumla naunga mkono. Lakini la mwisho ni kwamba, katika ufanyaji wa biashara, nchi yoyote duniani haiogopi wafanyabiashara. Kwa mfano kampuni kubwa za Marekani kama vile Amazon, *Boeing* na nyingine zote, hizi zote zipo karibu na nchi au Serikali

husika. Muhimu tu zile kodi zinalipwa na wale watu wathaminiwe, pasiwe na woga baina ya wafanyabiashara na Serikali, hawa ndio wenye *engine* ya uchumi wa nchi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache mimi naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Mama amejizatiti na yuko kazini, na yote haya yatafanikiwa ikiwa tutakuwa tuna umoja na umoja wetu inshallah, Mwenyezi Mungu ataujaalia udumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Matiko, baadaye atafuatia na Mheshimiwa Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Jafari Chege wajjandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie kwenye Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla sijachangia nipende kuishukuru Serikali kwa kweli kwa kufungua mnada wa Magena uliopo Halmashauri ya Mji wa Tarime ambao ulifungwa tangu mwaka 1997, na tukawa tunakosa mapato mengi sana maana ule mnada una *multiply effect*. Nashukuru sana, na namshukuru sana Waziri wa Mifugo na Naibu wake; na hii inaenda kuongeza mapato kwenye Serikali Kuu pamoja na kwenye Halmashauri ya Mji wa Tarime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia bajeti hii kwa kweli ambayo kwa mbali imeonesha matumaini makubwa kwa Watanzania, hasa kada ya wafanyakazi. Japo wameweka tija kwa mbali sana lakini ni mwanga mzuri, ukizingatia miaka mitano yote tulikuwa hatujawakumbuka hawa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutoa tozo ya asilimia sita, ambayo ilikuwa kwenye mikopo ya elimu ya juu. Kwa kweli imeenda kutoa unafuu mkubwa sana kwa wafanyakazi ambao walikuwa ni wanufaika wa mikopo hii ya elimu ya juu. Pia, kwenye kuondoa kodi kwenye *cold rooms*, Ibara ya 57 imeonesha, hii itachochea zaidi kilimo cha mboga mboga na matunda. Kwa hiyo nashukuru sana kwa hili na kwa kweli kwa hili wanastahili pongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia Ibara ya 73 wameonesha kwamba wameondoa faini kutoka shilingi 30,000/= mpaka kuja shilingi 10,000/=, ni jambo jema. Ningependa nishauri pia kuwa wafanye tathmini, kwamba faini isiwe kwenye *uniformity*, shilingi 30,000/= kwa gari za abiria, kwa gari binafsi na malori. Kama itawapendeza pia fanyeni tathmini ya kina ili muweze ku-*charge* kulingana na aina ya gari hizo ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wamepunguza faini kuwa shilingi 10,000/=, ni jambo zuri sana kwa sababu tunaajiri vijana wengi, lakini hapo hapo wameweka kodi ya kuingiza matairi mapya ya pikipiki, ambao ni ya hawa hawa vijana. Wameondoa kutoka asilimia 10 kwenda asilimia 25; ina maana hapo mnakuwa tena hamusaidii hawa vijana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeshauri muiangalie hii, kama mnaweza mkaiacha ikabaki pale pale asilimia 10; kwa sababu hatimaye watahindwa kununua haya matairi, watakuwa wanapewa adhabu ya matairi kuwa kipara barabarani na unakuta hizi shilingi 10,000 zinajirudia mara mbili mbili, na sasa unakuta haujasaidia chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ningependa kuzungumzia kwa haraka tu Ibara za 45 na 46 ambazo zimezungumzia kuhusu madiwani, ambapo kwa kweli kwa muda mrefu ilikuwa ni kilio kwa. Vilevile mmeondoa, na kwamba mtakuwa mnawalipa posho ya mwisho wa mwezi kutoka Serikali Kuu kwa halmashauri ambazo zina kipato

kidogo; na pale pale mmeleza kwamba, mnafanya hivyo ili hawa madiwani wasipige magoti kwa wakurugenzi, lakini pia kuingeze ufanisi kwenye shughuli hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikawa najiuliza, kwamba kwa nini mnaweka *double standard*? Kuwa zile halmashauri 16 zenye vipato vya juu wenyewe waendeleo kujilipa? Sasa kama wanaendelea kujilipa hamuoni kwamba inaweza ikatokea sehemu wakurugenzi wakaacha kuwalipa kwa makusudi ili waendeleo tu kupiga magoti kwa wakurugenzi? kwa ajili kwamba wana mapato makubwa ili wawalipe. Kwa hiyo ningepomba hili mliangalie, muweke tu kwamba Serikali Kuu mtalipa kwa madiwani wote bila kujalisha kipato cha halmashauri husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mmeweka kwamba ni mapato ya mwisho wa mwezi tu. Kuna halmashauri zingine kwa mfano Halmashauri ya Mji wa Tarime kuna kipindi tulikuwa tunakopa mpaka vile vikao vya madiwani vya kati kati hapo. Yaani vile vikao vile vinavyoendeshwa vinakopwa, sasa sijui hilo mnaliangalia kiviipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusu nyasi bandia, ni jambo jema ambalo linaenda kuchochea sekta ya michezo Tanzania, lakini napingana na ninyi kuweka kwenye majiji tu. Naomba sana muondoe, muweke kwa yeyote atakayetaka kujenga viwanja kwa *standard* ya kuweka nyasi bandia, basi aweze kupata huo msamaha wa kuingiza nyasi bandia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mkoa wa Mara, tuna kiwanja cha Karume pale Musoma Mjini. Pale si jiji lakini kile kiwanja kinatumika kwenye Ligi Kuu. Tukitaka kukiendeleza kuweka nyasi bandia tutashindwa maana mtataka tulipie kodi, ilhali Dar es Salaam na hizo halmashauri za majiji ambazo mmesema zina vipato vizuri wenyewe mnawapa msamaha. Hii naomba kwanza muitumie vizuri, Shinyanga pia inatumika, na kwingineko ambako si majiji. Kwa wekeni wazi iwe manispaa, iwe mji, iwe jiji, watakaokuwa tayari kujiendeleza

kuweka nyasi bandia, basi wapate msamaha wa kodi.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kwa kweli naipongeza Serikali ni hili la kuona kwamba wapunguze muda wa mkataba kwa hawa askari polisi kutoka miaka 12 kuja miaka sita, na ikiwezekana mwende mpaka miaka mitatu kama ilivyo kwa JMTZ. Lakini hapa mmewasahau watu walio kwenye idara moja, askari magereza na askari zimamoto nao mikataba yao ni miaka 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa nao washushwe kama askari polisi, iwe miaka sita na baadaye huko muwashushe pia kuja miaka mitatu. Lakini pia, ukizingatia, kwa mfano maslahi yao, wako idara moja hawa. Askari polisi mwenye *degree* analipwa *gross salary* ya shilingi 860,000 anapewa asilimia 15 ya taaluma, anapewa na fedha ya makazi; lakini askari mwenzake aliye magereza mwenye *degree* analipwa shilingi 770,000 tu, hapewi asilimia 15 ya taaluma wala hapewi fedha za *accommodation*. Kwa hiyo naomba muweze kuwapa wawe na usawa kwa sababu wako kwenye Idara moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusiana kwa kweli na tozo ambazo *tumezi-introduce*, Ibara ya 88 ya Sheria ya Posta na Mawasiliano, ambayo inaelekeza kukata kati ya shilingi 10/= mpaka shilingi 10,000/= kwenye hizi za *mobile transaction*. Fedha hizi zinaweza kufikia takribani trilioni moja na bilioni mia mbili hamsini na nne; na wakati unasoma hapa Mheshimiwa Waziri ulielekeza kwamba zinaenda kwenye sekta ya afya. Na ikizingatiwa sekta ya afya hatujawahi kufikia Azimio la Abuja, ambalo linatutaka tutenge asilimia 15 ya bajeti kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hizi trilioni 1.25 zitaenda huko, na najua hizi fedha kwa hivi mlivyoziweka, lazima zitakuwa zinapatikana *automatically*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziweze kuwa *ring-fenced* na ihakikishwe kwamba kweli zinakwenda kwenye sekta ya afya

kama ambavyo mmetueleza hapa, isiwe kwamba mnawakata Watanzania halafu baadaye hizi fedha haziendi. Tunahitaji, mathalani tukiamua kuwekeza kwenye miundombinu katika hii trilioni 1.234 tukichukua bilioni 800 tu tunaweza kujenga vituo vya afya 2,000 ambavyo hamjavijenga mpaka leo tangu tumepata uhuru wetu. Pia tukachukua bilioni 200 kupeleka kwenye vitendea kazi, dawa na vifaa tiba vingine. Vilevile, tukachukua labda bilioni 252 tukasema tunaweka kwenye zahanati ili kumalizia yale maboma tunaenda kutatua matatizo ya vifo vya mama na mtoto, matatizo ya Watanzania wakiugua kutembea umbali mrefu na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, kwenye Ibara ya 88 hiyo hiyo kumeelekezwa fedha bilioni 322 kwenda *TARURA* ambazo zimeelekezwa zinaenda kuwa *ring-fenced*. Pia kuna bilioni 396 ambazo mmesema mmezielekeza kwenye maji. Mwaka huu wa fedha umepita zilienda tu bilioni 292. Sasa hivi bilioni 396 kama kweli zikienda kwenye maji, na kwa bajeti ya maendeleo waliyoomba ina maana kuna fedha zitabaki. Kwa hiyo tunatarajia miradi ya maji tukija hapa mwakani iwe imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 100; na zote hizi ziwe *ring-fenced*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukisoma Dhima nzima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa; unasema ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Na ukisoma pia, Ilani ya CCM Ibara ya 8, mmesema mtazalisha ajira takribani milioni nane. Ukisoma Ibara ya 13 mnajenga Tanzania ya Viwanda, ukisoma Ibara ya 14 mmesema mtatambua na kuthamini sekta binafsi kama ndiyo inayochochea uchumi wa taifa letu. Pia Ibara ya 15 mmesema kwamba mtaendelea kutambua sekta binafsi kuwa ni *engine* ya kuchochea uchumi wa taifa letu na hivyo mtalinda na kuiendeleza hii sekta binafsi. Sasa, tunaratajia muweze kuyaishi haya mambo; lakini ni kinyume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa hivi viwanda vingi vimekufa wala hata havihuishwi. Vilevile kuna mazingira yasiyo rafiki kuweza kuvutia wawekezaji waje kuwekeza

Tanzania. Sasa ili uweze kwenda na hii ambayo imeonyeshwa kwenye Ilani yenu ya CCM, ni wajibu sasa hivi, sera ya viwanda iweze kuwa *attractive* kwa *investors* ili waje kuendeleza viwanda vyetu hivi na vilevile muweze kuona vikwazo vilivyopo. Mathalani, kule kwetu Kanda ya Ziwa kuna viwanda vya pipi vilianzishwa. *La Kairo* ambaye alienda kuzindua Mheshimiwa Hayati na Jambo *Sweet*, Kenya ndio *wana-supply* pipi kutoka Kenya wanaleta huku kwa sababu wao hawana kodi kwa pipi ambazo *wana-export*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania kuna asilimia 25 kama *wana-import glucose* na sukari kuja kutengeneza pipi hapa; lakini pia wana *VAT*, kwa hiyo wanashindwa *ku-compete*. Hivi viwanda vinakufa, na Mheshimiwa Magufuli alienda kuvifungua; Jambo *Sweet* na hiyo ya La Kairo, lakini sasa hivi vinakufa na ajira nyingi zinapotea na hatima yake hata hayo mapato na na vingine mnakosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nizungumzie kuhusu viwanda vya matrela. Tunajua tulikuwa na viwanda takribani 10 hapa Tanzania, sasa hivi vimebaki vitatu tu na hivyo vitatu vinasuasua. Kwa nini? Ni kwa sababu matrela yameagizwa kutoka nje, China, *German* na kwingineko hivyo hawa hapa ndani wanashindwa *ku-compete* kwa sababu kuingiza matrela mmeweka asilimia 10 tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tulinde viwanda vyetu ili tupate na mapato nashauri tuweke asilimia 25, ili sasa kama watahitaji kuingiza hayo matrela yaweze *ku-compete* na viwanda vyetu hapa. Lakini hata hivi viwanda na vyenyewe tuvitunde, tuvisaidie, tuvipunguzie kodi. Tukitengeneza matrela hapa Tanzania tutazalisha ajira nyingi, tutapata *SGL*, tutapata *pay as you earn* na kodi zingine ambazo ni *indirect* zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kushangaza sana. Ukiangalia Tanzania hatutengenezi magari, lakini *import* wameweka asilimia 25, matrela ambayo kuna Watanzania wanatengeneza asilimia 10. Nakuomba sana Mheshimiwa

Mwigulu muirudishe, muweke asilimia 25, itaenda kuongeza mapato ya taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine mmeondoa msamaha kwenye taa za *solar* ilhali mnajua kabisa; mbali na hizi takwimu ambazo tunaziweka kwenye madaftari na kwenye vitabu Watanzania wengi kaya nyingi za vijijini hawana umeme, hawajafikiwa na umeme. Tunategemea taa za umeme wa jua, ambao bidhaa zao pamoja na kwamba huwa kuna msamaha wa kodi bado zilikuwa ziko juu sana. Sasa leo mnaondoa ilhali mnajua kabisa umeme haujamfikia kila Mtanzania kule vijijini kila kaya haina umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri warudishe msamaha kwenye vifaa vya umeme wa jua ambavyo ni ghali sana ili kuweza kuwasaidia Watanzania ambao wamejiwekeza kule. Leo kuna saluni kuna mashine sijui za kusaga, watu wanasindika na nini. Mnavyoweka mnaua kabisa uchumi kule vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba waondoe kwanza mpaka pale ambapo watakapojihakikishia kwamba kila kaya kijijini ina umeme, ndio waweke sasa hii asilimia 25 ambayo wameleta ili kusema kwamba wapate uwiano sawa. Hivi ilivyo na msamaha uwiano wa bidhaa za umeme wa jua zilikuwa zipo juu sana, ukinunua *bulb*, *wiring* yake, ukinunua *control unit panel* zake, zote zipo juu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba sana, *pump* zinazotumia umeme wa *solar* nazo pia wazipe msamaha. Zinakwenda kuchochea umwagiliaji kwa watu wa *greenhouses* huko vijijini. Ukiwa na umeme wa *solar* unasaidia, lakini pia wanaofuga samaki *and the like*. Kwa hiyo naomba sana, Mheshimiwa Waziri aangalie hili ili tuweze kuchochea sekta ya kilimo na mifugo huko vijijini katika kuhakikisha kwamba tunachochea kwenye uchumi wa Taifa hili. (*makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tuhakikishe kwamba hii miradi ya kimkakati kwa kweli inamalizika *on time*

kama SGR. SGR ikimalizika itasaidia sana kuchochea uchumi wa Taifa letu. Itasaidia sana na siyo tu kuchochea uchumi, itapunguza hata na ajira ambazo zinapatikana ambazo zinatokana kwa sababu ya malori makubwa kuchangamana na magari, mabasi na vitu vingine kama hivyo. Tukimaliza SGR kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ina maana tunakwenda kukuza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma *transport economy* itakwambia, moja ya vitu ambavyo vinasaidia na kuchochea kwenye uchumi, ni kuwa na miundombinu imara ya reli ambayo itasaidia kusafirisha. Kwa hiyo naomba sana, kama fedha tumezitenga hapa ziende tuweze kumaliza huu mradi kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema, maendeleo ya watu *it includes* elimu, maji, umeme na miundombinu ya barabara kutoka vijijini ambavyo ndio wanalima kuja huku mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa hizi dakika zangu za kuchangia. Ahsante sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Jafari Chege na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mwigulu na timu yake kwa bajeti nzuri sana waliyoiwasilisha. Kwa mara ya kwanza, mimi ni kipindi changu cha pili Bungeni hapa. Nimeona Wapinzani wakianza kuisifu Serikali. Hii ni dalili ya kwamba kwa kweli Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anafanya kazi nzuri. Muda mchache tu umemsikia Mheshimiwa Esther Matiko akizitaja Ibara, akitaja vifungu vya Katiba, akitaja Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwa

vifungu, lakini amesifu mpaka ile tozo ya asilimia sita ya elimu ya juu. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adam kuna Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu nimpe taarifa Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili, kwamba kazi ya Mbunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Ndio maana ukiapa haijalishi umetoka chama gani kwa sababu CCM ipo madarakani sasa hivi ina Ilani yao lazima tusome na niwaombe tu hizi Ilani msikae nazo kama mapambo. Kasomeni mfanye rejea muweze kuishauri na kusimamia Serikali vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tena naipokea kwa mikono miwili, kwa sababu, narudia kwa mara ya kwanza, Ilani yetu kwanza inasifiwa na upinzani; lakini inasomwa. Kila miradi ambayo tulikuwa tunaipanga na inasomwa hapa. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taarifa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa kiongozi mzoefu wa kipindi cha pili. Upinzani sio uadui ni jicho la pili la Serikali. Kazi ya upinzani sio kukubali mambo yote ambayo Serikali inafanya vinginevyo wote tungekuwa chama kimoja. Kwa hiyo nampa taarifa, wajibu wetu sisi; sisi tunagonga muhuri sehemu ikifanywa vizuri, ikifanya vibaya tutapinga na nchi yetu itasonga mbele. Nampa taarifa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado *point* iko pale pale, sasa hata taarifa zao tunazipokea kwa sababu zina mashiko. Miradi ile ya nyuma ambayo kila mradi ulikuwa ukiletwa Bungeni ilikuwa inapingwa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ridhiwani una taarifa gani tena? Haya karibu.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji hoja kwamba, shida iliyotokea hapa ni kwamba kuna mtu kasoma Biblia kuliko Mroma Mwenyewe. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mi taarifa za leo zote nazikubali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendeleo kumpongeza Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoanza. Kwa kweli sasa hili Bunge tunakwenda vizuri, hata humu ndani sasa kumetulia, zile hoja tulizokuwa tunapingana pingana hazipo, lakini wakati tunasifia, tunamsifia Mheshimiwa Rais pia kwa teuzi mbalimbali.

Nakumbuka Mheshimiwa Mwigulu wakati anasoma bajeti yake alituambia kuhusu kadi ya njano na nyekundu; kwamba mama anazo zote mbili na tumeziona. Moja imetumika juzi juzi tu na kwenye mpira kuna kadi unapewa moja kwa moja nyekundu bila kuonywa, lakini nyingine unaonywa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwenyekiti wa Maadili kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Matiko, ninapoonaa maadili yanamomonyoka huwa najisikia vibaya na hasa ya viongozi. Kwa sababu sisi moja ya kazi yetu ni kuishauri Serikali kama Bunge na sisi Kamati ya Maadili tupo pia kwa niaba ya Bunge zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mama Samia kwa kuonesha kadi nyekundu kwa Kiongozi mmoja wa Serikali ambaye ametumia ulimi wake vibaya. Moja ya maadili ya kiongozi ni pamoja na kutumia lugha ya staha. Sasa huyu mwenzetu mmoja aliweka *comedy* akazidisha akatumia lugha ambayo si ya staha, mama alimwonesha kadi nyekundu moja kwa moja. Mimi nampongeza sana na hiyo italetta heshima kwenye Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwigulu kwenye eneo ambalo alilizungumza Mheshimiwa Munde, ameongea vizuri sana kuhusu lile suala la *land rent*. Tunahitaji kodi, kodi lazima ikusanywe na ni kweli kila nchi inaendelea duniani kwa kukusanya kodi. Naomba kuna vipengele kama viwili hebu Mheshimiwa Mwigulu akaviangalie au hata atakapoanza kuhitimisha hoja yake aje atufafanulie kidogo ni kweli kuna mkanganyiko kwenye eneo fulani. Kwa mfano, kuna wazee ambao walipata msamaha wa jumla kwenye kodi. Sasa itakapoingia ile tunalipa kwenye LUKU moja kwa moja wale wazee ule msamaha sijui itakuwaje. Pia na lile eneo ambalo utakuta kwa mfano mtu kwenye kiwanja kimoja ana mita tatu ambazo zote zipo kwenye kiwanja kimoja sasa wakati analipia LUKU ile sijui kama hakutakuwa na *contradiction* nyingine yoyote, basi hiyo Mheshimiwa Mwigulu atatufafanulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa upande wa *TRA*. Wananchi wengi wangependa kuwa na kampuni wanapotaka kufanya biashara, lakini mlolongo wa namna ya kufungua kampuni, mimi ni mjasiriamali na-*declare interest*. Kwa mtu wa kawaida kufungua kampuni kuna shida. Ile milolongo ya kuanzia kujaza fomu huko, ukishamaliza

uende kwa Mtendaji, uende kwa Bibi Afya, uende kwa watu wa Chakula wa *TFDA*, sehemu mbalimbali haina shida. Hata hivyo, kuna eneo moja ambalo kabla hujaanza *process* yoyote unatakiwa ufanyiwe hesabu na mtaalam wa mahesabu. Sasa wengi unakuta kwamba hawawezi kutoa ile fedha kumpa Mhasibu ambaye unakuta gharama yake ni kubwa labda Sh.600,000 au Sh.700,000 na mtu ndio anataka kufungua kampuni. Naomba aliangalie eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sehemu ya uhakiki. Tulishawahi kuzungumza huku, sehemu ya uhakiki wa madeni ni kichaka kabisa cha kuficha vitu mbalimbali. Maeneo yale kwa mfano, natolea mfano wa mwananchi mmoja wa jimbo langu ambaye anadai toka mwaka 2014/2015 madeni yake mpaka 2020 niliambiwa kwamba ameshahakikiwa. Nikawapigia mpaka Hazina wakasema wamekudanganya, hakuna katika majina hayo, huyo hawajaleta jina lake na huyu alihudumia Ofisi ya *RPC* na maandishi yao yapo, uhakiki sasa hivi una miaka karibu saba. Wanaendelea kuhakiki kwa hiyo ni kichaka cha watu kuficha haki za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la sensa, namshukuru Mheshimiwa Mwigulu, amezungumzia suala la sensa. Naomba kwenye suala hili waje kutoa elimu ya kutosha, Tabora limetuponza. Ukiangalia kwa mfano Jimbo la Tabora Mjini alisema hapa Mheshimiwa wa Viti Maalum kuhusu ukubwa wa jimbo lile na idadi ya watu, ni tofauti kabisa. Tabora Mjini ina watu wasiopungua 500,000 inaenda 600,000 huko. Ni jimbo kubwa nilisema hapa wakati nachangia asubuhi, lina kata 29, lakini kutokana na baadhi ya watu kutojitokeza kwenye sensa, ile iliyopita hawakuweza kukidhi mahitaji ya sensa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu, huwezi kupanga maendeleo bila kujua una idadi ya watu kiasi gani. Kwa hiyo, naomba sana waje kutoa elimu ya kutosha, Jimbo la Tabora Mjini ni kubwa na pale itakapofika kugawa majimbo, Tabora Mjini wasije wakaisahau ni kubwa ina kata 29, vijiji 41, ni jimbo ambalo sehemu nyingine ukienda ni masaa mawili kwenye jimbo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la urasimishaji kwa kumalizia. Wako watu ambao waliaminiwa, kampuni mbalimbali kwa ajili ya urasimishaji kwenye ardhi. Wamekusanya fedha za wananchi; wananchi wanasubiri kupimiwa na zile kampuni zimechukua muda mrefu na sehemu nyingi hazijarasimishwa rasmi. Hizi kampuni zinaonekana nyingine za kitapeli. Serikali iangalie kama kuna uwezekano wakizigundua wazifute kabisa ili kampuni zingine ziweze kuchukua hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Adamson Mwakasaka. Tunaendelea na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Jafari Chege na Mheshimiwa Cosato Chumi ajiandae.

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya, lakini pia kwa mwanzo mzuri katika kuongoza nchi yetu katika hii Awamu ya Sita ya uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyotangulia waliomaliza kusema, naomba nitumie nafasii hii kuipongeza sana Saerikali kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameendelea kuifanya na kazi ambayo imeanzwa na ndugu yangu Dkt. Mwigulu Nchemba na *Engineer* Masauni kwa kweli inatia imani kubwa sana na kwa hakika naamini tunapokwenda ni kuzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki cha bajeti hii ambayo kwangu nailita bajeti ya kwanza ya Uongozi huu wa Awamu ya Sita, ningependa nianze kwa kuwapongeza sana, kwa sababu yapo mbapo ambayo yamefanyika au yameelezwa kwenye bajeti ambayo mimi binafsi nataka niwashawishi Wabunge wenzangu, tuunge mkono moja kwa

moja asilimia mia moja ili mambo haya yaende yakafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, lipo jambo la kuondoa ushuru katika bidhaa kwa mfano zinazotoka Zanzibar kuja Dar es Salaam. Hili jambo zuri na limekuwa ni kilio cha muda mrefu na kwa kweli sasa kimeenda kupatiwa muarobaini wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wameeleza wenzangu waliotangulia, juu ya posho sasa zinazokwenda kulipwa kwa Maafisa wetu Tawala katika maeneo yetu, kwa maana wale Maafisa Tarafa. Pamoja na hilo pia kwa ajili ya sisi wanamichezo; viwanja vya michezo kuondolewa zile tozo za nyasi bandia, kwa kweli ni jambo zuri sana. Alizungungumza juzi ndugu yangu Mheshimiwa Sanga, kwa maelezo marefu sana na sitaki kurudia huko, lakini kwa kweli ni jambo la kupongezwa na tunaishukuru sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, nigusie malipo ya wanafanyakazi kwa maana ya *PAYE*, kushusha kutoka 9% mpaka sasa 8%, hili ni jambo kubwa na ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutumia nafasi hii kuiomba Serikali yangu kwa sababu yapo mambo pamoja na uzuri wake, lakini pia yamekuwa ni sehemu ya mambo ambayo tunamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hapa, atuwekee sawa kidogo. Lipo jambo katika mapendekezo ya Serikali kwenye bajeti hii ya kwamba sasa Mahakama inakwenda kukusanya kodi. Hilo limeelezwa na lilielezwa kwa vizuri sana na Mheshimiwa Waziri, lakini mimi kwa nafasi yangu au kwa masomo niliyosoma, pia nimewahi kufanya kazi mahakamani, nikiwa kama Mwanasheria, lakini pia nikiwa mtu anayesimamia kuona kwamba haki inatokea katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi, sitaki kuamini kwanza tunakwenda kuipa kazi Mahakama ambao siyo ya kwake.

Kwa sababu unapoipa kazi mahakama ya kukusanya kodi, maana yake katika mwongozo wa yale mambo ambayo Serikali inatakiwa kufanya hili sio mojawapo. Sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa maelezo ya majawabu ya baadhi ya mambo ambayo wachangiaji wameeleza, ningemwomba aliangalie jambo na atueleze vizuri. Ni kwa utaratibu gani mahakama inakwenda kuwa sehemu ya chombo cha kukusanya kodi; maana hatari ninayoiona hapa tusije kufika sehemu mahakama ikalazimika kuwapa watu mafaini makubwa ili mradi tu waweze kutimiza malengo au maelekezo ya Serikali ambayo wamepewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia liko jambo la kivutio chetu au alama yetu *Tanzanite*. *Tanzanite* inatambulika kama bidhaa inayotokea Tanzania. Kwa mkakati ambao umefanyika na Wizara ya Madini bado naona kwamba kuna jambo moja halijakaa vizuri, kwa sababu mpaka leo tunapozungumza bado *Tanzanite* inaonekana kwamba inatokea Kenya, *Tanzanite* inatokea India na *Tanzanite* na wakati mwingine inatokea Hong Kong. Sasa kama sisi wenyewe hatutochukua *initiative* za kuhakikisha kwamba *Tanzanite* hii inakuwa *branded* ikaonekana kwamba ni bidhaa ya Tanzania; kwa kweli tunakazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hili juzi Mheshimiwa Rais wakati anazindua Kiwanda cha Kuchenjua, kama itakuwa ndio lugha nzuri, maana nisijekuwa naongea Kikwere hapa, kama itakuwa lugha nzuri hiyo, wakati anazindua kiwanda kule Mwanza, alieleza umuhimu wa Benki Kuu kushiriki katika ununuaji wa madini haya hasa akitia msisitizo katika eneo la dhahabu. Naamini kabisa, kama *Tanzanite* itatengenezewa mkakati mzuri itakuwa ni sehemu kubwa ya vyanzo vya mapato kwa ajili ya kusaidia uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia naomba sana nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwa mtu mwenye maono ya mbali. Mheshimiwa Rais juzi alizungumzia juu ya *cryptocurrency* au wengine wanasema *bitcoin* ambayo ndio *future* ya pesa za dunia hii. Tunaona

nchi kama Marekani wenzetu wamefikia sehemu sasa wanatengeneza hata sarafu zao kwa kutumia dhahabu na vito vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwangu mimi kwa wito wa Wizara, wayachukue maangalizo au maono haya ya Mheshimiwa Rais, yakafanyiwe kazi ili tusije kukutwa na sisi kama vile tupo nyuma ya muda wakati dunia imetukimbia mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo pia jambo la riba alieleza hapa Mheshimiwa mzee Sanga na mimi sitaki kurudia sana lakini ni ukweli usiofichika Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wenzake ndani ya Wizara wanayo kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba jambo hili linawekwa sawa. Watanzania walio wengi wanalalamika sana, riba zimekuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na riba kuwa kubwa sana, lakini ukopeshaji nao katika mabenki umepungua sana. Sasa inaweza kuwa kuna matatizo huko ndani ya mfumo wa kibenki, lakini kwangu niwaombe sana, Serikali iangalie jinsi ambavyo Benki Kuu inaendelea kusimamia mfumo wa ukusanyaji wa pesa ili mambo yake vizuri katika upande wa riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, lakini kwa kupitia Mheshimiwa Waziri nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kushusha baadhi ya tozo katika maisha ya vijana. Vijana wengi wao walikuwa wanalalamika sana hasa wale vijana wanaoendesha bodaboda. Juzi tulikuwa tunagawa bodaboda pale Chalinze, niliwakumbusha vijana wenzangu, kwamba hakuna jambo kubwa ambalo Mheshimiwa Rais amelifanya kama kuondoa tozo au faini za bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo naomba nirudie tena hapa hasa kuongea na vijana wenzangu wa Tanzania. Kuondolewa kwa tozo au kushushwa kwa tozo hizo, si kibali cha sisi kufanya makosa ili Serikali ituadhibu. Tuwe makini sana

na huo ni upendo wa dhati ambao Mheshimiwa Rais ameonesha kwetu sisi vijana na tutumie fursa hii kwa ajili kuhakikisha nchi inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo pia, nataka nizungumzie jambo la *TARURA*. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta shilingi milioni 500 katika majimbo yetu. Jambo hili ni zuri na kwa kweli kama ni machungu, ametupunguzia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba *TARURA* inahitaji nguvu ya ziada. Hizi pesa zilizotolewa na Mheshimiwa Rais, uwe mwanzo wa kupanga mkakati mzuri kwa Serikali kuhakikisha kwamba inaongeza fedha nyingi katika Ofisi za *TARURA* ili barabara zetu ziweze kukaa vizuri. Kwa mfano, kule Chalinze, huko iko Kata ya Talawanda ambayo kama tusipokuwa makini, kata ile inakwenda kuwa kisiwa. Hakuna njia ya kuingilia wala ya kutokea. Matokeo yake tusipokuwa makini tunaweza kujikuta mwisho wa siku nchi yetu hii inakuwa na maendeleo katika maeneo ya miji lakini siyo kule kwenye vijiji ambapo yanatakiwa maendeleo yaende; na huko ndiko bidhaa kubwa zinakozalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri, amezungumza jambo la maji, nami namshukuru sana kwa sababu Wana-Chalinze bado wanaendelea kuishukuru Serikali kwa hatua kubwa wanayoifanya. Ila namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tutakapompitishia mafungu yake hapa, pesa hizi za miradi ya maji ziende mapema ili mambo yakakae vizuri katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo hii tuna mradi kama ule unaotoka Ruvu unakwenda Mboga, bado mimi binafsi kama Mbunge mwakilishi wa wananchi sijaridhika na ile *speed* yake. Nafikiri kwamba zikipelekwa pesa na mambo yakawa mazuri zaidi tutaendelea kufanya vizuri. Siyo hilo tu pia hata kwenye miradi ya mabwawa na miradi ya

umwagiliaji nako pia tunahitaji sana fedha zifike kwa wakati ili mambo yetu yaweze kukaa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo mwisho kwa umuhimu, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano kwa kazi nzuri anayoifanya. Amezungumza na akina mama, amezungumza na vijana leo na uelekeo wake ni maelekezo kwa Serikali na kwetu sisi viongozi tunaoongoza makundi hayo kuweza kwenda kusimamia vizuri ili nchi hii anayoiongoza iweze kwenda katika mstari ulionyooka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete. Tunaendelea na Mheshimiwa Jafari Chege, baadaye Mheshimiwa Cosato Chumi na Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niungane na wenzangu kwanza kabla sijaenda mbele zaidi, kumshukuru na kupongeza kazi kubwa aliyoifanya na Rais wetu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamesimama hasa wazoefu, wengi wamekuwa wakisema hii ni bajeti ya kumi; wengine ni bajeti ya tano kwa kadri ya muda wa miaka aliyokaa ndani ya Bunge. Sisi Wabunge ambao ni awamu yetu ya kwanza tunasema hii ni bajeti yetu ya kwanza. Kipekee kabisa tunakwenda tarehe 29 kwenye Majimbo yetu tukiwa tumetosheka na tumeshiba sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo kimsingi pamoja na miaka yote hii ya nyuma hayakuwa yakifanyika, sisi ndani ya Bunge hili kwa mara ya kwanza tunakwenda kwa wananchi wetu tukiamini na tukiyaona

yamefanyika, angalau tunaweza tukasema nini Mheshimiwa Rais wetu ametutendea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru sana na pia kuwapongeza Mawaziri wote; Waziri Mwigulu Nchemba na Naibu wake pamoja na Wizara nzima, kwa namna ya kipekee walivyokaa humu ndani na kusikiliza maoni ya Wabunge. Leo hii ukiangalia upande wa *TARURA*, ni historia, haijawahi kutokea kutengwa fedha zaidi ya shilingi milioni 500 kurudi kwenye Majimbo, halafu Mbunge ukashirikishwa namna ya utendaji wa fedha ile. Haijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tangu nimeingia hapa na nimekuwa nikilia sana juu ya daraja langu la mto Mori, na nimekuwa nikisema lile daraja linaunganisha tarafa tatu kati ya tarafa nne ndani ya Jimbo, hata tarafa ya nne nayo inaingia. Leo hii ninavyochangia hapa, nakwenda tarehe 29 ndani ya Jimbo nimepewa zaidi ya shilingi milioni 950, kwa ajili ya utekelezaji wa daraja lile. Nikiongeza na shilingi milioni 500 maana yake nina *1.4 billion*, ambayo inakwenda kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema inawezekana ikawa ni bajeti ya kwanza kwa awamu hii, lakini kwetu sisi Wabunge wa mara ya kwanza kiukweli imetutendea haki na imetunyanyua sana. Pia amekwenda maeneo mengi; maeneo ya maji imegusa, maeneo ya afya imegusa, kiukweli sina namna ya kusema zaidi ya kuwapongeza Mawaziri na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu ambacho nataka nichangie leo ni kumwomba Mheshimiwa Waziri, mimi napenda sana kushauri kuliko kusifia, kwa sababu naamini nikishauri vizuri ndiyo ataendelea kufanya kazi sawa sawa na ataendelea kuwepo kwenye Wizara hii na mwishoni atatengeneza historia ndani ya nchi hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba niende ndani ya vipengele vya kumshauri ili aendeleo kufanya kazi vizuri kuliko kumsifia

zaidi. Naamini ameshafanya mengi mazuri, Wabunge wameshamsifia na anastahili sifa hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ili kuhakikisha fedha zote za miradi ya maendeleo, tengeneza historia kuhakikisha fedha zote zilizotengwa zinakwenda kwenye majimbo na kwenye Halmashauri. Ukifanya hivi utakuwa umetengeneza historia ya miaka yote ambayo tunasema zinakwenda asilimia 10 na asilimia kadhaa kwenye bajeti za kisekta. Peleka fedha zote kwenye miradi ya kimaendeleo. Amini ninachokwambia Mheshimiwa Waziri, tukirudi hapa mwakani utakuwa umetengeneza historia nzuri sana, kwa sababu miradi mingi itakwenda kutekelezwa na mwishoni wewe ndiye utakayepata sifa hizi kwa wananchi wetu ndani ya maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda sana kuchangia kwenye *Property Tax* (Kodi ya Majengo). Nishawahi kusema nachangia kama mdau. Ningependa nichangie maeneo matatu na ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri utalichukua hili, utakuja kullitolea ufafanuzi. Unakuta kwenye kiwanja kimoja, mimi mmiliki wa nyumba nimejenga nyumba tatu kwenye kile kiwanja au nyumba nne ndani ya kiwanja; nimeweka Luku moja peke yake. Maana yake mwishoni nikilipa Luku, nalipia nyumba moja. Sheria inavyosema, ni kila *property*; nyumba iliyopo kwenye kiwanja kimoja, kama ni *property* Na. 5 zile nyumba tatu zote kwa sasa zinalipia kodi ya jengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikiwa Luku ni moja kwenye eneo lile, lazima angalau utakapokuja Mheshimiwa Waziri utuambie, zile nyumba mbili zinazosalia katika tatu kwenye kiwanja kimoja, ni mpango gani mkakati uliopagwa ili angalau zote ziwe *accommodated* kwenye Luku moja ya ukusanyaji wa eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye *Property Tax* kuna haya majengo, tuchukulie nyumba za ibada ambazo kimsingi kwenye sheria ya sasa hazikuwa zinalipa kodi. Kuna wazee wa miaka 65 na kuendelea, umri wao umezidi

walikuwa hawalipo hii *Property Tax*. Namna gani sasa unaenda kuwa-*accommodate*?Kwa mfano, majengo haya ya ibada yana Luku: Je, hawatahusika kwenye Luku zao kulipia *Property Tax*? Nafikiri hii na yenyewe kwenye mkanganyiko Mheshimiwa Waziri utaiweka sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna majengo ambayo yanalipiwa na wapangaji. Mwenye nyumba amejenga, Luku inalipiwa na mpangaji: Je ni namna gani ambavyo tutawa-*accommodate* wale wapangaji ambao wananunua Luku kwenye majengo waliyopanga, wakati *Property Tax* inatakakiwa kulipiwa na mmiliki wa eneo lile (*owners*)?Haya mambo matatu Mheshimiwa Waziri naamini ukiyaweka sawa sawa hakuna kinachoshindikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nichangie sana kulingana na Mahusiano ya Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo ya Taifa, Mheshimiwa Waziri tutakubaliana, ili maeneo yote kuwe kuna uchumi imara kwa wananchi, cha kwanza kabisa, lazima kuwe na *stability*, lazima kuwe na usalama wa wale wananchi ili kufanya biashara vizuri. Nitatolea mfano ndani ya eneo langu mimi la Rorya. Mimi shughuli zangu za kiuchumi ni tatu; moja, ni kilimo; pili ni uvuvi na tatu ni ufugaji. Kilimo sina shida kwa sababu naamini kwenye bajeti ya kisekta Waziri amenitengea fedha na nitakwenda kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zinabaki shughuli mbili za kiuchumi ili wananchi wale ndani ya Jimbo waweze kwendana na kasi ya mpango wa Taifa ndani wa miaka mitano. Tuchukulie mfano suala la uvuvi. Mheshimiwa Waziri mimi kule, napenda nilizungumze kwa Waziri wa Bajeti, Waziri wa Fedha na pia Waziri wa Mambo ya Ndani na ikibidi Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kuna wizi mkubwa sana unafanyika kwenye maeneo ya maziwani. Wavuvi wanapokwenda kuvua na ndiyo shughuli kubwa ya kiuchumi. Ndani ya Jimbo langu Mheshimiwa Waziri, asilimia 77 nimezungukwa na ziwa. Unaweza kuona, ili uchumi wa

wananchi wangu uweze kuendelea, ni lazima wafanye shughuli ya uvuvi, lakini haufanyiki sawa sawa. Wanapokwenda kuvua, wanakutana na shughuli kubwa sana ya kupigwa na kunyang'anywa zana zao za uvuvi. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ikibidi Waziri Mkuu atusaidie sana kwenye hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya shughuli mbili hizo nilizosema, ya tatu ni ya ufugaji. Mheshimiwa Waziri, leo ufugaji haupo *stable*. Kule ndani ya Jimbo langu, kila siku ndani ya Halmashauri ya Rorya isipopita siku mbili, siku tatu lazima utakuta wananchi wameibiwa mifugo; na lengo kubwa la uanzishwaji wa Halmashauri zile mbili, mpaka ikafikia sehemu ikatengenezwa Polisi ili kuhudumia maeneo haya yote mawili, haipo sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninavyozungumza, jana wananchi toka asubuhi mpaka saa 8.00 wanazunguka kutafuta mifugo yao ambayo imeibiwa. Uanzishwaji wa kanda maalum ndani ya ile Halmashauri kwa maana ya Tarime na Rorya, ilikuwa ni kuhakikisha angalau kuna usalama kwanza wa hizi Halmashauri mbili, lakini nisikufiche ningetamani sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alichukulie *serious* suala hili, kwa sababu kule imekuwa ni kero kubwa sana. Leo Mheshimiwa Rais akienda au Waziri Mkuu, amini ninachokwambia, bango la kwanza atakalokutana nalo ni suala la wizi wa mfugo. Imekuwa ni suala la kihistoria, limekuwa la miaka mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa unyenyekevu mkubwa, watafute mbinu za kukomesha hili suala ili angalau wale wakazi wa Rorya ambao kimsingi wameamua kuhamasika kwenye kuingia kwenye shughuli za ufugaji, wafuge mifugo yao, kama ni ng'ombe ikiwa ni salama kabisa bila kuingiliana na huu msugvano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwa sababu bila ya kufanyika, haya ndiyo yana mahusiano na mwingiliano wa ukuaji wa kiuchumi wa wananchi wangu. Kama utakutana na *disturbance* kwa maeneo haya mawili,

maana yake kila mwaka watakuwa wanakwenda na bado watakuwa wanarudishwa nyuma, kwa sababu mtu anajikakamua, anaanza kufuga ng'ombe wawilia au watatu; na mwingine wale ng'ombe ndiyo anaotumia kulipa ada ya watoto wake. Mwingine wale ndiyo wanazitumia angalau akipata shida kuuza na kuingia kwenye shughuli zake za kiuchumi na kujiendesha katika maisha yake. Halafu haifiki mwisho, wale ng'ombe wanakuja kukwapuliwa, anaanza upya yule mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sana, Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa sababu nimeshafuatilia kwa muda mrefu, walichukue walione ni namna gani angalau wanalitatu ili wananchi nao waweze kujikwamua kwenye suala hilo la kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege. Tunaendelea na Mheshimiwa Cosato Chumi, Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Yahaya Massare wajandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais nikiwa kama mtu ambaye nimekulia sehemu ya maisha yangu Wizara ya Mambo ya Nje. Mheshimiwa Rais ndiye mwanadiplomasia namba moja. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amethibitisha kwa vitendo kuwa mwanadiplomasia namba moja; kwanza, kwa ziara zake za Kenya na Uganda. Nilishasema hapa, kule Kenya imesaidia sana ziara ile kufungua milango hasa kwa sisi ambao tunalima mahindi, lakini pia Kenya nasi tunafanya biashara nyingi mbalimbali. Nampongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Mheshimiwa Rais pia ameendelea kuzungumza na kushiriki mikutano mbalimbali *online* ya Kimataifa. Ameshazungumza na

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha Duniani, pia amezungumza na Rais wa Benki ya Dunia, amezungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia, hayo ni sehemu ya ule udiplomasia namba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa nini? Kwa sababu ukienda katika bajeti yetu, katika "C" na "D", ambayo inaelezea kwamba sehemu ya bajeti yetu itatokana pia na misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo na mikopo ya ndani na nje. Takribani shilingi trilioni saba itatokana na mikopo pamoja na misaada. Sasa ili upate mikopo hii na misaada ambayo inatengeneza asilimia 20 ya bajeti yetu, ni lazima uaminiwe na uaminike Kimataifa. Vinginevyo huwezi kupata. Hili Mheshimiwa Rais amelithibitisha kwa vitendo kwa haya ambayo nimeyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile haitoshi, Tanzania imechaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa utakaofanyika mwezi Septemba. Katika kuchaguliwa huku, ilipita bila ya kupingwa. Kwa kuweka *record* sawa, mara ya mwisho Tanzania ilikuwa Makamu wa Rais mwaka 1991 na pia imewahi kuwa Rais wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika Mkutano wake wa 34 Mwaka 1979 wakati wa Salim Ahmed Salim.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu gani? Kama nilivyosema bajeti yetu asilimia 20 inategemea misaada na mikopo ya riba nafuu. Sasa katika hili, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yako kwa ujumla katika Serikali. Bajeti mliyotuletea kama walivyosema wenzangu ni bajeti kweli ya wananchi, lakini katika haya Mheshimiwa Rais, ambayo anayafanya kama mwanadiplomasia namba moja, yako ambao sisi kama watendaji katika Serikali tunao wajibu ya kuyafanya ili tusimwangushe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona katika maelezo yako ya bajeti Mheshimiwa Waziri, umeelezea masuala ya mikopo ya riba nafuu na misaada. Masuala haya

Mheshimiwa Waziri yanakwenda na *terms and conditions*; masharti na vigezo lazima vizingatiwe. Sasa nakuomba na timu yako ya wataalam, katika kufanya majadiliano, tuzingatie sana *terms and conditions*. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana ambapo tumekusumbua sana mimi na wenzangu wa miji 45, wakiwemo akina Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Mabula. Kwa kweli umekuwa msikivu na umelielewa lile jambo na umetuahidi hapo upo katika mazungumzo ya hatua za mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile jambo litakwenda kusaidia miji 45, siyo katika ujenzi tu wa miundombinu kwa maana ya barabara, pia unaenda kuisaidia miji hii na Halmashauri hizi katika kujenga vitega uchumi ambavyo vitakuwa ni vyanzo vya mapato. Kwa mfano, sisi Mafinga, mojawapo ya mradi ambao tumeuainisha ni kujenga soko kubwa la mazao ya misitu. Kwa maana ya kwamba katika SADC Kusini mwa Afrika, soko kubwa la mbao, milunda na nguzo, live pale Mafinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri na timu yake, tuharakishe jambo hili ili liveze kuanza kwa wakati. Pia kwa kutoa mfano tu, mradi wa maji wa miji 28 ambao ni mkopo wa fedha wa riba nafuu kutoka India *is not a grant* ni mkopo ambao tutaulipa. Tunapozungumza hapa ni mwaka wa sita haujaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ule udiplomasia namba moja wa Mheshimiwa Rais, yeye anatufungulia njia, nasi sasa ni wajibu wetu katika kufanya majadiliano, tuhakikishe hayo majadiliano yanazingatia *terms and conditions*. Kwa sababu tukimbana Mheshimiwa Waziri wa maji katika mradi wa miji 28, anasema kwamba bwana, kuna masharti ambayo kwa kweli ilibidi tukae upya na kuanza kuyafikiria upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tusimwangushe Mheshimiwa Rais, kama mwanadiplomasia namba moja. Ameshatutengenezea njia, sisi wataalam

tunapokaa kujadiliana katika kuhitimisha hayo masuala ya mikopo na misaada, basi tuzingatie sana *terms and conditions* ambazo zitakuwa *in our favor* kama Taifa. Nitazungumzia pia kuhusu *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na timu yake kwa kutushirikisha sisi Wabunge (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za usafirishaji katika nchi hii hazitokani na kuwa na bei ya mafuta, gharama za usafirishaji zinatokana na ubovu wa barabara. Tukienda kukabiliana na kuhakikisha kwamba tunaondokana na ubovu wa barabara, gharama za usafirishaji zitapungua. Nitatoa mfano, kutoka Mafinga kwenda Mdaburo wakati wa mvua ambapo ni kilomita zisizozidi 50, nauli ni shilingi 10,000, lakini kutoka Dodoma kwenda Iringa ambako ni kilometa 260 nauli ni shilingi 10,000. Kwa nini kilomita 50 nauli ni shilingi 10,000 sawa sawa na kilomita 260? Ni kwa sababu barabara ni mbovu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokuja na huu mpango wa *TARURA*, tukimshukuru Mheshimiwa Rais na hizo shilingi milioni 500 ambazo mmetushirikisha Wabunge kwa kiasi kikubwa, na hii fedha ambayo tunaipendekeza kwenye tozo za mafuta, ushauri wangu na ombi kwa Serikali, ikawe *ring-fenced* ili ikatuondolee kero ya barabara. Kutoka Mafinga kwenda Mgololo kilomita 80, sana sana unachoweza kufanya ni kukodi gari ya shilingi 100,000 ili ikupeleke, kwa sababu basi likienda na kurudi hizo gharama za matengenezo ni kubwa kupindukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti na waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tukubaliane hii tozo ipite, lakini iwe *ring-fenced* kwa sababu inaenda kuwa mkombozi wa barabara. Gharama za nauli toka naingia hapa Bungeni; kutoka Iringa kwenda Dodoma, nauli ya basi imebaki ile ile kwa sababu barabara inapitika *throughout*. Kwa hiyo, ubovu wa barabara ndiyo chanzo cha gharama kubwa za usafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, juzi amesema kuhusu Mchuchuma na Liganga. Hivi Rais akishasema, nini kinafuata? Ni utekelezaji. Kama tungeweza kupata kile chuma, hata hii reli ya *SGR* tunayojenga, wataalamu wanasema gharama zake zingepungua kwa asilimia 50. Siyo tu chuma na makaa ya mawe, kuna madini mengine. Naomba Mheshimiwa Waziri na timu yako jambo hili Mheshimiwa Rais ameshasema, sisi watu wa nyanda za juu kusini, itakuwa ni mkombozi mkubwa wa uchumi, italeta *speed of effect*, katika uchumi siyo tu Mikoa ya nyanda za juu Kusini na Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ukisoma bajeti, maeneo yote Mheshimiwa Waziri anasema, "napendekeza." Kwa hiyo, niwatoe shaka wananchi. Wengi wamesema kuhusu Luku kwamba wapangaji watalipa; wengi wamesema kuhusu tozo zilizopendekezwa kwenye miamala ya simu na namna ya kulipa gharama za simu; niwatoe hofu wananchi, kazi yetu Wabunge ni kuishauri Serikali na baadaye masuala haya kabla ya kutekelezwa, yatakuja kwenye Sheria ya Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasi kama ambavyo bajeti ikisomwa tunapewa siku moja ya kuitafakari, pia na wananchi nao wanaitafakari. Nasi humu ndani tunatoa maoni yetu kutokana na *feelings* za wanachi ambao tumeshaanza kuziona. Lengo ni mwisho wa siku kukusanya mapato. Kukusanya kwa namna gani? Ndiyo wajibu wetu na wataalamu wetu wa uchumi waweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, napongeza sana suala la nyasi bandia. Nakuomba Waziri, wewe ni mwana michezo, isiishie *level* ya Jiji. Nakuomba pia Mheshimiwa Waziri ile 5% ambayo itapatikana *Sports Betting*, umesema kwamba itaenda kukuza sekta ya michezo. Hata hivyo, nina angalizo, kusema kwamba nani ata-*determine*, kwamba *TFF* ndio ata-*determine* mtu atakavyokuwa ameomba nyasi bandia zije kwamba ana-*qualify* au asi-*qualify*, hapana. Nashauri jambo hili liachiwe *BMT*. (*Makofi*)

Mheshimwa Mwenyekiti, kiwango cha kuaminika cha *TFF* siyo kikubwa kama unavyodhania. Mheshimiwa Waziri kwenye hili naomba *BMT* ndio wapewe hiyo *mandate* ya kwamba kama ni Halmashauri imeomba, kama ni Jiji limeomba au kama ni taasisi au shule fulani imeomba, Baraza la Michezo la Taifa ndiyo liseme kwamba huyu apewe ama asipewe, lakini hii ambayo katika uchaguzi tu unaenda kila Mkoa, wadhamini washachukuliwa ndiyo uwape dhamana ya kwamba watupendekezee kiwanja gani kijengwe au kisijengwe, hapana. Napendekeza hiyo ibaki kwa Baraza la Michezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nasema nawasalimia kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Kazi iendelee.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mungu awabariki sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cosato Chumi. Tunaendelea na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Yahaya Massare na Mheshimiwa Constantine Kanyasu wajandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa utaratibu iliyochukua wa kutoa fedha shilingi 500,000,000 kwa kila jimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu nauona una tija zaidi tofauti na ilivyozoeleka. Kwa upande wa Jimbo langu la Bahi, shilingi 500,000,000 hizi zimenisaidia kutatua changamoto kubwa ya barabara inayotoka kwenye Kata ya Chifutuka ambayo iko kilometa 90 kutoka kwenye Makao Makuu ya Wilaya na wakati mwingine imekuwa inajifunga haipiti. Lakini kwa 500,000,000 hizi tulizozipata tunaenda kutatua kwa kiasi kikubwa tatizo hili la barabara na hatimaye kuweza kuleta maendeleo ya wananchi kupitia kata ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niipongeze sana Serikali. Bajeti hii ina ahueni kubwa katika kuleta maendeleo lakini pamoja na hilo, tunakuja kwenye matumizi ya bajeti. Bajeti yetu imekuwa mara nyingi haifiki asilimia 70 katika matumizi hususan katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hasa Wizara wa Fedha aelewe na atambue hili kwamba bajeti yetu iwe ni *rural centered development*. langalie zaidi katika kutatua shida zaidi za wananchi walilopo vijijini na kwa kweli tuna shida kubwa sana vijijini. Tuna shida ya zahanati, kwa mfano Jimbo langu la Bahi sina zahanati 16, sina *ambulance*, hata *ambulance* zinazokuja ugawaji wake bado haueleweki. Ukigawanywa kama hivi tulivyopewa 500, 500 italeta ahueni. Kwa hiyo, nadhani hii *model* iliyotumika ya 500,000,000 tuiangalie katika bajeti iweze kutumika katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya bajeti kupitishwa imekuwa tunasubiria kudra za Hazina ndiyo ziweze kutupatia katika maeneo yetu. Wakati mwingine unasikia upande fulani wamepewa, huku kwako hujapewa, kigezo hakieleweki. Ili twende sawa sawa, kuwe na *equal distribution*, ni lazima tuone namna gani. Kama tunaamua kutoa milioni 600 kwa ajili ya kumalizia maboma kwenye majimbo yote, ziende kote. Namna hii tunaweza tukaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishie pale kwenye *conclusion* ya Waziri wa fedha kuhusu kadi ya njano na kadi nyekundu. Maneno yale yana busara kubwa ya kuonesha namna gani kiongozi wetu wa Taifa hili alivyosheheni uzoefu wa kuweza kulliongoza Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hivyo tu ni kwamba Mheshimiwa Samia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Chama hiki kina utajiri wa rejea katika uongozi. Ni chama ambacho kimepita katika vipindi vingi tangu kuanza mapambano ya uhuru lakini baada ya nchi yetu kupata uhuru. Lakini, hata hivyo vile vile kupambana na mifumo mbalimbali ili kujiletea maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama chetu cha Mapinduzi kimekuwa kinafanya *reform* kila wakati. Iwe katika kipindi kile sasa tunaanza kuimarisha viwanda Watanzania tuweze kujitegemea. Lakini hata hivyo, tuwe tumekuwa tunaangalia tunaenda na sera gani, tunajibadilisha kila mara kutokana na matakwa ya jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kutoa Sera za CCM katika miaka ya 90. Lengo letu lilikuwa ni namna gani sasa tunaanza kwenda katika mageuzi ambayo yanatokea katika Dunia na sisi tuweze kuendana na namna Dunia inavyoenda. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Watanzania, Mheshimiwa Samia anarejea kubwa ya uongozi na ninataka niwaambie hakuna shaka ya kuwa na wasiwasi kwamba Mheshimiwa Samia hatalivusha Taifa hili. Atafanya vizuri zaidi kwa sababu ana msingi mkubwa ambao msingi umetengenezwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetokea kasumba ya baadhi ya Mwenyekiti wa chama kimoja kuonesha kwamba kama ana kauli ya kuweza kulazimisha kila anachotaka yeye. Nataka tu niseme kama nilivyosema Samia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi. Mwenyekiti huyu ambaye kidogo anataka kujipa ahueni kwamba eti anataka kuja 25 ashike dola alianza tangu enzi za Mzee Mkapa, Mzee Mkapa akaondoka yeye bado ni Mwenyekiti, akaja Mzee Kikwete yeye bado Mwenyekiti, amekuja Hayati Magufuli yeye bado Mwenyekiti. Sasa mtu ambaye amekosa pumzi kabisa amechoka hoi bina taaban anataka kuja kupambana na Mwenyekiti ambaye ni mpya kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia Mwenyekiti wetu ni Mwenyekiti ambaye ameonesha, Rais wetu ameonesha ni mtu anayejua hata Dunia inavyoenda. Ninyi mmeshuhudia hata mitazamo yake, juzi amesema kwamba sasa Taifa letu liangalie kuna mageuzi makubwa sana ya kidijitali yanatokea. Sasa hatuwezi kubabaishwa na Mwenyekiti huyu ambaye ni Mwenyekiti wa enzi na enzi, amekosa mvuto, amepauka na anajinasibu anasema wao

ni makamanda. Kwanza nataka niwaambie, sisi tulikomboa nchi nyingi za Afrika katika kupigania uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameanza kuvaa makombati hayo wanayoyavaa sisi tunawaona. Sisi tulishapigania uhuru na chama chetu kina heshima kubwa katika Bara la Afrika na ninataka niseme Mheshimiwa Samia sio wa kufanyiwa mashinikizo, yuko kwenye chama imara, anajiamini na nataka niseme tunaendelea kusonga mbele.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare na baadaye Mheshimiwa Mwanakhamis ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii nichangie katika bajeti hii kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama Samia Suluhu Hassana aliyepokea kijiti kwa Dkt. John Pombe Magufuli, Hayati mpendwa wetu ambaye alitutoka pasipo sisi kutaka lakini kazi ya Mungu huwa haina makosa mara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu mpendwa sana, sana kabisa mama yetu ambaye juzi tu ameonesha namna gani wanawake kuwa ni *tea bags* ambazo lakini bila maji ya moto haziwezi kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa jinsi ilivyotufanyia vizuri katika Majimbo yetu. Jimbo langu ambalo nimekuwa mwakilishi kwa vipindi viwili, limefanyiwa mambo mengi sana na Serikali yake chini ya Dkt. John Pombe Magufuli lakini sasa mama Samia Suluhu Hassan ameenda kuongezea kutuletea shilingi 500,000,000 kwa ajii ya kuboresha miundombinu iliyokuwa imechakaa katika barabara zetu za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ni kiranja wa Serikali na kiongozi wa Serikali katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano kwa jinsi alivyopokea mawazo ya Wabunge hususan katika kilimo cha alizeti na hivi juzi tu alikuwa Singida akizungumza na wadau mbalimbali juu ya kilimo cha alizeti ili kuondoa pungufu hili la mafuta ya chakula ambayo tunaagiza kutoka nje kupitia alizeti naamini kwa mikakati ambayo inapangwa sasa inaweza ikasaidia sana mikoa hii mitatu ambayo imewekwa kimkakati kuweza kulima alizeti zenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii hajia-*reflect* sana kwenye kilimo lakini tafiti za mbegi ambazo zinatakiwa ziende zikalimwe katika mikoa hii mitatu ya Simiyu, Singida na Dodoma zinafanyika katika mikoa ambayo ina mvua nyingi. Niombe Wizara ya Kilimo ikiwezekana, tafiti za mbegu za alizeti ambazo zitalimwa katika mikoa hii mitatu zikafanyike katika miongoni mwa mikoa hii mitatu. Mkoa wa Singida uwe kielelezo kwa sababu ndiyo waanzilishi wa zao hili na mbegu za kulima alizeti zikalishwe katika Mkoa wa Singida ili kuonesha matokeo chanya ya alizeti ambayo yatakuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa katika kilimo hapo hapo, Serikali inatakiwa iongeze nguvu kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji. Tutengeneze mabwawa kuinga mito ambayo inapeleka maji katika mito, maziwa, mito inayopeleka maji katika mabwawa kama hili hapa Suruingai – Bahi na mito mingine ambayo iko katika mikoa hii ya katikati ambayo ni mikoa kame tuweze kupata kilimo cha umwagiliaji *scheme* nzuri kama iliyopo *scheme* ya Bahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Singida nasi tunayo mito hata katika Jimbo langu. Niombe watu wa kilimo waje wafanye tafiti tuone ni eneo gani tunaweza tukaongezea hasa upande wa Jimbo ambalo natoka. Tuna *scheme* moja tu ya umwagiliaji ambayo ni *scheme* ya Itagata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mifugo, mikoa hii ambayo inaenda kulima alizeti, mashudu ya alizeti baada ya kukamuliwa ni chakula bora sana kwa mifugo. Wizara ya Mifugo nayo ije na mkakati wa kuhakikisha tunapata malambo ya kunyweshea mifugo yetu hasa katika Jimbo ambalo natoka limekuwa na wafugaji wengi, wengi wametoka kanda ya ziwa kwa sababu sisi tulikuwa tuna nafasi kubwa wamekuja kupata fursa ile ya majani na eneo pana la kuchungia mifugo. Tuna tatizo kubwa la malambo, lakini na majosho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hiyo ya Waziri Mkuu, nimpongeze sana Mheshimiwa jenista Mhagama kwa kazi nyingi na nzuri sana ambazo amekuwa akifanya katika Wizara hii ya Sera, Bunge, Vijana na watu wenye Ulemavu. Taasisi zilizo katika Wizara hii, mfano Taasisi ya *OSHA* ilikuwa ni kero kubwa sana kwa watu wenye viwanda, kulikuwa na tozo nyingi hasa unapoanza ujenzi wa jambo lako lolote *OSHA* walikuwa ni kikwazo. Leo wamepunguza tozo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii ya Bunge lako tukufu kuwapongeza *OSHA* lakini na kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kazi nzuri aliyofanya na kufanya sasa zile kero nyingi ambazo zilikuwa zinatokana na Taasisi hizi sasa ziweze kuwa ni changamoto ambazo zimeanza kuisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini taasisi nyingine iko chini ya Wizara hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Taasisi ya *WCF*, miongoni mwa Wabunge ni mashahidi jinsi walivyopata kupata *compensation* kwa matukio mbalimbali yaliyowapata ni mmojawao ambao nilifidiwa baada ya kupata ajali mbaya ya gari kupitia Taasisi hii ya *WCF*. Kwa hiyo, nichukue fursa hii

kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama na Wizara yake na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Naibu mawaziri waliopo katika Wizara hiyo kwa kazi nzuri ambazo tumeendelea kuziona zikionekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu huwezi kuzungumzia jambo lolote bila kuzungumza barabara. Sisi watu wa Mkoa wa Singida tunaunganishwa na Mkoa wa Mbeya kupitia barabara ambayo inapita katika Jimbo langu na ni barabara pekee ambayo imebaki ina urefu mkubwa. Ina kilometa 412. Katika kilometa 412, kilometa 219 ziko ndani ya Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa kuonesha nia ya kujenga kilometa 56.9 japo zimetangazwa kilometa 25 lakini kwa kilometa 25 maana yake itatuchukua zaidi ya miaka 20 kumaliza hizo kilometa 412. Niombe sasa Serikali ichukue juhudi za maksudi kuongeza kipande cha barabara cha kutoka Mkiwa – Rungwe, zile kilometa angalau zifikie kilometa 100 tunazozijenga kipindi hiki ili wananchi hawa nao waunganishwe na mtandao wa barabara, waweze kukimbizana na hali hii ya uchumi, waweze kuwa walipakodi wazuri lakini mazao yao yafike katika masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida pia unaunganishwa na Mkoa wa Simiyu kupitia daraja la Sibiti. Haijaonekana popote katika Bajeti ya Serikali, Bajeti ya Wizara ya Ujenzi kwamba mnaenda kuanzia wapi. Niombe sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, Waziri wa Fedha unatoka Singida, uone watu wa Singida wanavyoweza kuunganishwa na mikoa mingine. Usije kuwa mpishi alilia kwenye... itoshe hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja mahsus ambalo nilikuwa nataka nizungumzie. Hapa katikati kulikuwa na ugaidi mkubwa katika hifadhi zetu na mapori tengefu. Watu wanaomiliki silaha hasa bunduki aina ya *rifle* walifika mahali ukisalimisha silaha ile unasafiri basi huwezi kuichukua tena lakini ukiuza silaha yako au ukinunua silaha kwa mtu mwingine au mtu aliyekuwa anamiliki silaha akafariki, warithi

wake sasa hawapati vibali vya kumiliki silaha. Ni nini tatizo? Mtuambie zimepigwa marufuku? Silaha hazihamishwi? Hasa *rifle*, zote kuanzia 22 mpaka 458.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali basi ije na matamko ya kuonesha kwamba hwa watu wanaotaka kumiliki silaha kwa njia nzuri wanapata kumiliki silaha. Ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Serikali. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Massare, tunaendelea na Mheshimiwa Constantine Kanyasu, baadaye Mheshimiwa Yahya Ally Mhata ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais mama Samia Suluhu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya Kanda ya Ziwa katika siku hizi tatu alizotembelea huko. Tunampongeza sana na kumshukuru sana kwa kazi kubwa aliyioifanya pale kwenye kivuko ambako tunajenga daraja. Kwa mtu ambaye hajawahi kufika anaweza kufikiri tunazungumzia daraja la mita 200, lile ni daraja lenye takriban kilometa 3 na pointi, lakini umuhimu wa daraja hilo ni pale unapokuwa una mgonjwa unampeleka Bugando kwenye hospitali ya Rufaa na ziwa limeziba *water hyacinth* unachukua masaa matatu unasubiri *ferry*. Umuhimu wa daraja hilo ni pale unapowahi ndege na *ferry*haziwezi kupita majani yameziba na umuhimu wa daraja hilo ni pale unapokimbizana na uhai wa mtu unataka kuvuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba tumhakikishie Mheshimiwa Rais, wananchi wa Kanda ya Ziwa wanamshukuru sana na kumpongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa ambayo wameyasema weznangu. Kwanza nianze na msamaha wa kodi kwenye nyasi bandia. Mheshimiwa Waziri, nikupongeze sana kwa jambo hilo lakini nikuombe, nchi hii ina Majiji sita tu, unaposema umetoa msamaha wa kodi wa nyasi bandia kwenye majiji sita, maana yake unataka kupandisha michezo

kwenye majiji sita na tayari majiji haya yana *loopholes* nyingi na uwezo mkubwa wa kujiendesha na kuendesha viwanja vyake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetamani kusikia kutoka kwako unategemea kupata hasara ya shilingi ngapi iwapo utaruhusu Makao Makuu ya mikoa yote Tanzania watapata viwanja vyenye nyasi bandia. Maana mpaka ninapozungumza leo kila nikiangalia kwenye viwanja tulivyonavyo Tanzania...

**MHE. FESTO R. T. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Costantine kuna taarifa. Taarifa tafadhali.

## T A A R I F A

**MHE. FESTO R. T. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumuunga mkono mzungumzaji anayezungumza kwenye suala la nyasi bandia. Nataka kumpa Taarifa kwamba, kati ya hayo Majiji sita anayoyazungumzia, Dar es Salaam tayari wana viwanja, Mwanza tayari wana viwanja kwa hiyo kuna Majiji manne tu ndiyo ambayo hayana viwanja. Kwa hiyo, unachokizungumza ni kitu sahihi na sisi kama wadau wa michezo tunakuunga mkono. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Constantine, Taarifa hiyo.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea hiyo taarifa. Hapa ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri ni kwamba, kwa mfano tukisema kwenye mwaka wa fedha ulioisha ni wangapi walioingizia pesa kwa kulipa kodi kwa kuleta nyasi bandia? Na unatarajia utakapofuta sasa hiyo misamaha Mikoa mingine utakuwa umeingia hasara kiasi gani? Mimi nikiangalia Mikoa ni miwili na walioweka nyasi bandia ni walewale na inawezekana kuna mwaka mzima utaisha hakuna nyasi bandia. Kwa hiyo, unachokifanya Mheshimiwa

ni kuifanya nchi nzima iwe na mwamko wa michezo kuliko mikoa ambayo tayari imeendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mimi ninaunga mkono kabisa kodi ambayo umeileta kwenye *LUKU* ninaiunga mkono. Nadhani ni sahihi hata kama kiwanja kina *apartment* sita na *apartment* zote zikawa na *LUKU* yake n azote zikadaiwa kodi ni sahihi. Nataka nitoe mfano, sasa hivi ukiwa na *low density* umejenga *apartment* nane na kama zinatofautiana, unapokwenda kulipa *TRA* unalipa *property tax* ya kila *apartment*, sasa kwa nini unashindwa kulipa huo mchango ambao umeupendekeza, kodi ambayo imependekezewa kwenye kila *apartment*? Nafikiri ni sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili litaepusha sana kwanza makadirio ya hovy hovy yaliyokuwepo mwanzo ambayo Mheshimiwa wa Awamu ya Tano aliyaondoa, lakini uhakika wa ukusanyaji wa pesa yenyewe. Duniani kote maendeleo yanakuja kwa watu kulipa kodi na watu lazima walipe kodi ndiyo waone maendeleo yanakuja. Hatuwezi kupiga kelele hapa kila siku tunataka maendeleo wakati hatutaki kulipa kodi, lazima tulipe kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kulisema hapa na kumshauri Mheshimiwa Waziri, bado pesa nyingi sana inapotea. Mimi nina uhakika *TRA* wanakusanya kama siyo asilimia moja ya tatu ya kodi basi ni nusu ya kodi. Mlifanya mpango mzuri sana pale bandarini kwamba, kodi za magari zinajulikana, kabla hujaagiza gari unajua kodi yako hii hapa, jambo ambalo unatakiwa ulibuni na kulifanya huku mtaani ni kuondoa utamaduni wa mtu anajaza zile *audited accounts* halafu tunaanza mjadala miezi mitatu, miezi minne, miezi mingapi, matokeo yake tunakuja kuishia kwenye kuelewana nikutoe ngapi ili tuweze ku-*balance* tunapoteza kodi nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie upya namna tunavyoweza kufanya ili kuwafanya walipa kodi anapomaliza kulipa kodi zile *instalments* makadirio yake yaje *genuine* na

anapolipa awe amemalizana na Serikali, kila mtu atalipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine tupitie upya orodha ya wamachinga. Machinga tumewapa vile vibali wengine wana maduka, wengine wanauza uji, mwingine anauza mchicha, tupitie upya tu-*define* tunafikiria machinga mwenye kibali ni mtu wa namna gani? Ili kundi fulani ambalo tunafikiri limevuka kwenye hiyo *level* tulitoe. Tutakuwa tumeongeza malipo ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo niende sasa kwenye idara moja ya uvuvi. Nimeangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anapendekeza kufuta kodi ya *solar power*. Hivi sasa kule kwetu Kanda ya Ziwa, *solar panels* ndiyo zinazo-*charge* taa za kuvulia dagaa, lakini nimeangalia sasa amefanya *double standard*, wakati amependekeza kufuta msamaha wa kodi amependekeza kuongeza *withholding tax* kwa mazao yote ya uvuvi yanayopelekwa kiwandani. Mheshimiwa Waziri *this is too wrong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ngoja niseme, samaki ambao mvuvi anawapeleka kwenye kiwanda *production cost* yake ni *very expensive*, unapomkata asilimia mbili utahamasisha *smuggling*. Nataka nikwambie mvuvi kwenye mtumbwi mmoja ana-*invest about 20 million*, siku moja ili aende ziwani anahitaji mafuta lita 30. Kuna wakati anapata kilo 10 tu na hizo kilo 10 ndiyo anazokusanya kwenye boti zifike tani mbili ziende zikauzwe, wewe unafikiri zote ni faida, huyu sio mkandarasi, utakapoingiza kiwandani ukakata *2% withholding tax* kwa mvuvi utakuwa umekata mtaji tangu kwenye nyavu, kwenye mafuta na kwenye *operation cost*, sina uhakika kama watu wako wamelielewa vizuri suala hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimuona mtu yuko pale Mwanza ana boti la tani 10 la samaki amekusanya samaki hao wiki mbili na amekusanya kwa wavuvi wanaopeleka kilo 20, kilo 25 ambao kila siku wanatumia lita 30 za mafuta na

ana boti *investment* yake ni milioni 20. Sasa unaposema unaenda kukata *withholding tax* kwa samaki aliowapeleka kiwandani maana yake nini, unakata mtaji. Mimi nikuombe Mheshimiwa Waziri hili *practically* tunakwenda kufilisi watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliishauri hapa Serikali mwaka 2017, ilikuwa inafanya *operations* nyingi kwa wavuvi na matokeo yake wavuvi wote wakubwa ziwani wamekwisha, wale waliokuwa wanakopesha wavuvi hawawakopeshi tena. Na tuliwaambia kwamba, mnafurahi mnakusanya pesa ya faini, lakini watu wanafilisika.

Sasa leo watu wamerudi kwenye kuvua wanavua *illegal*, matokeo yake sasa ni nini, hakuna tena mvuvi anakopeshwa nyavu, hakuna mvuvi ana mtaji. Sasa hivi mtakapoleta hii kodi watu watapeleka samaki Uganda na Kenya. Nakuomba Mheshimiwa Waziri liangalie vizuri sana jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Mheshimiwa Waziri unisaidie kupata ufafanuzi, kwenye ukurasa wa 34 umesema, nimeona kuna mambo mawili kama hapa yana-*contradict*, unazungumzia kuweka kiwango cha kutoza kodi kwa wachimbaji wadogo, kwenye (a) umesema kutoza kodi wachimbaji wadogo wa madini kwa kiwango cha asilimia tatu kwenye thamani ya mauzo ya madini, lakini nimeona tena kwenye sehemu ya nne unasema kutoza kodi kwa yule ambaye amenunua madini kwa wachimbaji wadogo ili kuhakikisha kwamba, anawalipia kodi sasa sijaelewa. Kwa sababu, huyu ulishamtoza kodi huku chini, huku tena unakuja kumtoza kodi huku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukumbuke pia huyu anayeza madini hiyo siyo faida, hawa wanaochimba mashimo anachimba miezi mitatu anakwenda mita 100 hajaingiza hata 100. Shimo linamgharimu milioni 50, siku akianza kuzalisha mifuko 10, mifuko 10 anaitoa kwa *one week*, akiifikisha juu umeshachukua asilimia tatu, lakini bado unasema utahakikisha kwamba kuweka wajibu wa mchimbaji mdogo wa madini kama muajiri wa kukata kodi

mapato ya ajira kutoka kwa wafanyakazi wake pale tu madini yanapokuwa yamepatikana na kuuzwa kwa masoko ya madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini yametoka wapi? Yametoka kwa wachimbaji wadogo, umeshawakata kodi, huyu mchimbaji mdogo akienda kuuza unamkata kodi, tunapambana sana suala hili linafanana na kwenye samaki. Wenye viwanda wanalalamikia *royalty*, umekwishaenda kukata asilmia *mbili*, umeshamkata mchimbaji mdogo, unamkata na huyo, Mheshimiwa hii si *double taxation*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikuombe Mheshimiwa litazame vizuri. Tukiamua kumkata yule mdogo kule chini basi tu-*track source* yake iko wapi ili kusudi hawa waliopo wabaki huku chini

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Constantine Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na mwisho dakika zitakazobaki atachangia Mheshimiwa Mwanahamisi.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mama Samia Suluhu kwa maono mazuri aliyonayo juu ya nchi yetu, pili nimshukuru sana Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu wake na wafanyakazi wote wa Wizara ambao kwa namna moja au nyingine wameshiriki kikamilifu katika uandaaji wa bajeti hii. Tatu, naomba niwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bajeti,

Ndugu yangu Mheshimiwa Daniel Silo, Makamu wake CPA Omar Kigua kwa mchango mzuri waliutoa kwenye Kamati na kuishauri Serikali hatimaye leo hii tunaijadili bajeti hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo, kwanza naipongeza sana Serikali kwa maono yake iliyonayo juu ya kuhakikisha Madiwani wetu wanapata posho moja kwa moja kutoka Serikali Kuu. Tatizo hili lilikuwa tatizo kubwa sana, Rais wa Awamu ya Nne Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alifanya kama leo Mama yetu anavyofanya, aliamua kuhakikisha Madiwani wote wanalipwa kiinua mgongo kutoka Serikali Kuu, hii ilikuwasuluhisho la matatizo kwenye Halmashauri zetu. Leo hii tunapoamua kuwalipa madiwani posho zao kupitia mfuko mkuu tunahakikisha Halmashauri zote tunazitendea haki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana posho inayopatikana sasa hivi ni ndogo. Mheshimiwa Waziri kwa kuanzia ajaribu kuona *alternative way* ambayo tunaweza tukainua kidogo posho za Waheshimiwa hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu Mheshimiwa Diwani anahudumia vijiji 12, anatembea ana vijiji 12. Nina Kata mimi inaitwa Kata ya Sengenya Mheshimiwa Diwani ana vijiji 12, posho hii yote anayopata inatumika katika kuhudumia vijiji hivi. Kwa hiyo, badala ya kutumia kidogo kujikimu anajikuta anaitumia kwa ajili ya shughuli za wananchi. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri hili aliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kuwalipa Maafisa Watendaji wa Kata posho zao, posho za mafuta. Pamoja na kwamba, Maafisa Watendaji hawa hawana vitendea kazi, lakini ninaamini wataitumia posho hii kwa ajili ya kukodi bodaboda, ili kuweza kufanya shughuli za halmashauri. Sisi ni mashahidi, sisi ni Madiwani, tunafahamu Maafisa Watendaji Kata wetu ndiyo wakusanya ushuru wa Halmashauri, ndiyo walinzi wa amani

katika Halmashauri zetu kwa hiyo, kwa kweli, hizi 100,000/= watakazopewa zitawasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu hii isiwe hisani, Wakurugenzi wa Halmashauri wasije wakawakopa hawa Watendaji, walipwe kila mwezi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Waziri, lazima utoe *paper* itakayowa-*instruct* hawa Wakurugenzi, hakuna kuwaruka, vinginevyo hawa watakopwa. Sheria ya posho huwezi uka-*carry forward*, kama hautamlipa ndani ya mwaka wa fedha hautasema hili ni deni. Kwa hiyo, Wakurugenzi wengi wanaweza wakatamia kigezo hiki kutokuwalipa posho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu uamuzi wa kuwalipa Makatibu Tarafa ni wazo la busara sana. Hawa ndiyo viungo muhimu, wanafanya kazi kubwa katika Tarafa zetu kwa kweli, mmewapa vitendeakazi kwa maana ya pikipiki, posho hizi zitawasaidia kwenye mafuta, hongereni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuangalia suala la *TARURA*. *TARURA* tulizungumza hapa ndani ya Bunge kwamba, wanapata fedha ndogo, tumewaongezea fedha, jambo hili ni heri kabisa. Rai yangu Mheshimiwa Waziri, kuna Sheria ya *TARURA* ya mwaka 2007, Sheria ya Barabara, inakataza malori yote zaidi ya tani 10 kwenda vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kijijini kwetu ndiko ambako kuna mazao, wafanyabiashara, hasa kipindi hiki cha mazao mfano kwangu mimi, huu ni msimu wa ufuta halafu utakuja msimu wa korosho, hakuna lori la tani 10 ambalo litatakiwa lipite. Kwa hiyo, nawaomba sana Mheshimiwa kwa kuwa tunaongezewa fedha naomba Mheshimiwa Waziri ije sheria tuibadilishe, hakuna lori la tani 10 kijijini kwetu malori yote ni kuanzia tani 15, tani 30.

Sasa leo unaposema tani 10 yasionekane vijijini maana yake yakae barabara kuu halafu gharama ya kuanza kutoa mazao kutoka vijijini kuleta barabara kuu, tunaongeza gharama ya uendeshaji. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri

nakuomba sana hili mliangalie. Hii kero kubwa sana huko vijijini wananchi wetu wanalia, wafanyabiashara wanalia kwa sababu ya sheria hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *Property Tax*. Imezungumzwa vizuri, Mheshimiwa Mwigulu nakuunga mkono kwa uamuzi wa kubadilisha njia ya ukusanyaji. Ni kweli 2017/2018 *Property Tax* ilikuwa inakusanywa na Halmashauri kabla ya 2017/2018 ikawa matatizo makubwa. Badaye Serikali Kuu kupitia *TRA* na sasahivi mmebadilisha utaratibu huu wa ukusanyaji, mimi nauunga mkono. Rai yangu kwao, kupitia *LUKU* katika wilaya zetu nataka kujua mgawanyo wa mapato utakuwaje? Najua watu watalipa *Property Tax* kutoka sehemu mbalimbali za nchi hii.

Je, ile *Property Tax* itakayokusanywa ndani ya wilaya yangu, itabaki ndani ya wilaya yangu au ndio ile asilimia 15 uliyozungumza kwa utaratibu upi? Lazima tujue mgawanyo halisi wa *Property Tax* kwenye halmashauri zetu ili halmashauri zetu ziweze kufanya kazi inayostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Chumi amezungumza, kuna ahadi za viongozi. Viongozi wetu wanatoa ahadi nzuri sana, Mheshimiwa Mwigulu tunakuomba sana hizi ahadi za viongozi muwe mnaratibu na mnazingiza kwenye bajeti. Isiwe jukumu la sisi Wabunge kuanza kufanya *lobbying*, kuanza kuwabembeleza kuna ahadi, kuna ahadi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Mheshimiwa Rais alipokuja kwangu wakati wa kampeni aliahidi kujenga barabara ya lami kutoka jimboni kwangu kwenda Mkoa wa Morogoro kupitia *Selous*, ipo ndani ya ilani, lakini kwenye bajeti haipo. Lini itaingizwa ndani ya bajeti? Nilitarajia leo kingekuja kitabu hapa kikaeleza hizi ni ilani za viongozi wetu. Ilani hii itatekelezwa mwaka huu, ilani hii itatekelezwa mwaka huu, badala ya sisi kuanza kuja kuanza kubembeleza kuna ahadi! Waziri Mkuu 2018 aliahidi barabara kilometa tano ndani ya Jimbo langu, haipo popote tangu 2018 mpaka leo. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Mwigulu, tunaomba

hizi ahadi za viongozi wetu mziratibu na mziingize ndani ya utaratibu wa bajeti ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya Serikali Mheshimiwa Mwigulu aliongelea mambo ya msingi mengi, mambo ya kupunguza tozo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu. Mimi naunga mkono mia kwa mia.

Rai yangu Mheshimiwa Waziri yale yote ambayo mmeyaeleza yatekelezwe ndani ya mwaka ujao wa fedha ili tutakapokutana tuweze kuisifia bajeti na utekelezaji wake, vinginevyo tutakuwa tunadanganyana. Naomba sana itekelezwe kama tutakavyokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahya. Tunamalizia na Mheshimiwa Mwanahamisi, karibu.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu chetu cha Quran mwanamke ametajwa mara tatu, mwanaume ametajwa mara moja, kwa nini sasa? Wengi tunamzungumza Mama Samia, tunampongeza kwa kazi nzuri alivyoanza, lakini mimi ninasema Mama Samia tumuombee dua usiku na mchana, huyu ni mama, huyu ni mwanamke. Nilisema Kitabu cha Quran mwanamke ametajwa mara tatu kwa sababu mama ndiye aliyebeba mimba, mama ni mlezi, mama ana upendo. Kwa hiyo, naomba Watanzania, Waheshimiwa Wabunge, tumuombee Mama Samia afanye kazi kwa kuwatendea haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumuomba dua Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliyoanza kufanya, Mwenyezi Mungu awape nguvu na afya kwa kuitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge niliyetokea Zanzibar. Bajeti imezungumza vizuri sana, lakini bado nitasema kuna mambo yanayotutanza Wabunge tunaotoka Zanzibar. Mimi leo nilileta gari langu karibuni na barua hii hapa. Barua hii nimepewa nije na gari langu kuishi nalo Tanzania Bara kwa mwaka mmoja, wakati mimi ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mkataba wangu nikiwa hai ni miaka mitano, leo nimepewa barua hii nikae na gari langu huku mwaka mmoja.

Je, tunamuuliza Mheshimiwa Waziri hii ni sheria au ni haki au ni nini? ama ni sisi tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili niulizie kuhusu ma-*agent* kutoa gari Zanzibar kuja Tanzania Bara. Tuelezwe huyu *agent* ana mchango kwenye Serikali au ni nini? Tuelezwe kwa kweli imekuwa ni mateso ni maonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa wafanyabiashara wadogo-wadogo. Tunapenda sana wafanyabisahara wadogo-wadogo, vijana, akina mama na wazee, lakini vijana na wazee sasa hivi biashara zao wanafanyia katikati ya barabara, kwa kweli hii ni hatari maana hata Serikali inakuwa mapato inapoteza. Unakuta leo sado za nyanya zimepangwa barabarani, pana ujororo tu wa barabara tunaopita na magari, kwa hivyo naomba suala hili lishughulikiwe. Kwa kweli, wapangiwe nafasi, sehemu nzuri ya kufanya biashara zao wao wapate, lakini na Serikali ikusanye mapato vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Ilipopita bajeti Wabunge wengi tulizungumza kuhusu maliasili, kama hatukulisimamia suala la maliasili basi maliasili nafikiri baada ya muda mdogo itakuwa wanyama wetu wengi watapotea. Leo Mheshimiwa Mbunge anasimama anasema yeye tembo hana faida nae, ng'ombe ndiyo wana faida nao. Mimi naiomba Serikali lazima Wabunge wale waliopo pembeni mwa hifadhi wapewe elimu pia na wafugaji wapewe elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema tembo hana faida kwa sababu tembo ni mnyama aliyeumbwa hifadhi yake ni kukaa kwenye hifadhi, hatembe, hata ukimfuata tembo unamfuata nyumbani kwake. Kwa hivyo, mtu yeyote anayemfuata mtu nyumbani kwake unakwenda kumtafuta ushahi. Mimi nilikuwa naomba suala hili la hifadhi zetu lazima zilindwe, ziheshimiwe na sheria zifuatwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utalii. Tunasema sana utalii ni wa nje tulikuwa tunautangaza, lakini sasa tutangaze utalii wa ndani. Nani atatangaza utalii wa ndani? Kutangaza utalii wa ndani ni wananchi wenyewe wa ndani. Tuna wasanii wazuri, vijana, warembo, hawa tuwape ubalozi watangaze utalii wetu wasitafute watu wengine wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.  
*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanahamisi, mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii au kwa mchana huu.

Nawashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa wote mliochangia kwa kazi nzuri, kwa vile hakuna tangazo lolote basi nasitisha shughuli za Bunge hazi Saa kumi na moja kamili jioni.

*(Saa 07:00 Mchana, Bunge lilitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Thea Medard Ntara, afuatia Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo na baadaye tutaendelea na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza kabisa nami niungane na wenzangu kuipongeza sana Serikali. Ni mara ya kwanza kuingia katika Bunge hili Tukufu lakini kwa yaliyotokea kwenye hii bajeti kwakweli yanafurahisha sana. Na kwa upande nimpongeze Waziri wa Fedha nimpongeze mwenyekiti wa Kamati na Wajumbe wote wa Kamati ile ya bajeti, mmejithahi sana angalau kujibu yale ambayo tuliyokuwa tunayazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimefurahishwa kwanza kuhusu lile suala la mikopo, nimefurashishwa mno. Kuondoa zile siji *retention* zile adhabu kwenye mikopo, nimepigiwa simu yaani nifuraha nifuraha huko vyuo vikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuongeza mikopo kutoka bilioni 464 mpaka 500, niwapongeze Serikali. Na kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyoahidi, amesema watoto wote wenye vigezo watapata mikopo kupitia ule mradi wa *HIT*.

Mimi ninaamini kutakuwa na mabadiliko makubwa sana, si kwa vyuo vikuu tu lakini na kwa wale wanaomaliza. Na ndiyo kutokana na hii miradi nafikiri sasa fedha za *research* itapatikana. Niipongeze sana Serikali yangu, kwakweli *I just love you people*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala moja, Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kwenye hili unisikilize vizuri sana nashauri, kuna ulipaji wa madeni wazabuni na wakandarasi, na niombe sana Serikali haya madeni mnayolipa mzingatie na lile suala la Nelson Mandela kuna tatizo kubwa sana kwenye kile chuo Wizara ya fedha pamoja na Kampuni inayoitwa PPL walichukua mkopo wa mabilioni ya fedha takriban bilioni 38.7 kwa ajili ya ujenzi wa kile chuo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipochukua ule mkopo wakaipa ile kampuni PPL wao pia wakaingiza kampuni nyingine na kugawana kazi na wakampa mzabuni anayeitwa *ELERA Construction*, yeye ashughulikie na viwanja vya michezo. Sasa huyu hajamaliza vile viwanja vya michezo na anadai ile fedha, takriban milioni mia nne na kitu, ambayo ni *retention*. Sasa wale wamesema hawaweze kumlipa kwa sababu hajamaliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, kuna vurugu pale, wanashindana je, nani amlipe huyu na nani ambaye hataki kumlipa. Kwa hiyo kuna vurugu kati ya Wizara ya Fedha, Ardhi pamoja na Wizara ya Elimu, na Ardhi nafikiri inahusika. Sasa nimuombe Waziri alimalize hilo, na nikimaliza kuzungumza hapa Mheshimiwa Waziri nina *document* nitakupa uandike umalize lile tatizo la Nelson Mandela kwa sababu huyu mtu anataka *retention* lakini kazi hajamaliza, wewe ukimsimamia najua hilo litakwisha nafikiri umenielewa hapo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine nije kwenye ujenzi wa miundombinu. Mimi nakushukuru, kwenye elimu mmetoa bilioni 406 kwa ajili ya kuangalia miundombinu katika elimu. Niombe sana Serikali na hasa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Elimu, kaeni pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe majengo yaliyojengwa *UDOM*, Waheshimiwa wenzangu mtakumbuka, *UDOM* ile ilijengwa kwa *speed* kali mno ili kuwaokowa watoto wengi waingie vyo vikuu; wazo lilikuwa zuri na ni jema, lakini

niwaambie kitu, yale majengo yalijengwa mengine kwa *speed* ya ajabu kiasi kwamba si imara. Kuna nyufa na tiles zimebanduka. Niwaombe Waziri wa Fedha na Waziri wa Elimu nendeni mkatembelee pale *UDOM* mtasikitika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tufanya ukarabati kabla hali haijawa mbaya. Nendeni *UDOM*, lakini si huko tu kuna sehemu nyingi majengo yamechakaa; ukienda *MUST* ni balaa majengo yamechakaa, ukienda Hombolo barabara haifai na hizo ni barabara zote zinazolingia vyo vikuu. Jamani mbona tumeviweka nyuma ebu wasaidieni ili nao waonekane kweli ni vyo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hawa Hombolo wamepata eneo pale palikuwa kwa Mkuu wa Mkoa (*RS*); sasa muwasaidie, wanataka kutoa *structure* nzuri mno pale, nyinyi muwasaidie kwa kuwa-top-up ili waweze kujenga jengo zuri lenye tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudi kuzungumzia fedha mlizotenga kwa ajili ya sensa. Mimi nimefurahi mmetenga fedha za kutosha, bilioni 328 sio mchezo. Hata hivyo naomba sana m-*develop device* za kuweza kugundua watoto wenye ulemavu wanaofichwa wakati wa sensa ili tupate idadi kamili ya watu waliopo; sasa wale wanaofichwa ndani mtawagunduaje? Ninyi mtumie teknolojia, mtengeneze *devices* wakati wa sensa ili tupate idadi hata ya wale watoto wanaofichwa ili waweze kusaidiwa na Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niipongeze Serikali kwa kuingia kwenye hizi *blocks*. Nakumbuka Mheshimiwa Naibu Spika alisema nini Kiswahili chake, nimejaribu kutafuta hili neno *blocks* sijui ni vipande. Nipongeze kwa kuwa kwenye hizo *blocks*; tuna *PAP* tuna *IPU* maziwa makuu na *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *SADC* yenye ina nchi kama 15. Sasa unaona tukishakuwa *blocks* nyingi kiasi hiki mimi ninaamini kwanza tutaleta mahusiano mazuri na vilevile tutaondoa na vikwazo visivyo vya kikodi. Wazungu wale

waliotoka Songea wanasema *none tariff barriers* zitaondoka  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kufanya hivyo, na pia kwa kujikita huko mimi ninaamini tunaweza kufungua masoko vizuri na kuwa na urafiki wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi baada ya kusema hayo nikushukuru sana, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Thea. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, baadaye Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela ajiandae.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kuniona ili nipate kuchangia kidogo kwenye bajeti hii ya Serikali ambayo ipo mezani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kumshukuru Mungu sana mwingi wa rehema ambaye ametupa uhai na nguvu hata nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu hili siku ya leo, lakini namshukuru zaidi kwa ajili ya kulipenda sana taifa letu hili. Tumeshuhudia mambo makubwa Bunge hili la 12. Tulianza kushuhudia aliyekuwa Rais wetu Hayati Dkt, John Pombe Magufuli akiapishwa tarehe 5 Novemba, 2020 baadaye na sisi tukaja tukaapishwa, tarehe 13 Novemba, 2020 akaja akazindua Bunge akatoa hotuba nzuri sana. Kwa kiwango kikubwa bajeti hii ya Wizara ya Fedha, bajeti hii ya taifa imebeba maono yaliyokuwa kwenye ile Hotuba ya Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, baada ya yale matukio kwa upendo wa Mungu Rais wetu Mama yetu Samia Suluhu Hassan alichukua kijiti, na tumeshuhudia akifanya mambo yake kwa umahiri mkubwa. Alitupitisha kwenye taharuki ambayo tulipata baada ya kuondokewa na kipenzi chetu, Rais wa Wwamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli ambaye alifariki tarehe 17. Alitupitisha kwenye ile

taharuki kwa umahiri mkubwa sana na ameendelea kuijenga Serikali na sasa hivi tunaendelea kupaa. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana, anafanya kazi nzuri na kila mmoja anaamini hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu wake Mheshimiwa *Engineer* Masauni, Katibu Mkuu na watendaji wote kwenye Wizara hii ya fedha kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kufanya.

Tumeshuhudia uchumi wa nchi yetu ukipanda kwa *percent* 6.9, lakini pia na hali ya umasikini kupungua kutoka *percent* 28.2 hadi *percent* 26.4; haya ni mafanikio makubwa sana. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na baada ya hayo machache sasa niseme kidogo kuhusu hii bajeti ambayo imeletwa mbele yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wizara imekuwa inasikiliza hoja za Wabunge na hatimaye fedha zimetolewa milioni 500 kwa kila Jimbo kwa ajili ya kuiwezesha *TARURA* ili wajenge barabara za vijijini. Kwakweli kwa hilo ninaishukuru sana Serikali yetu, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo; kwa sababu Wabunge tumelalamika muda mrefu hapa kwamba hali ya barabara za vijijini ni tatizo na fedha hazitoshi. Kwa kuanzia ameamua kutoa hizo milioni 500, tunaamini kwamba itapunguza yale makali na kelele ambazo tulikuwa tunazipata kutoka kwa wananchi kwa sababu ya ubovu wa baarabara za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye sekta ya kilimo. Kama tunadhamiria kweli kweli kuhakikisha kwamba tunakuwa na uchumi wa kijani, kama kweli tumeamua kwamba tufanye kilimo cha uhakikani lazima tuachane na kutazama mawingu, ni lazima turudi sasa tujenge miundombinu ya umwagiliaji ili tuweze kufanya kilimo kinachoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo imeajiri Watanzania takribani *percent* 65 lakini mchango wake kwenye Pato la Taifa ni chini ya *percent* 25, hiyo hali haina uwiano kabisa na kusema kweli tunapaswa tubadilisha hiyo hali na namna pekee ya kubadilisha na kuhakikisha kwamba nchi inakuwa ya kijani na kwamba tunavuna sawasawa ni tuhakikishe kwamba tunatengeneza miundombinu ya umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaishi milimani kule Arusha Wilaya ya Arumeru. Kule kuna mvua za kutosha na kila mwaka kunatokea na mafuriko. Mafuriko haya yanakwenda yanaharibu mashamba na miundombinu sehemu za tambarare . Rai yangu kwa Serikali, tuhakikishe kwamba tunavuna maji haya na kuyatumia kwa ajili ya kumwagilia mashamba yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie kuhusu ahadi za Mheshimiwa Rais. Kwenye hotuba ya Rais ya tarehe 13 Novemba, 2020 alisema atatoa vipaumbele kwenye ahadi zake alizozitoa wakati wa kampeni. Nimkumbushe Mheshimiwa Waziri atenge fedha kwa ajili ya kutekeleza ahadi zile, maana sasa hivi zile ahadi ni wosia, na usipotekeeza wosia unapata laana, na haya maneno si yangu, aliyazungumza Rais wetu mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan wakati akiapisha viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kusema kwamba Halmashauri zetu nyingi zimeendelea kufanya kazi kwa shida kwa kuwa hazina mapato ya ndani. Kwa mfano Halmashauri ya Arumeru mwaka juzi ilikuwa imetengewa fedha kwa ajili ya mradi wa kituo cha mabasi lakini fedha zile zilirudishwa, sijaelewa kwanini ule mradi ulikatizwa. Nimuombe Mheshimiwa Waziri aliangalie hili sasa. Kwamba ili Halmashauri zifanya kazi vizuri zinapaswa ziwezeshe, watekeleze miradi mkakati kwa kule Halmashauri ya Meru tunahitaji bado kile kituo cha mabasi lakini pia kuna soko la Tengeru, lile soko la Tengeru linatoa huduma kwa wananchi wengi; linatembelwa hata na wananchi kutoka nchi za jirani kuja kufanya biashara na kuja kununua mazao pale. Niombe

Serikali ilianganalie ili hilo soko liweze kujengwa na kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanafanya biashara zao vizuri kwa ajili ya kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nipo kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais, nakumbushia barabara ya King'ori na nitaendelea kuikumbusha, kila nikisimama nitaendelea kuikumbushia; na hizi ni pamoja na ahadi ya kilometa tano ambazo Marehemu alitoa pale *USA River* tarehe 6 Oktoba, 2015. Kwa bahati mbaya mpaka leo hakuna hata mita moja iliyojengwa pale *USA River* pamoja na kwamba ule mji ulishatangazwa kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo. Niombe Serikali iendeleo kuwazia Mji wa *USA River* ili uingizwe kwenye ule mpango ule mradi wa *TACTIC* angalau nao miundombinu yake ijengwe kwa sababu ule mji ni Makao Makuu ya Wilaya ya Arumeru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa muda mfupi huu. Yako mengi yakusema lakini niishie hapa; nashukuru kwa muda ulionipa naunga mkono hoja (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsantse sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, tunaendelea na Mheshimiwa Grace Tendega baadaye Mheshimiwa Issa Ally na Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie katika hotuba hii ya bajeti iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa inanipa ugumu sana kupongeza sana, lakini kwa mara ya kwanza ninapenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuleta bajeti ambayo kiasi fulani imeakisi zile kelele ambazo tulikuwa tukizipiga. Ninasema hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais alituita pia wanawake wote bila kujali itikadi. Tulikwenda, tulimsikiliza na tukaona kwamba vitu anavyovizungumza ni vitu ambavyo

vikitekelezwa ipasavyo vitamkomboa Mtanzania na kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele. (*Makofi/vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya hivyo katika bajeti hii nitanukuu vitu vichache ambavyo tumeona angalau vinaweza vikasaidia Halmashauri zetu Mikoa yetu, Wilaya zetu, wananchi wetu wakasonga mbele kama tutatekeleza vile anavyotaka. Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake kwamba watahakikisha kwamba fedha ambazo zilikuwa zikitumwa katika Halmashauri mwishoni mwishoni, yaani kwa mfano mwezi Juni au Mwezi Mei wataniacha na wataziacha zitekelezwe lakini tunaomba Mheshimiwa Waziri mtuletee kanuni ili zikienda kule zisiende zikakae muda mrefu pia ili ziweze kutumika. Tunapongeza kwa hilo kwa sababu zilikuwa zikifika Juni na zinaondoka, kwa hiyo ilikuwa inaleta shida sana katika utekelezaji wa majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watu wamezungumza kuondoa ushuru wa nyasi bandia. Nasisitiza hili ni jambo jema kwa sababu tunakuza nyanja zote, ukikuza hata katika michezo hii itasaidia, lakini wasiishie mijini tunaomba Mheshimiwa Waziri waende mpaka vijijini, zile halmashauri ambazo zitaweza kuwa na viwanja wakanunua hizo nyasi basi wafanye hivyo, waliangalie wakati anakuja kuhitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kupungua asilimia tano za mabango ya *categories* zote, hii ilileta shida sana, tukakuta kuna watu walianza sasa kuwa wanaweka kaa alama tu kadogo pale wakawa wanakosa kodi. Sasa kupunguza watu watalipa kodi na watapata mapato na kodi ikitolewa ndipo tutaweza kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nina mambo mawili pia ya kusisitiza katika hili. Kodi ya majengo wamesema itakuwa kupitia LUKU. Wamezungumza wengi hapa kwamba nyumba ikiwa na wapangaji wengi itakuwaje wataiwekaje sawa. Nataka wanapokuja kuhitimisha waniambie, kuna nyumba ambazo zinatumia *solar*, kuna nyumba ambazo zinatumia

*biogas*, sasa hazina LUKU watapataje sasa kodi zake hapo? Mheshimiwa Waziri aje atuainishie namna ambavyo watapata kodi kupitia hii, kwa sababu siyo wote wana umeme na kuna maeneo mengine hakuna umeme.

Kwa hiyo, waje na mkakati maalum wa kujua kwamba kama watachukua kwa kupitia LUKU watafanyaje, lakini waliweke sawa pia kwa sababu mwenye nyumba yupo, wakiwa wapangaji watupu pesa zile atakwenda kuchukua kwa wapangaji. Sasa hili watuweke sawa hapa Waziri anapohitimisha ili tujue tunafanyaje katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kodi ya mapato *Pay As You Earn* wamesema kiwango cha mwanzo hawatozi kodi, lakini kiwango kinachofuata kinatozwa kodi. Ukiangalia hii napongeza kweli wametoa asilimia moja safi kabisa, lakini haitoshi. Ukipiga mahesabu unakuta karibu tu ni Sh. 2,700. Sasa Sh.2,700 bado ni kidogo, ni ndogo sana. Kwa hiyo tuombe waiangalie vizuri kukata mzizi wa hili lote, tuwapandishie mishahara watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwapandishia mishahara watumishi, wataweza kulipa kodi, lakini pia ni motisha kwao kwa kufanya kazi kwa juhudi na vile vile wanaweza wakatoa kodi. Kwa hiyo Serikali itapata *benefits* humo kwa kufanya hivyo kwa sababu itawafanya wawe na *moral* kubwa kabisa ya kujenga uchumi wa nchi na vile vile kiinua mgongo kitapanda. Tunajua kabisa watu wanastaafu, viinua mgongo vinakuwa chini, wameona kwa miaka mitano watumishi hawakupandishiwa mishahara, kwa hiyo wakifanya hivyo wataondoa kero ambazo zinawaumiza sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama amezindua kule Mwanza *SGR* kwa Mwanza. Sasa waharakishe basi ikamilike, kwa sababu kwa *SGR* tutaondoa mrundikano unaokuwepo pale Dar es Salaam. Kwa hiyo mizigo itakuwa inakwenda kwa haraka na uchumi utapanda. Hivyo, wakiweka mikakati mizuri wataweza kufika mbali na kuondoka kero za wananchi ambazo zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika suala la kodi. Naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize, mkoloni alikuja, alivyokuja hakuja na hela, alipokuja alikuja na wazo, alikuja na *idea* kwamba atafanya nini, kaikuta nchi ya Tanzania, akakuta kuna ardhi, alivyokuta kuna ardhi akaona hii ardhi itanufaisha watu kwa kilimo, kukawa na kilimo cha mkonge, katani na vitu kama vile. Akasema anatunga Sheria ya Kodi, kwa hiyo alivyotunga Sheria ya Kodi wananchi wao wenyewe waliinuka kwenda kufanya kazi pale ili waweze kupata pesa, watoe kodi na ndiyo hayo unayoyaona, tukachenjua barabara hizo mnazoziona, kodi ilitumika kujenga nchi, tukaweza kufanya mambo mengi sana ambayo yalifanyika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa katikati tulilegalega, kodi inatolewa lakini mambo hayaendi, watu wakawa hawajui kodi inaenda kufanya nini. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, hawa watu wa Wizara wawe na mikakati maalum ya ukusanyaji wa kodi. Huu ukusanyaji usiwe wa kinguvu, iende ifike mahali wananchi wenyewe waone kwamba kutoa kodi inamlazimu, yaani akinunua kitu asitoe kodi yeye mwenyewe kwa maumivu. Hivi kweli unaletewa barabara nzuri, kuna maji safi na salama, una afya unapata madawa na nini hospitalini, nani atakataa kutoa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kila kitu kikionekana kinafanyika vipi, wananchi watakuwa tayari kutoa kodi. Kwa hiyo waende wakafanyie kazi. Naomba niwape mfano tu wa Rwanda; Nchi ya Rwanda walikuja na sera ya kuondoa majani kwenye nyumba zao, lakini lengo lao lilikuwa siyo kuweka bati pekee, ilikuwa pia ni kukusanya maji. Kwa hiyo, walisema tunaondoa nyasi watu waezeke kwa mabati, japokuwa hapa kwenye mabati Wizara wameongeza tozo, ili katika mabati yale wakusanye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kupata maji, yale maji yakawa yanatiririka kwenye udongo, yanaharibu ardhi unakuwa mmomonyoko wa udongo, wakatunga tena sheria kwamba hakuna kutiririsha maji, kila mtu lazima hata awe na matuta mawili, matatu ya mboga kwenye nyumba

zao. Kwa hiyo hii siyo tu kwamba mna-save vitu vingi, watu watapata *vitamins* kwenye mbogamboga, watu watapata maji, vile vile watu watapata pesa. Wale wanaouza *gator* zile watapata biashara, mafundi watapata kazi, kunakuwa na *chain* pale ya watu kupata ajira na fedha inapatikana. Kwa hiyo sheria ndiyo mzizi wa kila kitu wa kupata pesa na kupata kodi. Kwa hiyo, naomba waangalie, watuletee tuone ni zipi ambazo zitafuatwa ili Watanzania waweze kuona namna gani wataweza kujenga nchi yao kwa mapenzi, siyo kwa shuruti, ili tuweze kupata fedha za kuendeshea nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, kuna kitu kimoja naomba nishauri, kuna mapendekezo ya kodi kwenye laini za simu kutoka Sh.10 mpaka Sh.200 kwa siku. Maana yake ni kwamba mtu atalipa Sh.6,000 kwa mwezi na kwa mwaka Sh.72,000, lakini tumesema tunataka tuingie kwenye teknolojia. Naomba isubiriwe kwanza, siyo Watanzania wengi wanaomiliki hiki kitu na Mheshimiwa Rais ametoka kuzungumza siku mbili, tatu hizi, kwamba tuangalie tujifunze kwa wenzetu masuala haya ya teknolojia yakoje na sisi twende nayo. Kwa hiyo tukianza kutoza huku tutakimbiza Watanzania wanaoweza kumiliki simu, Watanzania ambao wanaweza wakafanya biashara na uchumi ukakua kwa kutumia simu. Kwa hiyo waliangalie suala hili linaweza likawa zuri, lakini linaweza likaathiri kwa upande mwingine wa ukuaji wa teknolojia ili tuhakikishe kwamba Watanzania na sisi tunakwenda kama nchi zingine zinavyokwenda. Kwa hiyo twende na sisi tukazidi kusonga mbele na kuleta maendeleo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Grace.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Pindi Chana wajiandae.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya tele mpaka naweza kuchangia bajeti hii.

Pili, niishukuru familia yangu, lakini kipekee kabisa nimshukuru mke wangu aliyenipa uwezo mkubwa sana wa kuwajibika na kuweza kutimiza majukumu yangu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, bajeti hii ni bajeti ambayo itaendelea kusomwa na kusifiwa kuwa ni bajeti nzuri kabisa katika bajeti zilizowahi kujadiliwa katika Bunge hili Tukufu. Siyo nasema hivyo kwa sababu tu ya kutaka kusifia, lakini ukiangalia jinsi hii bajeti ilivyotengenezwa, unaweza ukalithibitisha hilo nia ya bajeti ukiangalia lakini pia ukiangalia dira lakini ukiangalia dhamira na pia ukiangalia pia utayari wa Mheshimiwa Jemedari wetu Mama Samia Suluhu Hassan, hiyo inakuashiria moja kwa moja kwamba hii bajeti itakuwa bajeti nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yenyewe naanza kwa kusema kabisa kwamba itatekeleza na kusimamia mazuri yote ambayo awamu tofauti tofauti za uongozi imeyatekeleza. Mazuri katika awamu hizo yako mengi sana, kila awamu iliyopita imekuwa na jambo zuri sana la kuigwa na kulisimamia kwamba liendelee kuwepo. Hata hivyo, kwa hali jinsi ilivyo kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuzungumzia kila zuri la awamu iliyopita, lakini kipekee tu nitaweza kuzungumzia jinsi walivyoweza kusimamia yale waliyotaka kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Awamu ya Kwanza ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, yeye aliamini katika Taifa lenye uchumi imara kupitia sera ya Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea lakini hali kadhalika nchi huru yenye fikra huru, yenye uchumi huru, yenye siasa huru bila kujifungamanisha na nchi yoyote ile. Hili lilikuwa ni jambo jema kabisa ambalo awamu hii pia italitekeleza kwa njia ya kipekee kupitia staili yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu iliyofuatia ilikuwa ni awamu ya Mheshimiwa Rais Ally Hassan Mwinyi na yenyewe ilikuwa na dhamira nzuri kabisa uchumi huria, lakini yenye watu ambao wako *proactive*, kukimbilia fursa ambazo zitawawezesha wao kujenga nchi yao kikamilifu hasa katika masuala ya kibiashara. Fikra hii lililenga katika kuimarisha dhana ya kuwa uchumi au suala la biashara lishughulike na watu binafsi, lakini wakati huo huo Serikali ikijikita katika kutekeleza mambo ya msingi ya kijamii na kuendeleza miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tatu, ya Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na yenyewe ilikuja na fikra pevu, nzuri kabisa ambayo yenyewe lililenga kabisa katika utekelezaji wa uwazi, lakini *seriousness* katika utekelezaji huo. Lengo lilikuwa ni kuwajenga wananchi waweze kujitambua, lakini pia kuona kwamba kila wanachokifanya wanakifanya kwa ajili ya manufaa ya nchi yao na uzalendo wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia awamu iliyokuja, Awamu ya Nne ya Mheshimiwa JK. Awamu hii pia lililenga katika kutengeneza uchumi uliokuwa imara, bora kabisa, ilijihakikishia kwamba inaweka miundombinu yote ya kuchochea uchumi na maendeleo, ilijaribu kuweka mkakati pia wa mahusiano ya kimataifa ambayo yalikuwa mahusiano bora kabisa na nchi za nje. Hii yote lililenga katika kuweka uchumi uliokuwa imara uchumi endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Tano, awamu ya jembe, tuliona kabisa awamu hii ilikuja kwa kasi kubwa. Hii ilikuwa ni awamu ya kazi lakini hali kadhalika ilikuwa ni awamu ya viwanda ambavyo vimejielekeza katika kutekeleza uchumi wa nchi hii. Pia awamu hii ilikuwa awamu ya uwajibikaji lakini na u-*champion* katika kupambana dhidi ya rushwa na ufiadini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia awamu hizi zote zilikuwa zimefanya vizuri na kama alivyosema Mheshimiwa jembe letu, mama yetu, jemedari wetu mkubwa, kwamba atajielekeza katika kutimiza mazuri yote, tunaona mazuri haya

yanajenga msingi mkubwa na imara katika kutekeleza yale yote ambayo tunayategemea katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uzuri wa hayo yote, nina shaka kidogo hasa nikiangalia kwa kadri jinsi tulivyoweza kutekeleza bajeti zetu zilizopita. Ukiangalia bajeti zetu zilizopita unaweza katika hali ya ubinadamu ukaona kwamba kunaweza kuwa na shaka. Kwa mfano, kwenye kilimo kilitekelezwa kwa asilimia 13 tu ya bajeti nzima. Halikadhalika viwanda, ile dhamira ya kutekeleza uchumi wa viwanda, bajeti zilizopita zilitekeleza kwa takriban ya wastani wa asilimia 20. Kwenye mifugo, ilitekeleza kwa takriban ya asilimia 18.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mazingira hayo yanaweza yakakupelekea ukawa na wasiwasi. Hata hivyo, wasiwasi huu unatoka moja kwa moja kwangu na imani niliyokuwa nayo ni kutokana na ile hali ya utayari wa mama yetu, hapo peke yake naamini kabisa kwamba hakutakuwa na wasiwasi kila kitu kitakwenda kama vile kilivyopangwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusisitiza kwenye hili ni nini? Nasisitiza katika utekelezaji. Naomba utekelezaji uwe wa umakini kabisa. Tukizungumzia utekelezaji hasa hasa unajikita katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni katika kutoa pesa inayohitajika, kusudi kila sekta ambayo imeomba pesa ipewe kwa kadri ya wakati na vile inavyohitajika na kwa kiwango kinachostahili. Awamu nyingine ni awamu ya utekelezaji, ambapo Wizara husika na watendaji kupitia sekta zake binafsi pamoja na halmashauri wawe wanawajibika kikamilifu kabisa kuhakikisha kila kitu wanachotakiwa kukifanya wanakifanya kama inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ambalo nataka kulizungumzia zaidi ni eneo la usimamiaji na hilo ndiyo jukumu letu sisi Wabunge pamoja na Madiwani. Sisi kisheria tumetambulika kwamba ni wasimamiaji ambao tunatakiwa tuisimamie Serikali kikamilifu kabisa. Kazi hii haiwezi kufanyika kikamilifu kama hatutapata taarifa zinazostahili katika

kusimamia mambo haya. Kumekuwa na changamoto kubwa sana katika eneo la usimamiaji hasa hasa ukiangalia kwamba watendaji wameamua kupokonya kazi hii ya kusimamia. Mara nyingi wamekuwa hawatoi taarifa kwa Wabunge ambao ndiyo wanaostahili kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu haya wanajikabidhi wenyewe na wewe kama Mbunge ukijaribu kufuatilia kupata taarifa stahiki kutaka kujua ili uweze kusimamia, kunakuwa na changamoto ya usiri na unaonekana kama wewe ni kama vile kizabizabina, lakini halikadhalika unaonekana kama wewe unajipendekeza, lakini pia unaambiwa kama wewe unajipa madaraka ambayo hustahili wakati hili ni suala letu au ni kazi ambayo sisi tumeambiwa kisheria kabisa tunatakiwa tuifanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba sana Wizara, naomba sana na Mawaziri wafanye kazi ya kutupa taarifa kabla hawajapeleka pesa ya mradi wowote, sisi tunastahili kujua mapema kuliko mtu mwingine yeyote.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja, sina shaka bajeti hii itakuwa ni bajeti yenye kuzungumzwa na kutekelezwa, lakini na kusifiwa duniani kote na miaka yote. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Hasunga, baadaye Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana na Mheshimiwa Elibariki Kingu ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi nami niweze kuchachangia

bajeti hii. Jambo la kwanza nianze kabisa kwa kuunga mkono bajeti hii ambayo kwa kweli ni nzuri sana na yenye matarajio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, kwa kweli Mungu awabariki, mnafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Awamu ya Sita kwa namna alivyosikia kilio chetu, alivyosikia kelele zetu na kuamua kuja na bajeti ambayo inaenda kujibu yale yote ambayo tulimwomba. Katika bajeti hii tumefurahi kuona kwamba kwa mara ya kwanza tunakuja sasa na chanzo kingine kwa ajili ya ujenzi wa barabara za vijijini na mijini. Kwa kweli tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaenda kujibu hoja kubwa iliyokuwa inawasumbua Wabunge kwa muda mrefu kwamba tunaenda kutekeleza huduma ya bima kwa wananchi wote. Wabunge hawa walikuwa wanapata shida sana, wanapigiwa simu kila kona kwa ajili ya kutoa fedha kuwasaidia wananchi kwenda kupata matibabu. Sasa hii tukiitekeleza, itatusaidia sana kujibu zile hoja zetu. La tatu ni mikopo ya elimu ya juu na ya nne ni miradi ya vielelezo ambayo inaenda kutekelezwa. Hivi vyanzo kwa kweli ni vizuri sana. Kwa namna bajeti ilivyo, kwa namna alivyoileta, kwa kweli inatia moyo sana na inaleta matumaini makubwa sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tulishatengeneza dira ambayo inaisha mwaka 2025 ambayo inataka maisha bora kwa kila Mtanzania ambayo tuliweka vigezo vyetu. Hapa takwimu zinaonyesha mambo mbalimbali ambayo Serikali imefanya. Nataka niseme kitu kimoja, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Awamu ya Sita na Awamu Tano kwa kazi waliyoifanya. Kwa sababu kwa mara ya kwanza, naona kilimo kimeweza kukuwa zaidi

ya wastani wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania. Kwa sababu uchumi ulikua kwa asilimia 4.8, kilimo kilikuwa kwa asilimia 4.9. Hii ni mara ya kwanza, haijawahi kutokea. Kwa kweli hii tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaangalia pia mchango wa kilimo kwenye uchumi, umechangia asilimia 26.9. Sasa hizi fedha, nikizungumzia kilimo, tukazungumzia viwanda, ndiyo msingi mkubwa na ndiyo nguzo na ndiyo vitu ambavyo tumevipa kipaumbele katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwa mfano, viwanda vilikua kwa asilimia 4.5, mchango wake kwenye pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.4, lakini ukiangalia mchango wa sekta nyingine; maji ilikuwa ni 0.5, umeme 0.3 na afya 1.4. Kwa hiyo, ina maana kuna sekta za muhimu ambazo zinachangia katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nitoe takwimu fupi. Ukiangalia ukuaji wa uchumi huu ambao tunao wa asilimia 4.8 bado wananchi wa kawaida hawawezi kuuelewa. Kwa nini? Kwa sababu mfumuko wa bei ni asilimia 3.3. Ongezeko la watu (*population*) ni asilimia 3.2. Ukizijumlisha kwa hesabu za kawaida unapata asilimia 6.5. Sasa kama hizo zote zinachukua asilimia 6.5 na uchumi unakuwa kwa asilimia 4.8 maana yake wananchi hawawezi kuona matokeo chanya ya ukuaji wa uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo basi, lazima tuweke jitihada za kuongeza ukuaji wa uchumi, ukue zaidi ya asilimia 6.5 ndipo wananchi wa kawaida tutakapokuwa tunasema uchumi umekua na wataona kweli umekua kwa sababu hata mifukoni kwao utakuwa unaonekana. Bila hivyo itakuwa haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna umaskini bado ni asilimia 25.7. Riba kwenye mabenki ni asilimia 15.75, bado riba ziko juu. Ndiyo maana nampongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Awamu ya Sita kwa hotuba aliyoitoa kule Mwanza na hatua alizozisema kule

Mwanza alipokuwa anafungua jengo la Benki Kuu, ndiyo msingi mkubwa wa hii bajeti. Ameagiza kwamba anataka riba kwenye mikopo ishuke na bila riba kushuka hatuwezi kujenga uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linaendanda sanjari na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha amesema, hii hotuba lazima tufunge mikanda, nami nakubaliana kwa sababu ametekeleza sera zote mbili, anazitumia kwa wakati mmoja katika kuhakikisha anajenga uchumi. Anatumia *Government expenditure* na *taxation*, vyote amebana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida ukibana, matokeo yake ni kwamba uchumi unaweza ukadorora. Sasa ili kusiwe na mdodoro wa uchumi lazima Benki Kuu ije na sera za fedha za kuhakikisha riba kwenye mabanki zinashuka ili kuhakikisha mzunguko wa fedha unaongezeka. Sasa hili naamini litakaa vizuri na Benki Kuu watakaa vizuri, kwa sababu kazi ya Benki Kuu ni kuangalia kila jambo ambalo Serikali inafanya na wao wanalisimamia kwa kutekeleza sera za fedha kwa kuangalia ile riba na mzunguko wa fedha. Hilo naamini wata-*balance* na ndiyo hapo uwekezaji na uchumi wetu utaweza kukua. Wasipofanya hivyo kutakuwa na mdororo wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya msingi ambayo nafikiri, kwa sababu hotuba hii imejibu karibu vitu vyote vingi, naomba nipendekeze mambo yafuatayo ili yamsaidie Mheshimiwa Waziri na kuhakikisha kwamba tunaenda sasa, tukimaliza hii miaka mitano, tunafika mahali pazuri zaidi. Jambo la kwanza napendekeza, Mheshimiwa Waziri ni vizuri ukarudisha ile Tume ya Mipango ambayo ilikuwepo. Kazi yake iwe sasa ni kufikiria vipaumbele, kuangalia vitu ambavyo nchi inaweza ikafanya, kuangalia namna ufuatiliaji na tathmini inavyotakiwa kufanyika ili utekelezaji wa bajeti na *location* ya *resources* ifanyike sawa sawa. Naamini hii tume itasaidia sana; na hii ndiyo takuwa na *dialogue* kubwa na kuwafanya watu wote waweze kushiriki katika mjadala mpana wa namna ya kujenga uchumi wa nchi yetu; *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ukiangalia sekta ya kilimo, ukiangalia viwanda, ukiangalia kwenye biashara, utaona tija bado iko chini sana. Mpaka sasa hivi hatuna chombo chochote katika nchi hii kinachozungumzia masuala ya tija, namna ya kuongeza tija, namna ya kuhakikisha kwamba tunapandisha uongezaji wa tija katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nashauri mwangalie uwezekano wa wa kurudisha Baraza la Taifa la Tija ili lisaidie katika uchambuzi na kuhamasisha na kuwa na kampeni kali ya kuhamasisha na namna ya kuongeza tija katika kilimo, kwenye mifugo, uvuvi, viwanda, na kwenye huduma mbalimbali za uzalishaji. Hiyo itatusaidia sana, itatupeleka mahali ambapo ni pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, tunazungumzia ujenzi wa *SGR* ambao utaenda kuchochea uzalishaji na kujenga uchumi wa nchi yetu hii. Nami napendekeza ile *TAZARA* upande wa nyanda za juu kusini, tunaitegemea sana. *TAZARA* ile mpaka sasa hivi ina uwezo wa kufanya kazi vizuri, lakini hatuna mabehewa ya kutosha na hatuna menejimenti ya kutosha. Kwa hiyo, ni vizuri Mheshimiwa Waziri mkaimarisha menejimenti ya lile shirika, mkaongeza mabehewa, yatachangia kwa kiwango kikubwa sana katika uchumi wa nyanda za juu kusini na hivyo tutakuwa tunaenda sambamba na huu ujenzi wa *SGR* ambayo tutajenga katika maeneo mengine. Nilidhani hiki ni kitu muhimu sana.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, kuna taarifa.

## TAARIFA

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba unavyozungumzia Shirika la Reli la *TAZARA* halina faida tu

ndani ya nchi yetu, reli ile inaunganisha Tanzania na Zambia. Hivyo uchumi wa nchi hii ya Tanzania na Zambia tuna kitu kinaitwa kwenye uchumi *comparative advantage*. Yale ambayo hayapatikani Tanzania, tunayapata sisi Watanzania na yale yanayopatikana Tanzania hayapatikani Zambia wanayapata Wazambia. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo lakini nataka nimwambie kwamba *TAZARA* ni kitu muhimu sana kwa sababu kitasaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa uzalishaji wa Mikoa za nyanda za juu. Kwa hiyo, kwa kuwa ina-*connect* na Zambia ndiyo maana tuliomba kwamba pale Tunduma, Mpemba tutengeneze bandari kavu ili mizigo yote *SADC* wawe wanakuja kuichukulia pale. Ikisafirishwa mpaka pale, naamini tutakuwa tumefanya vizuri sana katika uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, nililokuwa nataka kupendekeza ni suala la kuongeza uwekezaji katika sekta za uzalishaji. Nimeangalia namna fedha zilivyotengwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji kwenye sekta za uzalishaji bado hatujaweka vizuri. Nafikiri Mheshimiwa Waziri mkalitifakari na kuliangalia kwa mapana na marefu. Hili litasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, ambalo nataka niseme ni kuhusu sekta jumuiifu ya masuala ya fedha. Sasa hivi kuna ukwasi kwenye mabenki. Mabenki mengi hayana uwezo wa kutoa mikopo kwa sababu hawana fedha za kutosha. Hii inatokana na kwamba mabenki mengi yame-*concentrate* mijini, yanatoa mikopo kwa watu wachache, watu walio wengi hawajajumuishwa katika mfumo jumuiifu wa masuala ya fedha (*financial inclusion*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, katika jitihada ambazo Serikali ilikuwa imechukua na mkakati huu wa kuhakikisha kwamba sasa tunatumia teknolojia; mitandao hii ambayo inayo Vodacom, sijui Tigo na nini, imewafanya

wananchi walio wengi sasa waweze kuingia katika sekta jumuiifu ya masuala ya fedha. Sasa basi tunapokwenda ku-charge pale, inabidi tuchukue na tahadhari kidogo kwa sababu inaweza ikarudisha nyuma wananchi wengi kuwa katika mfumo jumuiifu. Madhara yake ni nini? Kume-manage uchumi ambao ni *informal*, ambao hauko kwenye sekta rasmi, ni kazi kubwa sana. Tukijenga uchumi ambao ni *formal*, kila mtu yuko *included*, kila mtu anaweza ku-access mikopo, kila mtu anaweza kuwekeza, hiyo itatusaidia sana katika kuweza kujenga uchumi imara na kuweza kufikia malengo yale tunayokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kwamba Waziri Mkuu wa Singapore alipokutana na viongozi wa Afrika baada ya kustaafu mwaka 1992 aliulizwa, unafikiri ni vitu gani nchi za Afrika zinaweza kujifunza kutoka Singapore zikaendelea kama nyie mlivyoendelea kule Singapore? Sasa yeye alisema, ningekuwa Rais ya Afrika, ningekuja na mambo saba.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona bahati mbaya muda haukuwa kwangu, basi naunga mkono hoja. Nataka niseme, bajeti hii tuiunge mkono kwa kila namna, tumsaidie Rais, tuisaidie Serikali ya Awamu ya Sita, tukatekeleze miradi ya vielelezo ili tuweze kufikia malengo yanayokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hasunga. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, baadaye afuate Mheshimiwa Elibariki Kingu na Mheshimiwa Aieshi Hilary, ajiandae.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kwanza kusema

kwamba naunga mkono hoja. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Masauni. Kwa kweli nawapongeza sana. Ili itifaki iwe imezingatiwa, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, mama jembe, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli bajeti hii ni bajeti ya mfano. Nina salamu nyingi kutokea katika Mkoa wetu wa Njombe. Wananchi wa Njombe wanashukuru sana, kwa kweli wanasema hii bajeti ni ya kuigwa, ya mfano, kwa sababu inakwenda kuweka pesa kwenye mifuko ya wananchi. Kumekuwa na maboresho makubwa sana upande wa kodi na sasa pesa zinakwenda kuwepo kwenye mifuko ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naanza na suala zima la Madiwani. Suala la Madiwani nimekuwa nikiliongelea sana hapa na ninashukuru Serikali kupitia Wizara imesikia kilio hiki cha posho za Madiwani na Serikali wamesema watalipa. Tunazo Halmashauri *grade* A, B na C. Hapa kuna *point* mbili; kuna suala la Serikali kuchukua dhamana ya kuwalipa Madiwani moja kwa moja kwenye *accounts* zao na vile vile kuna suala la kuongeza kiwango cha posho za Madiwani. Haya ni mambo mawili tofauti. Tutaomba wakati wa kutoa ufafanuzi, haya mambo mawili yaeleweke. Tunapochukua dhamana ya kuwalipa Madiwani moja kwa moja kupitia Serikali Kuu: Je, viwango vinakwenda kubadilika au viwango ni vile vile? Kupitia *ALAT*, maombi ya Madiwani ni kwamba viwango pia viboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine upande wa Serikali za Mitaa ni malipo ya haki ya madaraka kwa *WEO* na Makatibu Tarafa. Kwa upande watendaji wetu, unakuta mtendaji mmoja ana vijiji tuseme vitatu au vine, analipwa shilingi 100,000, posho hiyo, jambo ambalo nalipongeza sana na kuliunga mkono. Katibu Tarafa, ana vijiji takribani mara nne ya yule Mtendaji wa Kata. Sasa huyu katibu wa Tarafa naye tunamlipa shilingi 100,000 na huyu *WEO* naye shilingi 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi kutoka kwa Makatibu Tarafa ni kwamba kile kiwango cha mafuta walichokuwa wanapewa kutoka kwa ma-DAS kibaki pale pale, waendeleo kusaidiwa. Kwa hiyo, hii shilingi 100,000/=, wanayopewa Makatibu Tarafa, isiwe mbadala kwamba hawatapewa tena ile pesa waliyokuwa wanapewa kutoka Ofisi za ma-DAS, kwa sababu kazi za Makatibu Tarafa ni zaidi ya kazi ya Watendaji wa Kata. Sasa viwango hapo vinafanana. Kwa hiyo, ni ombi maalumu ambalo tunaweka mezani kwamba kuna kiwango walikuwa wanapewa kutoka ofisi ya DAS kiendeleo kuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha hilo, niendeleo kuomba Wizara isaidie sana mashine za *ki-electronic*. Watendaji wetu wa kata wote wapewe zile mashine za kukusanyia mapato za *ki-electronic* ili mapato yasipotee, tunapojadili bajeti, mabato yaeleweke. Baadhi ya Watendaji wa Vijiji bado wanakusanya mapato kwa mkono (*manually*), siyo *electronic*.

Kwa hiyo, tunaomba sana mashine za kukusanyia mapato za *ki-electronic* ziende vijijini. Katika masoko bado tunakusanya mapato kienyeji. Katika *stendi* zetu bado tunakusanya mapato kienyeji bila mashine. Suala hili la mashine za *ki-electronic* tunaomba sana lizingatiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo pia linaweza lika-*boost* mapato, tunayo mikoa mipya; Njombe ni miongoni mwa mikoa ambayo ilipatikana dakika za hivi karibuni; Simiyu, Geita, Katavi na mengine. Mikoa hii mipya makao makuu ya mikoa hii mipya, mpaka leo makao makuu mengi hayajawa Manispaa. Tuangalie Makao Makuu ya mikoa hii mipya kama inakidhi kuwa Manispaa. Naleta salam kutoka Mkoa wa Njombe. Njombe tunaomba iwe Manispaa. Halmashauri ya Mji wa Njombe tumeshakaa katika vikao vya DCC na tunakidhi. Tufanye...

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana subiri. Mheshimiwa Kanyasu Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa taarifa mchangiaji. Kwanza anachangia vizuri sana na moja ya mikoa mipya anayozungumza Makao yake Makuu ni Geita Mjini, ambayo imekidhi viwango vya kuwa Manispaa tangu mwaka 2018. Nilikuwa nampa tu taarifa tu Mheshimiwa.

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naipokea taarifa hiyo na nadhani hizi salamu sasa zinazidi kukamilika kwa Serikali. Hii mikoa ni yetu, tunaweza tukasubiri vile vigezo kwamba kwa sababu tumeamua tuwe na mikoa mipya, mikoa hii mipya lazima viongozi wetu wa Kitaifa, Waziri Mkuu aende pale. Sasa mkoa mpya usipoweka *airport*, Waziri Mkuu anaendaje pale?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi, Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nataka tu nimpe taarifa mchangiaji anayechangia sasa kwamba anapoendelea kuchangia, akizungumzia maslahi ya Mkoa wa Njombe asisahau kuzungumzia maslahi ya Mkoa wa Ruvuma jirani yake, kwamba Mkoa wa Ruvuma nao pia ni Mkubwa sana, unahitaji kugawika ili tuweze kupata Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Selous. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dalili kwamba upande wa Serikali za Mitaa

tukiboresha mifumo mapato yanaongezeka; unapofanya Manispaa au mikoa miwili, miundombinu inaongezeka. Kama pale Njombe tunakuwa na uwanja wa ndege, boshi wetu Waziri Mkuu akija, ana-fly kutoka Dodoma. Ana-land pale, anatembelea mashamba ya parachichi, hatumtoshi *byroad*, kwa sababu anakazi nyingi. Kwa hiyo, tunaoma Mkoa wa Njombe na mikoa ya mingine ambayo ni mipya ipewe Manispaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuwa na Manispaa, kuna miradi ya kimkakati. Tuchukulie mfano stendi mpya ya mabasi, ile ya pale Dar es Salaam, Mbezi Luise. Sasa mradi kama ule utawekaje mahali ambapo ni *Town Council*, siyo Halmashauri ya Manispaa? Maana kuna miradi inaenda kwenye jiji, kuna miradi inakwenda Manispaa na miradi inayokidhi *Town Council*. Hii mikoa tuliamua sisi iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wakati muafaka sasa tuone namna gani Makao Makuu ya mikoa hii mipya yanakuwa Manispaa kwa maslahi ya Watanzania na kwa faida ya Watanzania. Tuchukulie mfano, pale Njombe ikiwa Manispaa, unakuta bidhaa zote za kilimo kutokea Makete lazima zipite Manispaa. Viazi, chai inayotoka Lupembe, lazima ipite pale Njombe Manispaa. Kule Ludewa kuna Ziwa Nyasa, samaki lazima zipite Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inapokuwa manispaa miundombinu, barabara za lami, mabenki uwekezaji unakuwa mkubwa kule ziwani kule ni mbali na tuendelee kuwa wanachama wa maziwa makuu sisi kama nchi tuendelee kuwa wananachama wa *great lakes network* itatusaidia sana kuweza kufanikisha uwekezaji katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala zima la mchuchuma na Liganga kwa kweli nina *salute* Mheshimiwa Rais amezungumzia Lichuchuma na Liganga. Lichuchuma na Liganga wanasema kuna *political will*. Rais wetu mama yetu mpendwa amesema tatizo ni nini leo Waziri amejibu maswali vizuri sana hapa swali lililoulizwa na Mbunge wa Jimbo kuhusu

Mchuchuma na Liganga. Tunapongeza sasa tuanze madiwani wanaongelea Wabunge Mchuchuma na Liganga Mheshimiwa Rais Mchuchuma la Liganga sasa shida iko wapi? Hapo sijaelewa kwa hiyo suala hili Mheshimiwa tuimairishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* naunga mkono, *TARURA* tumetenga hizo milioni 500 kila jimbo tukumbushane *TARURA* ilikuwepo ipo na itaendelea kuwepo sasa hizo pesa zinapoenda tunatoa shukrani nyingi lakini ionyeshe tofauti isiwe kama wakati ule wa mwanzo wanasema *business as usually* tuone namna gani pesa hizi zikienda zionyeshe tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu ni mapato yanayotokana na uchumi wa *blue*. Uchumi wa *blue* ndani yake kuna bahari, uchumi wa *blue* ndani yake kuna *costal area* zote, uchumi wa *blue* ndani yake kuna maziwa Tanzania peke yake tuna maziwa yasiyopungua tisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na haya maziwa *lakes great lakes* ni muhimu sana haya maziwa, Mungu ametuletea bahari atulipiii hiyo bahari ina samaki tunaweza tukavua kwa wakati wowote kwenye haya maziwa tunavua. Kwa hiyo, muhimu sana tuangalie uchumi wa *blue*.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Nadhani ni kengele ya kwanza ya...

**MWENYEKITI:** Ya pili!

**MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili naunga mkono hoja ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana tunaendelea na Mheshimiwa Elibariki Kingu,

Mheshimiwa Aeshi Hilaly na Mheshimiwa Subira Mgalu  
ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu, nimebahatika kuwa Mbunge hii ni *term* yangu ya pili kwa maana ni mara yangu kuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishiriki kupitisha bajeti zote za Serikali kwa Bunge lililopita ninaomba niwe *honest* kwa mara yangu ya kwanza toka nimekuwa Mbunge nimeshuhudia bajeti iliyobeba dhima halisi ya wale waliotutuma kwa maana walipa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza, kama Mbunge nimeshuhudia kiwango kikubwa sana cha kasi ya upelekaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika halmashauri zetu. Ninaomba niseme kwa dhati ya moyo wangu na Kiongozi Mkuu wa shughuli za Serikali kipenzi chetu Waziri Mkuu Kassim Majaliwa yumo humu ndani. Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe na Naibu wako Mheshimiwa Eng. Masauni mmewatendea haki sana walipa kodi na wananchi waliotutuma katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndugu yetu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alikuwa Singida ndani ya siku moja mbili zilizopita, na nitaka nilisema hili Mheshimiwa Waziri Mkuu nanijuwa na huko hapa na ninajua Mheshimiwa Gulamali atatulia niseme wema wa Waziri Mkuu aliyeuonyesha kwa watu wa Singida akiwa ameambatana na Waziri wa Kilimo na Naibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi wa Singida wanakupongeza kwa jambo kubwa moja, ulipokwenda Singida kwa *agenda* ya zao la Alizeti ambalo ni zao la Serikali la kimkakati, ulitumia zaidi ya masaa nane ukiwa umekaa kwenye meza ukisikiliza hoja za

wananchi wetu na walipa kodi wetu mmoja baada ya mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu usikivu wako wananchi wametutumia meseji na ushahidi tunao wanasema hawajapata kuona kiongozi wa kiserikali, wa nafasi kubwa kama Waziri Mkuu anaweza kukaa na akatulia kwa masaa zaidi ya nane akisikiliza michango ya wananchi tena wananchi wengine ambao hawana hata uelewa mpana wa mambo ya kimkakati ya kiuchumi, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu uliwasikiliza wananchi wa Singida wakatoa mawazo yao wakatoa wanataka *direction* gani katika *production* ya *sunflower* katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niungane na wananchi wa Mkoa wa Singida kusema kabisa kwa dhati ya moyo wangu kama kuna karama za kiuongozi Mungu anazitoa, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri wetu Mkuu umepewa karama kubwa sana ya kiuongozi karama ya kuwa na unyenyekevu wa hali ya juu ya kujishusha *to the ground* na kuwasikiliza walipa kodi. Umetupa somo kubwa sana sisi vijana tunaokuwa katika uongozi ahsante sana kiongozi wetu Mungu akubariki sana kaka yangu. (Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la Alizeti ni zao ambalo Serikali ya Awamu ya Sita na niwapongeze sana Mawaziri wa Wizara hizi mbili ni zao ambalo wameamua kwa dhati kulifanya kuwa zao la kimkakati na ninataka nitoe takwimu zifuatazo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tuna *make seventy eight percent* ya *market share* ya uzalishaji wa mafuta ya Alizeti katika ukanda wa *East Africa* na baadhi ya nchi za maziwa makuu ikiwemo Zambia, pamoja na Kongo. Asilimia 78 ya *market monopoly* Tanzania tumeikamata, nchi inayotufuata kwa mbali sana ni Uganda kidogo, wakifuatiwa na Rwanda ambazo *production* yao ni karibia tani kama 4,000 kwa mwaka mzima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukisema na ninaomba kabisa Waziri Wizara ya Fedha na Naibu mnisikilize, hili mkiweza kulichukuwa wazo langu nina imani kabisa mtakwenda kuifanya Tanzania inakwenda kuwa *another giant* katika kuliteka soko la Afrika kwa sababu anayeongoza ni *South Africa* ambaye amekamata 48, 46 percent ya *production* ya mafuta haya katika ukanda mzima wa Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize ushauri wangu tumeweka *incentive* kwa wale tunawaita *strategic investors* katika sekta ya *sunflower production*. Kwa Mkoa wa Singida *strategic investor* tunaye huyu mmoja katika kile kiwanda kikubwa cha uzalishaji, viwanda vingine huyu yeye amepewa *zero VAT* kwa maana ni muwekezaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilipe Bunge lako taarifa katika zao hili la Alizeti takwimu zimeshasomwa na hapa Bungeni namna gani Serikali na Taifa tunatumia a *lot of forexes* kuagiza mafuta kuja ndani ya nchi. Na wakati mwingine mafuta haya uenda yanakuwa hata hayana ubora ule tunaoukusudia. Tanzania tukiamua kwa mipango thabiti na tumepata Waziri wa Fedha naomba nikiri msikivu sana anayefikika kwa haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu na kiongozi wetu Mkuu wa Serikali yupo hapa Bungeni, ushauri wangu ninaomba Wizara ya Kilimo Wizara ya Biashara na Masoko sijui na vitu gani ninaomba kwa dhati ya moyo wangu chukueni ushauri huu. Nendeni mkaangalie wale wazalishaji wadogo wa mafuta katika Mkoa wa Singida na mikoa jirani, wazalishaji wale mkienda kuwaangalia wawezesheni wapate mashine za kisasa katika kuhakikisha ya kwamba ukamuaji wa mafuta unakidhi tija kwa sababu mashine nyingi wanazotumia hazina ubora wa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkiweza kulifanya hili Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara ya Viwanda na hii chachu mliyokuja nayo ya kuleta mbegu za kisasa katika zao

la Alizeti nataka niwaambie kwa idadi ya wakulima tulionao wa Alizeti kwa Mkoa wa Singida peke yake Mkuu wa Mkoa amekuja na takwimu kwenye kikao cha Mkuu wa Mkoa Singida peke yake kwa wakulima wetu tunauwezo wa *cover production* ya nchi nzima ya Alizeti na tukabusti uchumi wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mheshimiwa Bashe ushauri wangu ninawaomba kwa kuwatumia wakulima hawa ambao umeamua kuwekeza kwao, nataka niwaambie Singida tunayo ardhi ya kutosha yenye rutuba, tuna watu akina baba wenye uwezo wa kufanya kazi tuko tayari tukiwezeshwa na Serikali kuhakikisha tunazalisha tuweze kupiga hatua katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kuliongelea juzi nimetembelea Kisarawe nimetembelea Wilaya ya Mkuranga anapotoka kaka yangu na Waziri mahiri kabisa kijana Mheshimiwa Ulega usipokuwa makini unaweza ukafikiri hili Taifa watu wanafanya ngonjera hili Taifa linapiga hatua *this country is moving* nchi hii inapiga hatua kubwa ya kimaendeleo ya kiuchumi, tumekwenda pale kwenye kiwanda tukiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye Kamati ya Sheria na Katiba tumejionea uzalishaji wa *gypsum* kwenye kiwanda kile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumza kiwanda kile ambacho kipo kwenye nchi yetu ya Tanzania kime-*capture market* ya nchi saba Afrika Kenya, Zambia Malawa Msumbiji mpaka Zimbabwe wanauza *gypsum*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu Mheshimiwa Waziri kiwanda kile cha kimkakati kina changamoto moja kubwa na nilizungumza hapa Bunge lililopita kuhusiana na mifugo watu wengine wakaniona na *attack personality* za watu leo Serikali mmefanya *research* ushauri niliutoa yale matozo yote ya kwenye nyama mmeyafuta wananchi kule wanapiga makofi *production* ya nchi itaongezeka ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Mifugo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wamefanya kazi matozo niliyoyasema hapa Bungeni wamefanya utafiti wamejiridhisha leo nimesoma ripoti ya Waziri wamefuta zile tozo ninawapongeza sana Wizara ya Fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba nendeni mkakitembelee kile kiwanda Wizara ya Fedha mimi kila jambo nikilizungumza hapa ninazungumza kwa maslahi ya Taifa langu siweki maslahi yangu ninazungumza maslahi ya nchi mtu achukie apende asipende nimeiweka Tanzania yangu mbele kwa maslahi ya vizazi vinavyokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu nendeni mkakitembelee kiwanda kile cha Mkuranga wale watu wana changamoto moja Mheshimiwa Waziri karatasi wanazozitumia katika ku-cover ile *gypsum* haipatikana Tanzania karatasi ile inakuwa *imported* kutoka nje ya nchi na inapekelekea *cost of production* inakuwa kubwa inasababisha bidhaa inakuwa na bei kubwa na ninataka nikuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kile wakati wana *ki-acquire* kilikuwa na uwezo wa kuzalisha milioni 4 waka-*expand* uzalishaji mpaka milioni 15 na *actual production* ni milioni nane wameweza kuliteka soko lote la Afrika na Mheshimiwa Waziri Mkuu nilifanya upelelezi kutaka kujua *resources* tulizonazo zinazoweza kukifanya kiwanda hichi ku-*sustain* tumeambiwa ma-*gypsum powder* tuliyonayo yanaweza yakazalisha *gypsum* kwa zaidi ya miaka 40 na yapo yakutosha kwenye Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba Waziri wa Fedha wewe na naibu wako fanyeni utafiti wa kitaalam tumieni vyombo vyetu vya kiserikali nendeni mkawasaidie mwekezaji huyu ajira aliyoitoe nilipoona sikuamini kama niko Tanzania, sikuamini kama niko kwenye nchi hii ya Tanzania, msaidieni mwekezaji huyu aweze kupata nafuu ya kodi kwenye hii kodi moja ya makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnaona hilo haliwezekani pelekeni fedha kwenye kiwanda chetu cha kuzalisha karatasi nunueni mitambo izalishe karatasi wapate *market* ya kuuza kwa mwekezaji huyu mtakuwa mmesaidia na mtakuwa mmeliongezea nguvu Taifa katika kuzalisha kodi wanayolipa wale watu na *production* wanayofanya nimekwenda kulala usingizi hata...

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa!

### T A A R I F A

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge anavyozungumzia suala la kiwanda kinachozalisha karatasi nchini ni Mgololo kiwanda kile kile nimefika pale na nimeona uzalishaji wa kiwanda na kina changamoto ya masoko ya ndani ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kingu malizia washa *mic* umalizie muda wako.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwanza taarifa lakini aina ya karatasi ninazozungumzia za *gypsum* sio karatasi kama hizi ni karatasi ni *industrial paper* zinazotumika kwenye *gypsum*. Ambazo mwekezaji huyo anatumia fedha nyingi kuzi-*import* Mheshimiwa Waziri Mkuu kaka yangu kama tunaweza tuone fedha kwenye kiwanda kile kilete mitambo ya kisasa kizalishe karatasi kwa sababu soko tayari lipo *unless otherwise* mpeni msamaha wa kodi mwekezaji huyu anayeleta ajira kwenye Taifa letu na kusababisha *TRA* kukusanya kodi ya kutosha katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti muda umeisha!

**MWENYEKITI:** Kengere imepiga zamani nimekuachia.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.Tunaendelea Mheshimiwa Aeshi Hilaly baadaye Mheshimiwa Subira Mgalu na Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana anayoifanya na hatimaye wananchi wote watanzania wote kwa ujumla wameridhika na mwendo kasi anaokwenda nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba tumuombe Mwenyezi Mungu aendeleo kumpa afya njema aendeleo kututumikia sisi wananchi ambao kwa sasa tunaimani kubwa sana kwa yale yote ambayo ameanza nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya hapa ndani ya Bunge, lakini vilevile amekuwa ni mwepesi pale anaposikia kuna tatizo basi anakwenda haraka sana na kwenda kulitatu tatizo lile ambalo sisi kama Wabunge huwa tunatoa miongozo humu ndani na mwisho wa siku inawezekana taarifa ikawa ya uwongo au ya kweli lakini alikuwa mtu mwepesi wa kwenda kulishugulikia tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tatu naomba niwapongeze sana mawaziri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu namfahamu vizuri sana ni mchapakazi na mzalendo lakini Mheshimiwa *Engineer* Masauni ambaye ni kijana mwezangu

tumekuwa tukifahamiana kwa kweli ni wazalendo wawili ambao wamekidhi kushika nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja tatu lakini moja nimekuwa nikilia ndani ya Bunge Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumekuwa tukipitisha bajeti kila mwaka kuhusiana na uwanja wa ndege wa Sumbawanga Mjini, uwanja ule una faida kubwa sana kwetu lakini mwaka juzi nilipiga makofi hapa nikapiga kelele na hatimaye nikaahidiwa kujengewa uwanja wa ndege na bajeti ikapita, mwaka jana vivyohivyo na mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ameisema, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameitaja tena kaitaja mara mbili uwanja wa ndege wa Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu nipate uhakika tu kutoka kwake wakati anakuja kutujibu mwaka huu ni kweli tutafanikiwa kujengewa uwanja wa ndege hilo nataka nilipate kwa sababu juzi tumeenda kumzika mzee wetu Mheshimiwa Marehemu Mzee Mzindakaya tulikuwa na Mheshimiwa Spika tumepata shida sana kutua katika uwanja ule. Na yeye mwenyewe Mheshimiwa Spika akaridhika na akaahidi ndani kwa wananchi pale kwamba kwa mwaka huu wa fedha atajitahidi kupambana kuhakikisha kwamba uwanja wa ndege ule unajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikuombe sana kama una viwanja kumi unataka kujenga mwaka huu kiwanja namba moja kiwe kiwanja cha Sumbawanga Mjini ni aibu kubwa tunaposafiri sisi kutoka hapa mpaka Mpanda wakati Mpanda imezaliwa kutoka Mkoa wa Rukwa wana uwanja wa ndege wa lami Sumbawanga hatuna uwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Songwe wameweza kupata uwanja wa ndege kabla ya Sumbawanga kwa hiyo utaangalia kero tunayoipata sisi Wabunge, lakini na wananchi pamoja na Mheshimiwa Rais mwenyewe wakati anasafiri kuja kwenye kampeni kero kubwa...

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**MWENYEKITI:** Taarifa!

## T A A R I F A

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimpe mzungumzaji taarifa kwamba ule Mkoa wa Songwe huko Mkoa wa Mbeya na sio Mkoa wa Songwe kwa hiyo hata sisi Mkoa wa Songwe tunahitaji bado kiwanja ahsante (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hilaly.

**MHE. AESHI K. HILALY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naipokea taarifa lakini nataka niseme ukitaka kujua kero hiyo waulize viongozi waliopita Mkoa wa Rukwa wanashuka Mbeya, kutoka Mbeya uwanja wa Songwe mpaka uikute Sumbawanga kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga kuna matuta zaidi ya mia 250 na hayo matuta kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi hayuko hapa, lakini Mheshimiwa Kamwele ambaye alikuwa Waziri pale aliahidi mbele ya marehemu Mheshimiwa Rais John Pombe Mafuguli kwamba ndani ya miezi mitatu atakuwa ameondoa yale matuta, yale matuta ni kero kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukuombe kama matuta hayawezekani kuondolewa uwanja wa ndege iwe kipaumbele cha kwanza mwaka huu tujengewe uwanja wandenge ili uweze kurahisisha usafiri wa kwenda maeneo yale. Maeneo ya Rukwa yana vivutio vingi sana vya utalii lakini hatuwezi kupata watalii kuja kule wakiangalia kero ya usafiri ya kutoka Dar es salaam mpaka uikute Sumbawanga kwa hiyo utakuta unachenji karibuni mara tatu mara nne kubadilisha usafiri ili uweze kufika Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa uzalendo wenu kwa uchapakazi wenu, kwa urafiki wenu baina nyie na mimi

mwaka huu ule uwanja utajengwa kwa kiwango cha lami.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili hoja yangu ya pili ni kuhusiana na *property tax*, Serikali ina nia njema sana na naunga mkono zoezi hilo lakini linanipa changamoto kidogo nikasema nijaribu kuchangia bajeti hii ni nzuri lakini nikasema nichangie kwa sababu ya wasiwasi na wasiwasi ni akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema tunachaji kupitia kwenye hizi *LUKU* za *TANESCO* lakini bahati mbaya kuna nyumba nyingine kiwanja kimoja zimejengwa nyumba nne na kila nyumba moja ina *LUKU* ya kwake sasa sijui kama tutakuwa tunalipa *property tax* au tutakuwa tunalipa kila mpangaji ana lipa ile kodi nilitaka nijue nifafanulie kidogo.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimejikuta Dar es Salaam pale kuna mtu ana *apartments* zaidi ya 20 au 30 na kila mtu ana *LUKU* yake. Sasa ile *property tax* maana yake ni nini? Ni kodi ya jengo au ni kodi ambayo kila mpangaji anatakiwa alipe? Hilo unatakiwa unipe ufafanuzi kidogo kwa sababu nimekaa nikiwaza sana sipati majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo haliniingii akilini. Nimekuwa nikilalamika hapa Bungeni na kwenye Kamati nilipokuwepo. Kuna hawa watu wanaotengeneza *LUKU* kuwauzia *TANESCO*. Nitatoa mfano wa Kampuni wanatengeneza *LUKU* wanawauzia *TANESCO*, baadaye wanakuja kutengeneza *sub meter*, inatengenezwa na huyo anawauzia wananchi ambao ni wawekezaji wanaojenga *apartments* hizi, wale wanafunga *LUKU* zao wenyewe, wananunua umeme kutoka *TANESCO* wanawauzia wananchi wale ambao ni wapangaji, wao wananunua kwa shilingi 380 kwa uniti lakini wao wanawauzia shilingi 500 kwa uniti moja, sasa ninataka nijue je, Serikali imeruhusu wafanyabiashara kuuza umeme ambao unazalishwa na *TANESCO*? Ninachokijua mimi ni kwamba mfanyabiashara au mwekezaji anaweza akazalisha umeme

akawauzia *TANESCO* na *TANESCO* wajibu wake ni kuwauzia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zimeibuka kampuni nyingi na kwa bahati mbaya sana kampuni hiyo hiyo inatengeneza *tokens* inauza bila Serikali kujua. Ile kodi anayouza kwa faida anamlipa nani? Mheshimiwa Waziri wa Fedha jambo hili liangaliwe sana. Watu wa *TANESCO* wanafahamu na hii ndiyo biashara yao baina ya *TANESCO* na hao ambao wanauza umeme kwa wapangaji wadogo wadogo.

Nitakutolea mfano, mtu ana jengo lenye kama *apartments* kumi, ananunua umeme wa *TANESCO* anafunga *LUKU* ya *TANESCO* moja halafu anachukua *sub meter* anafunga. Wale waliofungiwa *sub meter* wananunua tena *token* ambazo Serikali au *TANESCO* hawafaidiki na chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo kuna vitu viwili kwanza wanavunja sheria, lakini la pili, wanatengeneza faida. Je, ile faida tunawajibikaje sisi kama Serikali tunapata wapi kodi kutokana na hilo jambo? Mheshimiwa Waziri nikuombe, kama utapata nafasi mniite niwaeleze kwa sababu jambo hili nimekuwa nikilifuatilia sana ni wakwepaji wakubwa wa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu lingine ni kwamba kwenye nyumba hizi nyingine kama *National Housing*, tunafungulia luku za *TANESCO* ambazo kila mwananchi aliyepanga atalipa moja kwa moja *property tax* kupitia luku. Je, hawa waliofungiwa *sub meters* wanamlipa nani hiyo kodi ya pango? Tunajua? Hatujui! Ipo kwenye mfumo? Haipo kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo nataka niseme liangalie hili, *TANESCO* wanafahamu tatizo hili na tumekuwa tukihoji sana, nani kawapa leseni ya kuuza hizo *tokens*? Na watengenezaji wapo. Wale wafuatilieni muone miaka mitano hii hiyo biashara waliyokuwa wanaifanya wamemlipa nani kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niipongeze Serikali imeweza kuangalia Madiwani wakasema wanaweza wakalipwa moja kwa moja kutoka Wizarani. Tumeangalia Makatibu Tarafa, tutawalipa laki moja kutoka Wizarani, lakini tumeacha changamoto moja ya Watendaji wa Kata ambao na wenyewe tumewaongezea posho shilingi laki moja, lakini umetoa maelekezo kwamba shilingi laki moja hizi zitalipwa moja kwa moja na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kutengeneza tatizo lingine. Watakopwa wale jamaa mpaka mwisho, na hakuna Mtendaji wa Kata atakwenda kumfuata Mkurugenzi wake akadai malimbikizo ya madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninataka niseme kwamba huu mfumo ambao tumeuanzisha mwanzo kwamba Madiwani watalipwa moja kwa moja kutoka Hazina na Makatibu Tarafa watalipwa posho ya shilingi laki moja, na Watendaji ambao tumewaongezea shilingi laki moja walipwe moja kwa moja kupitia Hazina. Tukiwaruhusu wapewe na Halmashauri kutokana na mapato ya ndani hizo hela hawatazipata kamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, hilo ninakuomba kwamba kama kuna uwezekano basi na hizi posho za Watendaji wa Kata zihamishiwe moja kwa moja Hazina ili waweze kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa ni huo. Lakini kubwa ni suala la *TANESCO* na *LUKU* na hizi *sub meters* ambazo zinasambazwa kwenye *apartments* nani anawajibika katika hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aeshi Hilaly. Tunaendelea na Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Kunti Majala na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere wajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa nafasi kusimama ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Masauni, pamoja na watendaji wote kwa maandalizi mazuri, pamoja na Mawaziri wote kwa Wizara mbalimbali ambazo zilikuwa msingi wa kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi nzuri anayofanya. Waziri Mkuu amekuwa *champion* wa mazao mbalimbali ya kimkakati, utamuona kwenye mazao ya korosho, pamba, alizeti na mkonge. Katika u-*champion* wake umesababisha Serikali kuleta marekebisho mbalimbali ya tozo kwenye mazao hayo ili kulinda uwekezaji wa ndani na kuwawezesha wakulima. Kwa hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi anazoendelea kufanya. Na kutokana na uwajibikaji wake unaoendelea, na matokeo mazuri ya bajeti iliyowasilishwa, imenifanya nikumbuke maneno aliyoyasema kwenye hotuba yake baada ya kuapishwa tarehe 19 Machi, 2021 pamoja na huzuni aliyokuwa nayo, Mheshimiwa Rais alisema yafuatayo: nanukuu "*Huu si wakati wa kutazama mbele kwa mashaka, bali ni wakati wa kutazama mbele kwa matumaini na kujiamini.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya yamejidhihirisha kwa kazi mbalimbali zinazoendelea. Sambamba na hilo kwenye ukurasa wa sita wa bajeti aliyowasilisha Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba amenukuu

ahadi ya Mheshimiwa Rais, mama Samia Suluhu Hassan ya kudumisha mazuri ya awamu zilizopita kuyaendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya. Kwa kazi zinazoendelea tumemuona kwenye ujenzi wa *SGR*, uwekaji wa jiwe la msingi kipande cha Mwanza – Isaka, tumemuona akishuhudia mikataba ya ujenzi wa meli tano Mwanza jioni hii. Tumemuona kwenye uzinduzi wa kiwanda cha kuchakata dhahabu yote haya yanadhihirisha ahadi yake ya kuendeleza mema yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala ya kuleta mengine mapya ambapo ndipo nitakapojielekeza, napenda niipongeze Serikali kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuamua kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi zaidi ya trilioni nane kwa utaratibu wa *non-cash special bond* isiyotumia pesa, haijapata kutokea. Wastaafu wa nchi hii wanakwenda kupata ahueni hata sisi watoto wa wastaafu tunashukuru kwa hatua hii ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Serikali imekuja na ubunifu wa kuangalia vyanzo vingine vya mapato kwa kuwa na mtazamo wa kuja kutumia masuala ya *Euro bond*, pia kwa kujielekeza Serikali kufungua soko la ndani la hati fungani kwa wawekezaji wa nje, Serikali kuanzisha bima ya afya Watanzania wote, Serikali kuamua kulipa posho za madaraka kwa Watendaji wa Tarafa na Kata, Serikali kuanza kuzipa mitazamo mipya Halmashauri zetu za Majiji na Manispaa kutumia masuala ya hati fungani katika ku-*finance* miradi yao ambayo inakwenda kupunguza mzigo wa Hazina kutoa pesa kwa ajili ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee katika hilo, nipongeze ubunifu wa kupendekeza vyanzo vya mapato kuongeza Mfuko wa *TARURA* kwa ajili ya barabara zetu. Hapa nishukuru kwa kiasi cha bilioni nne na milioni mia tano ambazo Mkoa wetu wa Pwani tumezipokea na pendekezo la bilioni 322. Niwaombe Watanzania barabara za vijijini ni kila kitu zinasafirisha malighafi, zitawezesha viwanda vyetu, zitapunguza gharama za uzalishaji, zitawawezesha akina mama kufika kwenye vituo vya afya, zitapunguza gharama

za usafirishaji. Kwa muktadha huo naomba nishukuru kwa kusema kwamba barabara ya Chalinze – Nsigi – Talawanda – Bago inakwenda kupata faida hii. Barabara ya Lugoba – Mindukene – Talawanda – Magulumatari, barabara ya Kibiti – Mkongo – Mwaseni inaenda kupata faida ya hela hizi. Barabara ya Bungu – Nyambunda; barabara ya Kimanzichana – Mkamba – Panzui – Msanga, maeneo ya Mkoa wa Pwani ndiyo maana tuna sababu ya kuunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti hii kwa sababu Serikali imekuwa sikivu. Kamati yetu ya Bajeti imependekeza mambo mengi lakini kati ya hayo pamoja na Wabunge wote Serikali imechukua zaidi ya asilimia 70 ya mapendekezo hayo. Hii inaonesha namna gani Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba pamoja na timu yako, mkiongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, mmeweza kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais wetu, naye amekubali mapendekezo hayo leo yapo ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la miradi ya maji; pendekezo la kuongeza tozo kwenye masuala mazima ya mawasiliano kwa ajili ya kusaidia miradi ya maji, naomba Watanzania tuliunge mkono hili jambo kwa sababu maji nayo ni uhai, maji ni kila kitu. Sambamba na hilo, ninaomba tu kutoa ushauri kwenye suala zima la nia ya Serikali ya kufuta msamaha kwenye suala la taa za *solar*. Katika hili niombe Serikali yangu Sikivu ilitazame tena hili. Kwa sababu yapo maeneo bado yanatumia umeme wa jua na bado yapo matumaini, kwa mfano maeneo ya Visiwa vya Kibiti, maeneo ya Mbwela Mashariki, Mbwela Magharibi, Maparoni, Salale na Mkuranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Visiwa vya Kwale, Koma, tuna Visiwa vya Bwejuu, Jibondo, maeneo ya Mafia bado tunasubiri umeme wa *solar*. Kwa hiyo niombe sana tozo hii, vifaa vyote vya umeme viendeleo kusamehewa kodi ili kuweza kuwafanya Watanzania wenzetu wanaoishi visiwani waweze kupata huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa mkakati wake wa kuweza kutaka kupandisha vyeo watumishi wa Serikali. Mmetenga bilioni 400 kwenye bajeti kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi 92. Niwaombe tu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Mchengerwa kuzisimamia pesa hizi zitumike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo utaratibu mara nyingi maafisa utumishi wamekuwa wakichelewa kuwapandisha watumishi vyeo, badala yake hela hizi unapofika mwisho wa mwaka zinakuwa zimesalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niunge mkono hatua zote za Kiserikali za kufanya maboresho ya kodi mbalimbali zenye nia ya kulinda viwanda vyetu. Sisi Mkoa wa Pwani tunashukuru ulindaji wa viwanda vya marumaru, vipo viwili tu nchi nzima ambavyo ni kiwanda cha Keda Chalinze na kiwanda cha *Goodwill* Mkuranga. Tumeona namna ambavyo Serikali mmetia mguu katika marumaru inayouzwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile hiyo haitoshi kwa upande wa akina mama tunashukuru tozo mbalimbali ambazo zimeondolewa kwenye masuala ya kilimo cha mbogamboga na matunda, kwenye masuala ya usindikaji wa maziwa, kwenye masuala ya bima ya mifugo, kwenye masuala ya mazao mbalimbali ambayo ama kwa hakika tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimalizie kwa kuwapongeza Kamati yetu chini ya Mwenyekiti kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti hapa ndani. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hatua yake ya kuupa msukumo mradi wa kusindika gesi asilimia Mkoa wa Lindi, mradi wa Mchuchuma Liganga, mradi wa bomba la mafuta, yote haya ambayo yamewekewa hatua za kikodi ili miradi hii iweze kuchangia ajira kwa Watanzania, iweze kuchangia mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Balozi wa kuhamasisha kodi, nimalizie kwa kuwaomba Watanzania

kulipa kodi kwa sasa hivi na hatua zinginezo. Niwaombe tuendeleo kulipa kodi ni umeme, imepunguzwa sasa hivi 27,000 maeneo yote, kodi ni elimu kwa vijana wetu, Serikali imeongeza zimefikisha bilioni 500 kila kijana wa Tanzania atakayekuwa na sifa za kwenda chuo kikuu atapata mkopo, hiyo ndiyo kodi ya Watanzania. Pia kodi ni barabara kila kijiji cha nchi hii kitapata barabara. Kodi ni madawa tumeona mtazamo wa Serikali wa kumaliza maboma 8,000 na vituo vya afya 1,500 pia kuongeza madawa bilioni 263 zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe wafanyabiashara, mazingira wezeshi katika bajeti hii yameainishwa, mmepunguziwa viwango mbalimbali vya kodi, mmepunguziwa urasimu mbalimbali lakini kubwa Serikali imeweza kutatua mfupa wa asilimia 15 ya gharama za sukari ya viwandani. Wafanyabiashara mmeachiwa ili kuongeza ukwasi kwa uchumi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sote kwa pamoja tumuunge mkono jemedari wetu, mweledi, mchapakazi, mama yetu kipenzi, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan na tunakuombea dua, Mwenyezi Mungu akujalie na tunaamini utatufikisha pale panapostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Subira Mgalu. Tunaendelea na Mheshimiwa Kunti Majala, baadaye Mheshimiwa Mwita Getere, Mheshimiwa Janejelly James na Mheshimiwa Haji Amour Haji wajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kunipatia nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya Awamu ya Sita ambayo tunaianza mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kuipongeza Serikali. Tangu lilivyoingia Bunge la Kumi na Moja kilio changu kilikuwa ni malipo ya Madiwani kupelekwa Serikali Kuu, hata wakati

nachangia Wizara ya TAMISEMI nilisema kwamba tunaomba Madiwani wetu wakalipwe stahiki zao na Serikali Kuu ili kuwaondolea mzigo wa kukopwa...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tupunguze sauti tuwasikilize wachangiaji.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izeze kuwalipa Madiwani wetu kupitia Serikali Kuu ili kuwapunguzia mihani na msalaba mzito waliokuwa wanaubeba Madiwani kwa kukopwa na Wakurugenzi kwenye halmashauri zao. Kwa hiyo niwapongeze sana, na niipongeze sana Serikali kwa kuliona hilo na kuweza kuwapelekea Madiwani kwenda kuwalipa kwenye Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza hapa wakati nachangia Wizara ya TAMISEMI, kwamba Serikali ikipeleka Madiwani wetu kwenda kulipwa Serikali Kuu tuna watu hawa ambao pia wao ndiyo watendaji wetu wakuu huko chini baada ya Madiwani. Wenyeviti wa vijiji tunao ambao ndio wanafanya kazi kule nikapendekeza kwamba Madiwani tuwapeleke Serikali Kuu ili zile fedha zilizokuwa zinalipa Madiwani ziende na zenyewe zikasaidie kuwalipa posho angalau ya shilingi laki moja wenyeviti wetu wa vijiji, na wao waweze kutekeleza majukumu yao na wajibu wao kwa weledi kuliko sasa wanapata posho ya shilingi 10,000 na wakati mwingine hazilipwi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hilo Mheshimiwa Waziri atakwenda kulichukua kama alivyoelekeza Mama, naamini watamshauri vyema, hali kadhalika na mama aweze kuona kwa jicho la kipekee kwa ajili ya kuwasaidia wenyeviti wetu wa vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende sasa kwenye hotuba ya Waziri na ninaomba nianze na suala zima la kodi ya majengo. Wamesema Wabunge wengi, lakini na mimi naomba niseme hofu yangu kwenye suala zima la kodi ya majengo. Mheshimiwa Waziri anatuambia kwamba

itakwenda kulipwa kwa mfumo wa LUKU na kila mwezi italipwa shilingi 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi ya majengo kwa kila nyumba ni shilingi 20,000. Ukilipa kila mwezi shilingi 1,000 kwa mwaka mzima utakuwa umelipa shilingi 12,000 hii shilingi 8,000 nani anaifidia? Niombe nisaidiwe ufafanuzi kwenye suala zima hili la kodi ya majengo. Lakini ukiangalia tu kwa uhalisia wa kawaida ni kitu ambacho hakiwezekani, kwamba mpangaji niende nikampe huo mzigo wa kulipa kodi ya jengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye kodi ya majengo pia ametuambia kwamba shilingi 1,000 na shilingi 5,000 kwenye nyumba yenye mita moja, na zile nyumba ambazo zina mita zaidi ya moja zinatengenezewa mfumo wao, ni lini zinakwenda kutengenezewa huo mfumo? Imekuaje watengeneze huo mfumo wa kodi ya jengo kwenye nyumba yenye mita moja wakashindwa kutengeneza huo mfumo wa nyumba yenye mita zaidi ya moja? Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri aende akakae na timu yake vizuri watengeneze namna bora ambayo tunaweza kwenda kukusanya kodi hii ya majengo ili tuweze kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 nikiwa nachangia bajeti hii nilisema kwamba Serikali imekuwa haipunguzi kodi kwenye vifaa vya ujenzi, lakini inakwenda kuongeza kodi kwenye vifaa vya ujenzi huku wanataka kodi kwenye majengo. Ukiangalia hapa kwenye ongezeko la ushuru wa forodha, Mheshimiwa Waziri amekuja na mapendekezo ya kuongeza ushuru kwenye bidhaa ya mabati asilimia kumi au Dola za Kimarekani 250. Sasa tunataka wananchi wetu waweze kujenga na kuishi kwenye nyumba bora leo unakwenda kuwaongezea kodi huko kwenye hizo bati ni mwananchi gani atakayeweza kwenda kujenga nyumba kwa kwenda kupandisha kodi ya mabati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaturudisha nyuma tena watu hawa watarudi nyuma, hawataweza kwenda kumudu gharama za kununua mabati na matokeo yake nyumba za mabati zitapungua tutakwenda kuanza kurudi kwenye

nyumba za matope za *full suit* juu na chini kama enzi hizo tulizotoka huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo nimuombe Mheshimiwa Waziri, kama umeamua kuchukua kodi ya majengo tunaomba basi punguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi; na kama mnaamua kuchukua kodi kwenye majengo basi huku kwingine tuache ili watu waweze kupumua na waweze kuona ni namna gani wanaweza kuichangia Serikali yao kwenye suala zima la kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye kuzungumzia suala la barabara zetu za kimkakati za kuunganisha mikoa pamoja na wilaya. Ili tuweze kukuza uchumi wetu; na Tanzania sisi tunategemea sana suala zima, la kilimo na kilimo bila barabara hatuwezi kupata tija kwenye kilimo. Sasa sisi mikoa minne, Mkoa wa Tanga, Manyara, Dodoma na Singida tuna barabara yetu ya kutokea Kilindi. Nilisema, kwamba, barabara hii ina ahadi ya marais watatu, Rais Awamu ya Tatu, Rais Awamu ya Nne na Awamu ya Tano waliahidi kujenga barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na barabara hii sisi kwenye uchumi ndiyo barabara itakayoweza kusaidia wakulima wetu kuweza kupata tija kwenye mazao yao. Lakini pili, ni juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amezindua zao la kimkakati kwenye mikoa mitatu, mkoa wa Dodoma, Singida pamoja na Simiyu. Kama barabara hizi hazitakwenda kupitika na hizi ndoto za mazao ya kibiashara ya kimkakati ambayo tunaenda kuyapeleka kwenye maeneo yetu, haya mazao pia itakuja kufikia hatua wananchi wamelima mazao haya lakini watakosa barabara za kuzipitisha mazao haya kwa ajili ya kwenda sokoni na kwenda kwenye viwanda vyetu. kwa hiyo mwisho wa siku hatutakuwa na tija kwenye suala zima la malengo ama na matarajio yetu ya kwenda kupandisha uchumi wa taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeiona barabara hii kwenye mpango, lakini kwenye bajeti mmeweka kujenga barabara kilometa 20. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwa

umuhimu wa zao la alizeti ambalo tunalima Mkoa wa Dodoma na Singida niombe barabara hii Mheshimiwa Waziri ukaingalie kwa jicho la kipekee iende ikajengwe kwa haraka ili tuweze kupata tija kwenye suala la zao hili la mkakati ambalo Serikali mmeweza kuliona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana tena na suala hilo hilo la ujenzi wa barabara zetu hali kadhalika Serikali imekuwa ikipata kigugumizi sana kwenye suala zima la ulipaji wa fidia. Tunapokwenda kujenga barabara zote na maeneo mengine suala la ulipaji wa fidia Wizara ama Serikali mmekuwa mkipata kigugumizi na kuchelewesha ulipaji wa fidia ambao umetusababishia miradi mingi kushindwa kumalizika kwa wakati na hivyo hasara kwa wakandarasi wetu pamoja na kuchukua muda mrefu kumaliza miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mnapokwenda kutekeleza miradi ya kimikakati niwaombe sana, kwa suala la ulipaji wa fidia, fedha hizo zitoke kwa haraka na hatimaye tuweze kuwa tunakwenda kwa kadri ambavyo tunajipangia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la utekelezaji wa bajeti na nitazisema wizara chache, pia suala zima la utekelezaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo kwenye wizara mbalimbali hali kadhalika Serikali imekuwa na kigugumizi sana. Waziri wa Fedha kwa kweli Wizara yako imekuwa na changamoto kubwa kwa kuwa mmekuwa mkichelewesha kupeleka fedha kwenye wizara zetu. Vilevile hata mkizipeleka pia hamzipeleki kama Bunge lilivyopitisha, mnapeleka kidogo kidogo ambazo mwisho wa siku haziendi kwenda kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kwa kipindi cha miaka mitano Wizara hii imepelekewa fedha za maendeleo asilimia 19.3, lakini Wizara ya Mifugo kwa miaka mitano pia mfululizo wamepelekewa fedha za maendeleo kwa asilimia 21, yaani hata asilimia 30, 50 haijafika. Kwa hiyo tunaona ni kwa namna gani Wizara ya Fedha mnakwamisha

maendeleo ya taifa letu kwa kuvuta miguu kwenda kupeleka fedha kwenye shughuli za maendeleo kwa ajili ya kuweza kuleta tija kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya *Petrol* kuongeza tozo ya mafuta ya taa, na Mheshimiwa Waziri pendekezo lake anasema anakwenda kuongeza tozo ya mafuta ya taa ili kudhibiti wafanyabiashara wakubwa wanaokwenda kutumia mafuta ya taa kuchakachua *diesel* na *petrol*. Mheshimiwa Waziri yaani umekaa na watalaam wako, mkachakachua, mkapanga, mkapangua mkazichanga karata ukaona mbinu rahisi ama njia rahisi ni kwenda kupandisha mafuta ya taa ambayo ndiyo nishati peke yake iliyobaki kwa wananchi wengi ambao bado hawajafikishiwa umeme vijijini?. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri niombe nenda kwenye suala zima la uongezaji mafuta ya taa hiyo shilingi mia moja uliyoiongeza, hebu nenda kajipangeni upya. Tunafahamu fika, hata wewe Iramba kwako unajua ni vijiji vingapi vyenye umeme? Nenda, watu leo bado wanatumia mafuta ya taa, tunapoendelea kuongeza huu mzigo wa shilingi mia kwa wananchi wetu haikusaidii, hata wewe utakuja kuulizwa ulikuwa na maana gani? tuwaache hawa watu, tafuta namna ya kuwadhibiti hawa wanaochakachua huku, punguza mzigo kwa mtanzania mnyonge asiyekuwa na hatia. Kwa hiyo nenda ukaondoe kodi hii ili wananchi wetu waweze kupata nafuu ya maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la shilingi mia moja pia kwenye lita ya kila mafuta ya *petrol* na *diesel*; nimalizie tu. Pia hili nalo nikuombe Mheshimiwa Waziri nenda kaliangalie, ukiongeza tozo tena kwenye *petrol* na *diesel* hali kadhalika maisha yatapanda, nauli zitapanda, vyakula vitapanda kwa sababu vinasafirishwa, kwa hiyo gharama ya maisha inakwenda kupanda huo mzigo anaenda kubeba mwananchi wa kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie la mwisho. Ahadi nyingi za viongozi wetu waliopita zimekuwa zikisemwa humu

ndani mara kwa mara na ni wajibu wetu kwa sababu ahadi ni deni; na siku zote ahadi zinazoahidiwa na viongozi wetu kwa mfano Mheshimiwa Rais au Makamu wa Rais ama Waziri Mkuu inakuwa ni taasisi siyo mtu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka 2015/2020 Serikali Awamu ya Tano iliwaahidi Watanzania kuwapatia milioni 50 kila kijiji, lakini mpaka sasa bado sijawahi kuisikia wala kuona hii milioni 50. Ahadi ni deni, Mheshimiwa Waziri wa Fedha niombe hii milioni 50, kwa kuwa ni ahadi kama ahadi zingine na wananchi wetu Watanzania waliopo huko bado wana matumaini wanasubiri milioni 50 kila Kijiji, niombe sasa hii milioni 50 kila kijiji itolewe ili wananchi wetu waende wakapate mitaji yenye tija na waweze kujenga uchumi wa taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa Mwita Getere naomba niwatambue wageni wawili wa Mheshimiwa Hamis Mwijuma ambao ni viongozi wa Kamati ya Wakulima wa Msitu ya Dilemma kutoka Muheza mkoani Tanga, ndugu Mohamed Shehe na Ndugu Adam Kibaha, hawa pia ni wapiga kura wake, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwita Getere baadaye Mheshimiwa Janejelly na Mheshimiwa Haji Amour Haji, wajjandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa mambo mengi tu, lakini nimkumbuke aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli. Kama huko aliko

duniani na huku nje mambo yakaharibika sisi tutamlaumu yeye aliyetuachia watu wazuri kwenye safu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magufuli alikuwa utatu mtiifu, Wakristu msinieleme vibaya nikasema Utatu Mtakatifu, utatu mtiifu. Wa kwanza ni huyu Rais wetu wa sasa ambaye alikuwa Makamu wa Rais, Mama Samia, ndiye aliye wa kwanza kwake. Wa pili alikuwa naye Waziri Mkuu ambaye bado anaye Rais wa sasa. Makamu wa Rais wa sasa alikuwa Waziri wake wa Fedha ambaye naye yupo. Hivi nchi inayumbaje, nchi ambayo Magufuli ameiacha kwenye watu waliokuwa utatu wake mtiif inaachaje? haiwezi kuacha. Kwa hiyo mimi naamini katika hili tunaloendanalo nchi itaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme maneno, na kwa maneno haya msini-*quotet* mkasema sasa wewe mgombea ukamishna, a' a', ni maneno yangu. Nchi yetu inatakiwa iwe na watu watakatifu, watu wakumuogopa Mungu, watu wasio na mapenzi ya kujipendekeza kumbe roho zao zipo tofauti. Wakitokea watu wa namna hiyo na Mama Samia ambaye sasa ni mtiifu wakati wote nchi itakwenda salama; lakini kama kuna watu wala rushwa, watu wabadhilifu watakao mzunguka mama akiwa kwenye jukwaa wanampamba huku ndani wanafanya mambo mengine nchi itakwenda chini.. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi niseme tumuombe Mungu, watakatifu mawaziri wake wote wafuate watu wale watatu ambao Hayati Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli alituachia. Alituachia Makamu wa Rais ndiye amekuwa Rais wa sasa, alituachia Waziri Mkuu bado yupo na anafanya kazi, yaani huyu si wa kusema tena. Hivi nchi inawezaje kwenda nje ya Majaliwa? haiwezekani, nchi inawezaje kwenda tofauti na Mpango? Haiwezekani.

Kwa hiyo tuwaombe viongozi wetu, mawaziri wetu na viongozi wote wawe watiifu, roho zao ziendane na wanavyosema kwenye majukwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inanishangaza sana kumuona mtu yupo jukwaani anazungumza mambo mazito, lakini huku chini ana mambo ya ajabu sana, mla rushwa mkubwa, kwa nini sasa inakuwa hivyo? Tuombe watu wetu Mungu awasaidie waende upande ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili nalizungumza polepole maana hili lilikuwa la nchi. Nilikuwa naangalia *PAYE* ile kodi ambayo inalipwa na watumishi wa Serikali. Waheshimiwa Wabunge nataka hili mlielewe vizuri. Tuna madaraja manne ya *PAYE*. Daraja la kwanza ni wale watu wa 270 mpaka 540 ambao wanalipa asilimia tisa, maana yake ikipunguzwa sasa itakuwa asilimia nane. Daraja linalofuata ni 540 mpaka 740, hawa wanalipa asilimia 20, ikipunguzwa itakuwa asilimia 19. Daraja linalofuata ni 740 mpaka 1,000,000, hawa wanalipa asilimia 25. Daraja la mwisho ni kuanzia 1,000,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wabunge nimesikia watu wengine wanazungumza huko mitaani kwamba Wabunge wanazungumza haya mambo hawalipi kodi; jamani, hii *Pay As You Earn* maana yake makundi yote sisi ndio tunalipa. Mbunge analipia milioni moja na kitu kwenye makundi yote. Kwa *formular* hii kundi la kwanza litalipiwa na kundi la pili, kundi la pili litalipiwa na kundi la tatu, kundi la tatu litalipiwa na kundi la nne, kwa hiyo sisi Wabunge makundi yote tunayalipa hela. Sisi ndio tuna kodi kubwa katika watumishi wa Serikali ambao wanalipa Serikalini hapa, kwa hiyo tuseme kwamba tunalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa na ombi langu hapa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba unisikilize hapa kidogo. Mimi naona badala ya kupunguza asilimia moja ya hii kodi hili kundi la kwanza la 270 mpaka 540 tuliondoe, tuliondoe hilo kundi lisilipe kodi kwa sababu ukipiga hesabu yake ni kama bilioni saba au bilioni nane. Tuliondoe tubaki na kundi la pili na kundi la tatu na kundi la mwisho ili hawa ambao wana hela kidogo waendeleo kupata kidogo waendeleo kuishi. Kwa hiyo ushauri wangu kwa hapo nilikuwa naona hapo inakuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie *TRA*; na Mheshimiwa Mwigulu kama ni jambo la kutufanyia sisi Watanzania ili tukukumbuke masaa yako yote ni kuangalia mfumo wa *TRA* kwa sababu mfumo wa *TRA* si rafiki kwa kukusanya hela, mfumo wa *TRA* unakupa nafasi ya kwenda kukadiria. Mimi naleta makontena ya bilioni tatu halafu tunakubaliana sasa nilipe ngapi. Mimi ninaduka unakuja kunipigia mahesabu ya bilioni mbili, milioni 500 au milioni 100 au bilioni 50 tunakubaliana nilipe ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tutafute mifumo mizuri ya *TRA* ili hela zetu ziweze kupatikana, vinginevyo hakuna hela tutakayokusanya hapo. Kwa hiyo tuangalie mifumo ya *TRA* kwenye maduka, kwenye bandari na kwenye maeneo yote tuweze kuona kwamba tunaifanye mifumo hiyo ili tuweze kuishi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kodi ya majengo. Mimi hii kodi kwangu naona kama ni jambo gumu sana, na hasa kwa watu wa vijijini. Naiomba Serikali, Mheshimiwa Mwigulu wewe ni mtaalam wa hesabu hizi. Hii kodi wala msiipeleke kwenye umeme huko, hii kodi pelekeni kwenye Wizara ya Ardhi. Mtu mwenye kiwanja mumuungezee kakodi hako alipe, si ni mali yake, kuna ubaya gani? Hii kodi msiipeleke popote ipelekeni kwenye Wizara ya Ardhi walipe kupitia Wizara ya Ardhi, mimi nadhani hapo itakuwa nzuri zaidi kwenye upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizingumzie Deni la Taifa. Deni la Taifa ni himilivu, na tunasema ukiangalia nchi ambazo ni *ten* bora zenye madeni makubwa ni pamoja na Tanzania, ni ya kumi. Ni kweli tuna deni kubwa, lakini kukopa si dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi tajiri duniani ni Marekani, lakini nchi yenye madeni makubwa duniani ni Marekani. Sasa sijui kama watu mnaliona hilo, nchi tajiri duniani ni Marekani na nchi yenye madeni makubwa duniani ni Marekani; kwa hiyo kukopa si dhambi, mimi nafikiri tunakopa kufanyia nini ndiyo hoja. Kwamba tunakopa kulipa

mishahara, tunakopa kufanya vitu ambavyo havina tija.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nishauri kwenye Serikali hii ya Awamu ya Sita, Mama asiogope kukopa, akope kwenye malengo maalum. La muhimu hapa sana ninachoomba ni kwamba sisi Wabunge sasa ufike wakati tupewe taarifa, kwamba tumekopa wapi na tunadaiwa wapi, na hili deni tunalipa lini na likoje. Ije taarifa rasmi hapa Bungeni tujue tunadaiwa kiasi gani na tunadai kiasi gani na nani anatudai, tujue ili sisi Wabunge tuwaeleze watu huko, kwamba deni letu ni himilivu, lakini tunadaiwa na watu fulani, lakini kukopa si dhambi; kwa sababu hakuna kitu kinaitwa *good debt*, madeni yote ni mabaya hakuna deni zuri, hata sisi madeni yetu ni mabaya tu hakuna deni zuri hapa.  
(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie mifumo ya usimamizi wa fedha za bajeti zetu, na hapa ndipo patamu. Kuna watu wanaitwa Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mkoa, Ma-DAS, Makatibu Tarafa, Wakurugenzi, Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji; ni nani anasimamia vizuri miradi inayopolekwa kwenye Vijiji huko na kwenye Kata? Ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana. Akienda Naibu Waziri kwenye Wilaya anakutana na Mkuu wa Mkoa, anakutana na Mkuu wa Wilaya. Kama kuna hela zimeliwa kwenye Wilaya hiyo Mbunge analalamika, Wananchi wanalalamika, Waziri aliyeenda pale kama ni Naibu au Waziri wa Wizara analalamika, Mkuu wa Mkoa anamwambia Mkuu tuachie hilo tutatekeleza, mwaka wa kwanza. Anakwenda pale Waziri Mkuu mradi ule ule kwenye sehemu nyingine umeliwa, Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wanamwambia tuachie Mkuu hilo tutatekeleza. Sasa najiuliza, hivi nchi yetu imekuwa ya kurugenzi ya matukio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi inatokeaje mkoa au wilaya fedha zinaliwa milioni moja, milioni mbili, milioni mia tatu, milioni mia nne, kila siku tunapoenda kwenye mkoa na wilaya kuna madeni na kuna hela zimeliwa, Wakuu wa Wilaya

ukikutana nao wanakwambia mkuu tuachie, tunatekeleza mkuu tuachie tunatekeleza, watamaliza lini? *(Makofi)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita kuna taarifa.

## TAARIFA

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa mchangiaji, hapo anapoongea ni penyewe sasa, maana tunapitisha bajeti nyingi kubwa lakini ukiangalia kiuhalisia hela zinaliwa na hakuna mtu anayefungwa. Nilikuwa napenda kumpa taarifa mchangiaji yupo vizuri sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. BONIPHACE W. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Unajua humu ndani tupo tofauti, wapo Wabunge wanaoishi kwenye lami huko na kuna Wabunge tunaishi vijijini, sisi wa vijijini ndio tuna shida. Hivi Mbunge kama mfano Mheshimiwa Zungu, Mwenyekiti wetu ana shida gani kule, kule atazungumza watu wake tu wakawaida wale, lakini ukiangalia magorofa yamejaa, lami imejaa, kila kitu kimejaa; umeme upo vizuri, atazungumza mambo mengine yapo ya kibinadamu lakini si kama ya kwetu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mfumo wa utendaji wetu ukubalike ili Wakuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya wawe na mikataba. Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ambaye eneo lake lina wizi, lina ubadhilifu watuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani tukawe na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mkoa, Watendaji wa Kata, Makatibu Tarafa, Ma-DAS, Ma-RAS miradi inaliwa wapo, ukienda mkuu tuachie, ukienda mkuu tuachie, wanamaliza lini?

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

### T A A R I F A

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa kaka yangu ninaye mheshimu sana, Mheshimiwa Getere. Siyo nchini kote Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wanafanya ubadhilifu. Mimi kwa Wilaya ninayotoka, ya Ikungi Mkuu wetu wa Wilaya Mpogoro pamoja na Mkurugenzi wake Kijazi wanafanyakazi iliyotukuka ambayo hata Waziri Mkuu alipokuja kwenye ziara ndio moja ya wilaya alizisifia ambazo hazikuwa na makando makando katika utendaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapowazungumza kwa u-*general* tuwatendee haki baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi ni waadilifu sana na wanaitumikia nchi kwa moyo wa uzalendo sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita malizia dakika yako.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mtaalam amezungumza, mimi nimezungumza toka awali hakunisikia, nimesema baadhi, labda Kiswahili cha kikurya hukusikia vizuri. Kwa hiyo, mimi nataka niombe kusema hivi, unajua tunavyozungumza uhalifu wa jambo tunazungumza *in terms of average*. Kama tuna watu Wakuu wa Mikoa 100 wanaofanya vizuri au kwa mfano sisi Wabunge tuulizwe kwenye Majimbo yetu ni Wabunge wangapi wana miradi iliyoliwa? Wataweza kunyoosha juu Wabunge hapa, miradi ambayo ipo ambayo haitekelezeki ni mingapi? Hivi tujjulize swali, Mtendaji wa Kata akiamka asubuhi anaenda wapi? Ana ratiba gani, Katibu Tarafa anaenda wapi? Tutengeneze utaratibu ambao mtu akiamka asubuhi kama ni mtumishi wa Serikali ana kazi ya kufanya, anaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hilo nataka nikuambie tukitengeneza mfumo mzuri, maana yake Serikali yetu itaenda vizuri. Kila mtu atakuwa anaamka na kitabu tuwe

*tuna-search* umeenda kufanya kazi gani leo? Leo tuna wale maafisa ugani anaweza kuishi Dodoma, anakaa Singida. Tunataka kuwajua asubuhi wanaamka wanaenda wapi? Kazi gani wanafanya? Watoe taarifa ya kila siku wanafanya kazi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti: kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwamba niunge mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita. Mheshimiwa Janejelly, halafu atafuatiwa, Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Maimuna Mtanda, ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye kitu muhimu ambayo ni Bajeti ya Serikali. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwigulu, mzee wa Yanga na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Masauni, mzee wa kimyakimya na timu ya wataalam wote wa Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika bajeti hii imeonyesha Wizara ya Fedha ina wachumi waliobobea. Wamekuja na bajeti ambayo imegusa kila kundi la Mtanzania. Ukiangalia vijana wameguswa, wazee wameguswa, wafanyabiashara wameguswa na akinamama wameguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama Samia Suluhu. Usiposhukuru kidogo hata kikubwa huwezi kushukuru, kwa masuala ambayo amefanya kwa watumishi wa Tanzania. Mimi nijikite kwenye hotuba aya ya 44, maslahi ya watumishi. Akiwa kwenye Mei Mosi alisema, atapunguza *Pay As You Earn*, itabakia tarakimu moja ambayo ni nane na amefanya hivyo. Alisema atafuta tozo asilimia sita kwa mikopo ya vyuo vikuu, amefanya hivyo.

Vilevile ametoa bilioni 449, kwa ajili ya kupandisha madaraja ya watumishi, si kazi ndogo hii. Mpaka sasa ripoti za leo watumishi 78 wameshapandishwa madaraja, kati ya

watumishi 92,619 ambao wanatakiwa kupandishwa. Kwenye hili ni lazima nitoe ushauri kidogo kwa Serikali, kwenye upandishaji wa vyeo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi watatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upandishwaji wa vyeo, kuna kasoro kidogo imetokea. Tunakumbuka 2016 watumishi walipandishwa madaraja, lakini muda kidogo yakafutwa, wakanyang'anywa zile barua za kupandishwa vyeo. Sasa, zoezi hili lilivyoanza, imekuwa ni adhabu kwao, wanahesabika walipandishwa 2017. Kwa hiyo, hawana sifa ya kupandishwa vyeo sasa hivi na watumishi wengine wameshaka miaka 10, lakini barua waliyonyang'anya ilikuwa ni Serikali yetu Tukufu. Kwa hiyo, tuombe hilo wajaribu kurekebisha kidogo, hawa watumishi wafikiriwe, ambao walikuwa mwaka 2016 wako kwenye haki ya kupandishwa vyeo, lakini walipandishwa halafu wakanyang'anywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye michango ya Mifuko. Niishukuru sana Serikali, wamekuja na muarobaini wa kwenda kuponya wastaafu wetu. Wanapoamua kwamba makato watabaki nayo na watayapeleka kwenye Mifuko. Hata hivyo, niwaombe Serikali yangu Tukufu na Waziri wa Fedha, fedha hizi wakishabaki nazo ziende kwa wakati. Tusije tukasababisha malipo mengine ya *penalty* kwa kuzichelewesha na tusije tukasababisha wastaafu wetu kuchelewa kupata maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna madeni ya wafanyakazi yanayosababishwa na upandishwaji wa madaraja. Kuna watumishi ambao walipandishwa mwaka na 2018 na 2016, bado hawajalipwa tofauti yao, kati ya mshahara wa zamani na mshahara mpya, yamekuwa ni madeni sugu. Tuombe hili nalo Wizara ya Fedha, maana ndio wahakiki wa madeni, basi wakawalipe watumishi hawa wafaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mfuko unaitwa Mikopo ya Usafiri kwa Watumishi wa Serikali, mikopo ambayo haina

riba. Mfuko huu uko chini ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Tuiombe Serikali yetu wakae watafute namna ya kuuongezea fedha huu Mfuko, ili watumishi wote sasa waweze kufaidi matunda ya Mfuko huu. Fedha imekuwa haitoshi kwa hiyo, wengine wanasikia historia tu kwamba kuna mikopo ya magari yawawezeshe kuja kazini na kurudi nyumbani, lakini hawajawahi kupata mkopo huu. Ni kwa sababu, Mfuko umepewa fedha kidogo. Kwa hiyo, tuombe hapo fedha iongezwe kwenye huo Mfuko ili watumishi waweze kufaidi matunda ambayo wamewawekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la Madiwani ambao watalipwa moja kwa moja kutoka Serikali kuu. Kwenye halmashauri kama tunasema hawa Madiwani watalipwa na Mfuko wa Serikali kuu, tuangalie na wale watumishi ambao walikuwa wanalipwa moja kwa moja kutoka kwenye halmashauri. Watumishi hawa wamekuwa wanakopwa sana, lakini walivyolishughulikia kama Serikali, manispaa za mjini ndio waliwahi kuhamisha watumishi wao wakalipwa na Serikali kuu, lakini wa pembezoni mpaka sasa hivi, wanalipwa kutoka kwenye vyanzo vya mapato vya halmashauri. Hasara wanayopata, hawawezi kupewa bima ya afya, hawawezi kuwa kwenye *pension* watumishi hawa. Sasa nao tuwasaidie waweze kufaidi matunda ya Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye malipo ya Watendaji wa Serikali za Mitaa. Tumeamua kuwalipa Madiwani, Watendaji wa Serikali za Mitaa, lakini tumesahau Wenyeviti wetu wa Vijiji na Serikali za Mitaa. Hawa ndio huanza na wananchi wetu *from zero*, lakini Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa au Mwenyekiti analipwa shilingi 30,000 kwenye Manispaa zingine, pengine shilingi 10,000 yaani haina *standard*. Hata hiyo yenyewe kulipwa inaweza ikapita miezi sita, hajawahi kulipwa.

Suala hili linawaondolea heshima na uimara wa kufanya kazi na wanakuwa wana wasiwasi wa kufanya kazi. Kwa hiyo tuombe Serikali hawa watu nao iwaangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nimshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu, Tunamwamini, kwamba bajeti hii tukiipitisha, itaenda kwa wakati kwenye manispaa, kwenye mikoa yetu na kwenye majimbo yetu ili ikafanye kazi kama ilivyopitishwa. Tuna uhakika huu upandishaji wa watumishi, fedha zitabaki watapandishwa wenye haki za kupandishwa, lakini wakiangalia ile kasoro ambayo tumeisema ya 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga hoja mkono mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Janejelly James. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Haji Amour Haji na baadaye, Mheshimiwa Maimuna Mtanda na Mheshimiwa Anastazia Wambura, wajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa ruhusa yako nami nisiwe mchoyo wa kushukuru, kwa kunichagua katika kuwasilisha mchango wa bajeti yetu ya Serikali, ambao ni mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia kwanza napenda kumpongeza pamoja na timu yake, Waziri wa Fedha na Mipango, kwa hotuba yake nzuri na mtiririko wake mzuri katika kuwasilisha katika hadhira yetu hii ya Bunge. Pia, nampongeza Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kutufikisha hapa tulipo na kwa kuweza kuweka maelekezo yake mazuri sana kama ambavyo katika bajeti zetu hizi tunavyokwenda nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchangiaji wangu, nitajaribu kugusa mambo matatu. Cha mwanzo, nitajaribu kuangalia suala la uchumi wa nchi yetu. Unajua kukua kwa uchumi maana yake wakati mwingine watu wanajaribu kutafuta, ile tafsiri ya uchumi. Kwa nini uchumi unaambiwa kwamba umekua kwa asilimia nne au asilimia ngapi. Mwananchi wa chini mara nyingi huwa hawezi kujua uchumi namna unavyokua, lakini kwa namna ambavyo maendeleo ya nchi yetu yanavyopiga hatua, hasa katika masuala ya

ujenzi wa miundombinu yetu, maana yake ile ni dhahiri kwamba uchumi wa nchi yetu unakua. Kigezo cha mwanzo ni kuona ile miradi mikubwa iko katika hali ya uendelevu, kwamba, tangu ilivyoanza miradi hiyo maana yake iko katika hali ya uendelevu. Sasa uendelevu ule maana yake ni kigezo dhahiri kwamba nchi yetu ya Tanzania inakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la plii, tukizungumzia suala la bajeti, bajeti yetu hii tutasema kwamba ni ya ushirikishwaji wa watu kulipa kodi bila ya hiari. Kwa nini nazungumza kwamba ni bajeti ya shirikishi ya watu kulipa kodi bila ya hiari, kutokana na kwamba kwa namna ya zile kodi zilivyowekwa. Wabunge wengi wanajaribu *ku-question* suala la kodi ya nyumba kwamba, labda pengine litampa mzigo mwenye nyumba au mpangaji katika nyumba. Suala lile kiukweli na kiundani kabisa maana yake ile ni dhahiri kwamba, tunashirikisha ile jamii iliyokuwepo katika makazi yetu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijaribu kulaumu au kujaribu kulalamika kwa Sh.1,000/= ambayo inalipwa kwa kila mwezi kwamba, ikawa ni suala ambalo ni kubwa sana kwa kushirikishwa wananchi wetu kulipa katika tozo ya nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nasema kwamba bajeti yetu ni uendelezaji wa kazi za Awamu ya Tano ambayo imeziacha. Nasema kwa mujibu wa bajeti ambayo iliyokuwepo, ni dhahiri kwamba mfumo wa bajeti uliokuwepo, haya mambo yote ambayo yameachwa, kwa upande wa Serikali ya Awamu ya Tano, maana yake ni dhahiri kwamba kodi inalenga hasa kumalizia yale yote ambayo yameachwa. Kwa imani yetu, tuna uhakika kwa uongozi tuliokuwa nao kwamba, yale yote ambayo yameachwa na Hayati Dkt. Pombe Magufuli, mambo yale yote yataweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina wasiwasi kwa mujibu wa timu tuliyoukuwa nayo na kwa uongozi wetu wa mama na kwa namna ambavyo, yeye mwenyewe binafsi anavyofanya kazi katika kuishirikisha jamii. Kaanza kuishirikisha jamii ya

wanawake, akaweza kuwaeleza namna ya uchumi wa nchi tunaokusudia kwenda nao. Tangu juzi tunamwona Rais wetu akiwa kule Mwanza, nako vile vile akishajihisha masuala haya haya ya ulipaji kodi. Ni dhahiri anaweka ile picha ya namna ya mfumo wa Serikali ya Awamu ya Sita namna ilivyo, leo tumemuona akiwashirikisha vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akawaeleza vizuri sana kuhusu kuwaundia Mabaraza yao ya Vijana kwamba, huku upande wa Tanzania Bara hakuna Baraza la Vijana, lakini kutokana na hotuba yake ile, nasema kwamba vijana wamepata moyo mkubwa sana. Kutokana na maneno yake ni dhahiri kwamba vijana wamepata mwamko na hasa katika masuala ya hii bajeti yetu, vijana wataleta mchango mkubwa sana na wanaweza kusababisha kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija suala la bajeti iliyoletwa, maana yake imekidhi mapendekezo yote yaliyokuwa yamependekezwa na Wabunge katika Bunge letu hili. Wabunge wengi walikuwa na vilio vingi kabisa, walikuwa wanalia kuhusiana na suala la *TARURA* na mambo mengi ambayo walikuwa wanaeleza au wanatoa vilio vyao yameweza kupatiwa muarobaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema kwamba mama kaja, kwa ajili ya kutatua muarobaini kama lilivyo jina lake Mama Samia Suluhu kweli kaja kuleta suluhu ya uchumi wa nchi yetu. Kwa muktadha huo maana yake kitu cha mwanzo kabla ya bajeti, mama alianza kutatua tatizo la *TARURA*, akazungumza suala la Mfuko wa kila Jimbo kuwapatia shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuzungumza suala hili, nadhani kwamba, nijaribu kumuuliza Waziri tu kwamba huu Mfuko ambao tayari mama kausema, kuhusiana na shilingi milioni 500 kwenye majimbo. Huu Mfuko, je, sisi wa upande wa Zanzibar unatuhusu? Najaribu kuuliza hivyo kwa sababu, kuna Mfuko ule wa Jimbo ambao unatuhusu sote, lakini sasa je, hizi shilingi milioni 500 kwa kila

Jimbo kwa sababu zimezungumzwa kwa kila Jimbo, sasa je, kwa upande wa kule Tanzania Visiwani au Tanzania Zanzibar, je, watapata kiasi gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nitazungumzia suala la VAT. Pia katika hili nalo nashukuru kwamba, Waziri kajaribu kuzungumiza suala vizuri sana kuhusuana na VAT kwamba, upande wa Zanzibar na kwa upande wa Tanzania Bara. Alisema kwamba, kutakuwa na ule unafuu wa kusameheana, kwamba kutakuwa hakuna ulipaji; bidhaa itakayolipiwa Zanzibar ikija Bara maana yake haitotozwa VAT. Hata hivyo, tatizo bado linabaki kwa upande wa bidhaa nyingine, hasa kwa upande wa zile bidhaa ambazo ni kubwa, kwa mfano, kama magari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali zote mbili zikae pamoja, maana yake wawe na ushuru wa aina moja, kuliko kwamba kuna bidhaa ambayo inatozwa Zanzibar, ikija huku unaambiwa kwamba ulipe *different*. Serikali yetu ni moja, Tanzania yetu ni moja, Watanzania ni wamoja. Kwa hivyo, tusijaribu kujenga kitu ambacho kitaleta hitilafu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuhusiana kwa upande wa VAT, kuna suala la vitu ambavyo ni *tangible* na vitu ambavyo ni *intangible*. *Tangible* havina tatizo kwa sababu vinajulikana kwamba kama ni bidhaa zenye kushikika, lakini kuna bidhaa ambazo ni *intangible*, kama suala la mawasiliano, hili suala hili sijui tutalifanyaje katika ugawanaji wa mapato? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kuna Mbunge wetu mmoja, aliwahi kulizungumza suala hili kwamba, Zanzibar wana asilimia 18 kwa upande wa Tanzania Bara kuna asilimia 15. Je, katika utozwaji huu ile *different* maana yake itakuwaje? Nadhani kwamba viongozi wote wawili kwa upande wa Zanzibar na upande wa Tanzania Bara, wangekaa pamoja kujaribu kulijadili suala hilo. Suala hili pia lipo hata kwa upande wa miamala na nadhani kwamba nalo litaweza likaja likaleta hitilafu hiyo. Kwa hivyo, nashauri Waziri

suala hilo aweze kuliangalia vizuri, ili lisije kuleta hitilafu yoyote kwa pande zetu zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nitazungumzia suala la upande wa kilimo. Tanzania ili kuweza kukua kwa uchumi ni vizuri zaidi tukajaribu kuangalia sekta ya uchumi katika hali bora kabisa. Kilimo chetu hiki nadhani kinaweza kikakua na Serikali ina nia kabisa kabisa na ndiyo maana ikaweza kupeleka hizi fedha, kwa ajili ya kutengeneza njia au barabara vijijini kwa ajili ya kurahisisha watu kuweza kusafirisha mazao yao kwa njia ya urahisi. Hata hivyo, ni vizuri zaidi kwa upande wa kilimo tukajaribu kuangalia na miundombinu. Je, miundombinu ambayo iliyokuwepo katika sekta ya kilimo, inaweza kukidhi haja ya uchumi wetu wa Tanzania kuweza kukua? Maana yake hilo lote tujaribu kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napongeza sana bajeti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia, kwa jitihada yake kubwa anayoifanya na kwa mwelekeo wote ambao anauonyesha. Kwa namna ambavyo nchi yetu ya Tanzania kama ulivyokuwa msemu wa Rais wetu wa Zanzibar kule “yajayo yanafurahisha” kwa maana hiyo tutegemee kwamba Tanzania “yajayo yatakuwa yanafurahisha”. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja ya bajeti yetu hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji Amour Haji. Tunaendelea na Mheshimiwa Maimuna Mtanda na Mheshimiwa Anastazia Wambura ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia chochote kuhusiana na bajeti ambayo ipo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi

kubwa ambayo anaifanya pamoja na wasaidizi wake wote. Kwa kweli, ametuheshimisha sana wanawake wa nchi hii, wanawake sasa hivi wamekuja juu, wamepata ujasiri mkubwa, lakini yote hayo ni kutokana na mwongozo wake vile anavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri na timu yake yote, kwa namna ambavyo wameandaa bajeti. Bajeti ni nzuri, bajeti ambayo inawagusa wananchi wote wa nchi hii, kuanzia wakulima, wafanyakazi, wafugaji, pamoja na watumishi wote. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa namna ambavyo mmepokea maoni ya Wabunge, hatimaye mmeweka kwenye bajeti suala la fedha za Madiwani pamoja na Watendaji wa Kata na Maafisa Tarafa, kulipwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muhanga wa Madiwani. Katika Jimbo langu la Newala Vijijini, Madiwani waliomaliza muda wao wanadai Halmashauri posho zao, mpaka leo hawajapata. Kwa hiyo, sasa hii ni tiba, tunashukuru na tunatumaini kwamba Madiwani sasa watafanya kazi kwa moyo, watakuwa na ari kubwa kwa sababu wanajua unapofika mwisho wa mwezi watapata posho zao bila shida. Sasa katika hilo, nami nashauri kwamba tuangalie pia zile posho angalau ziongezeke kidogo kwa sababu kiasi kile kwa kweli ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye masuala muhimu, masuala ya ukusanyaji wa mapato. Natambua kabisa nchi hii ina miradi mikubwa ya Kitaifa inayotekelezwa ambayo inahitaji fedha nyingi. Pia ipo miradi katika Halmashauri zetu ambayo nayo inahitaji fedha za kutosha, lakini kuna Madiwani ambao watalipwa posho kupitia Serikali Kuu, kuna Maafisa Tarafa, kuna Watendaji wa

Kata, fedha hizi ukiangalia zinatakiwa zikusanywe ili hii miradi pamoja na hizi posho ziweze kupatikana. Kama hazitakusanywa vizuri, kwa usimamizi imara, haya ambayo yamewekwa kwenye bajeti yanaweza yasitekelezeke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tuweke namna nzuri ya ukusanyaji wa mapato ili yasivuje, tuweze kutekeleza miradi yetu kwa ufanisi mkubwa. Naomba nitoe mfano mdogo. Kupitia Ripoti ya CAG hii ambayo ameitoa ya mwaka 2019/2020 kuna fedha zaidi ya shilingi bilioni 1.2 ambazo zilikusanywa nje ya mfumo kupitia katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Sababu ambayo CAG ameitoa ni kwamba fedha hizi zilipita nje ya mfumo kwa kukosekana kwa mashine za POS. Pia kulikuwa na fedha nyingine ambazo zilikuwa zinatumiwa, zile fedha mbichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana haya, matatizo ya POS tujijimarishe sasa, tuhakikishe tuna vifaa vya kutosha ambavyo vitaenda kutumika kila eneo linalohusiana na ukusanyaji wa mapato yetu ili malengo yetu yakapate kutimia vile ambavyo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kwa dhati sasa kuanza mpango wa utoaji wa huduma za afya kwa maana ya Bima ya Afya kwa wananchi wote. Ni jambo jema kwa sababu Taifa ambalo litakuwa na wagonjwa wengi, basi halitaweza kuzalisha vile ambavyo tunatarajia. Kwa hiyo, kupitia mpango huu ni matumaini yangu kwamba wananchi watakuwa na afya bora, watafanya kazi zao vizuri na hatimaye Taifa litaweza kujipatia fedha nyingi katika kutekeleza miradi. *(Makofi)*

Mheshiwa Mwenyekiti, sasa hapa naomba nitoe rai kwamba, kwa sababu tumeshaweka huo mkakati, tuandae namna ambayo wale wanaokwenda kukusanya fedha za Bima ya Afya au watakaosimamia ujazaji wa fomu za Bima ya Afya wapatiwe mafunzo maalum, kwa sababu sasa itasambaa nchi nzima tofauti na ilivyo sasa hivi kwamba

wanaopata huduma ya Bima za Afya ni wachache kuliko tunavyotarajia kama Taifa kwamba sasa watu wote wanakwenda kupata hizi huduma za Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naongea hivyo? Naongea hivyo kwa sababu ukienda kwenye Ripoti ile ya CAG, alibaini madai ya zaidi ya shilingi bilioni 2.1 ambayo Bima ya Afya yanaidai Serikali kwa sababu tu ya changamoto ya zile kasoro za ujazaji wa fomu. Sasa ukiangalia wanaopata hizo huduma sio wengi kiasi hicho, lakini fomu ambazo zina shida ya kulipwa fedha zake ni zaidi ya shilingi bilioni 2.1. Je, Watanzania wote watakapoingia kwenye huo mfumo, ni kiasi gani cha kasoro kitasababisha upotevu wa dawa kwa kiasi kikubwa? Kwa hiyo, naomba sana mafunzo yatolewe, watu wawe na ujuzi wa kujaza zile fomu ili changamoto hizi zisije zikajitokeza kule tunakoelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza tena Serikali, kwa kweli katika bajeti hii imeweka mambo mengi sana kuhusiana na masuala ya kilimo. Ukienda kwenye kilimo cha mihogo wameweka namna ambavyo watasimamia mazao ya mihogo, lakini pia hata kwenye korosho. Sasa changamoto yangu ni viwanda. Katika nchi hii kuna baadhi ya viwanda havifanyi kazi sawasawa. Kule kwetu Newala ambako tunazalisha korosho kati ya tani 20 hadi 30 kwa mwaka hatuna kiwanda cha uhakika cha kubangua korosho ili kuithaminisha korosho hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kiwanda cha *Agrofocus*, hiki kimebinafsishwa, lakini tuna kiwanda cha *Micronox*; kiwanda hiki kimepewa mtu ambaye uwezo wake tunadhani ni mdogo kwa sababu, kwa mfano msimu uliopita hakuwa na malighafi. Inaonekana hakuwa na fedha, kwa hiyo, yale ambayo tulitegemea tuyapate kutokana na kiwanda hiki yanashindwa kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vile wakati vinafanya kazi kule Newala, zaidi ya asilimia 80 ya waliokuwa wanafanya kazi pale ni wanawake. Sasa hivi viwanda havifanyi kazi, wanawake wamekaa chini, wanashindwa

kuwasaidia akina baba, wanashindwa kutimiza majukumu yao. Naiomba sana Serikali, nimeangalia pia kwenye bajeti sijaona mkakati wa dhati wa namna ya kuinua viwanda vile vikaweza kufanya kazi kuanzia msimu unaofuata. Kwa hiyo, changamoto hii maana yake bado ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tuna taarifa kwamba kulikuwa na mnunuzi kutoka nje alitaka kununua kiwanda kimojawapo na Serikali ina taarifa hiyo. Naomba basi Mheshimiwa Waziri wakati unakuja kufanya majumuisho utuambie hatima ya ununuzi wa kiwanda kile imefika wapi? Hii itawasaidia wananchi wa Newala kujiajiri kupitia ubanguaji wa korosho wanazozilisha kwa wingi katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo linaleta changamoto kubwa katika Mikoa au Wilaya ya Newala kwa ujumla ni suala la barabara. Wilaya ya Newala ipo Kisiwani, haina hata barabara moja ya lami kati ya wilaya na wilaya au wilaya na mkoa inayofika Wilaya ya Newala. Barabara zote ni za vumbi, lakini ni wakulima wazuri sana wa korosho na mihogo. Kwa hiyo, usafirishaji wa mazao yao ni changamoto kubwa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali ilikuwa kuunganisha barabara za mkoa na mkoa kwa kiwango cha lami. Wilaya ya Newala inaunganisha Mkoa wa Lindi kupitia Mtama kwenda Mtwara, lakini barabara ya kutoka Amkeni – Kitangali mpaka Mtama yenye kilometa 74 ni ya vumbi. Tunaishukuru Serikali imeshajenga kwa kiwango cha lami kilometa 22. Tunaomba Serikali iboreshe barabara hii, ijengwe kwa kiwango cha lami sasa ikamilike ili wananchi wa Newala ambao wanapata huduma zao nyingi katika Jiji la Dar es Salaam nao waweze kutumia barabara hii ikiwa katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho jioni hii ya leo katika bajeti hii ya Serikali. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Kabla sijaendelea, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango na Naibu wake Mheshimiwa Masauni pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kuandaa vizuri mpango huu. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri alitenda haki katika kuwasilisha. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, sisi Wabunge ni wapika kura wake. Nadhani sote tutakubaliana kwamba hajawaji kutuangusha wapiga kura wake na anazitendea haki kura zetu za ndiyo ambazo tulimpa hapa. Hii ni kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya kazi bila ya kujali leo ni Jumamosi wala leo ni Jumapili. Kama tutakumbuka ni kwamba juzi tu hapa tarehe 6 Juni, 2021 tulikuwa naye Lindi katika Mkutano wa Wadau wa Korosho na alitoa tamko zuri sana kutoka kwa mama yetu. Kutokana na matamko haya, wakulima na niseme ni wakulima wote wa korosho pamoja na wadau wengine walifarjika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Jumapili ya tarehe 13 Juni, 2021 tumemwona pia akiwa Singida na Wadau wa Alizeti na ambapo pia alitoa matamko mbalimbali ya kutia faraja kwa wakulima na wadau wa alizeti. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na ninaomba tumwombe kwa Mungu kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye alichukua swali ambalo aliniulizia mtu kwa niaba tarehe 01 Juni, 2021 linalohusiana na barabara ya kutoka Kibiti

– Lindi hadi Mtwara. Hili linazungumzia uharibifu mkubwa wa barabara. Nashukuru sana na ninaomba tu kukumbushia kwamba kweli alifanyie kazi kwa sababu lile ni tatizo kubwa na Serikali ilitoa maelezo hapa kwamba sasa mbadala wake itakuwa ni kwamba magari yenye uzito mkubwa au mizigo mizito iwe inapitia katika Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo lipo pale, nafiri inabidi Serikali ilianganalie kiupekee zaidi kwa sababu katika maeneo ya Kikula, Kilanjelanje, Mandawa na maeneo mengine, kuna uchimbaji mkubwa wa mawe ambayo yanatumika kama malighafi viwandani kwa ajili ya kutengeneza saruji. Sasa hapa katika haya maeneo utaona kuna uharibifu mkubwa sana, kuna mashimo makubwa ambayo ni hatarishi. Tukisema kwamba mizigo ile iwe inasafirishiwa Bandarini, kule hakuna Bandari ni lazima mizigo hii ipite barabarani kwa ajili ya kupeleka viwandani.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ilianganalie hili kwa jicho la pekee ili kusudi tuweze kupunguza zile ajali ambazo zinatokea mara kwa mara kutokana na yale mashimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye bajeti sasa. Niseme tu kwa kweli bajeti hii iliyowasilishwa ina ubora wa kipekee ambao hata wachangiaji waliopita wameweza kutaja na kikubwa zaidi ni uendelezaji wa miradi yetu mikubwa ya kimkakati. Kwa sababu hiyo nampongeza sana Mheshimiwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu, Mama yetu mpendwa, Rais wetu pamoja na Makamu wa Rais kwa ujumla na Serikali ya Awamu ya Sita kwa kazi nzuri ambayo wanawafanyia Watanzania. Mungu wetu atusaidie kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ubora wa bajeti hii, ninachokiona kikubwa ni uhitaji zaidi katika kujitegemea. Nasema hivi kwa sababu moja, bado tuna mahitaji makubwa. Tuna mahitaji katika kuendelezaji wa miundombinu mbalimbali katika Sekta ya Afya, sekta ya elimu, sekta ya barabara na kadhalika. Hata hivyo, tuna

uhitaji wa kuongeza mishahara kwa Madiwani na kwa Watumishi kwa ujumla kama Mheshimiwa Mama yetu alivyoahidi siku ya Mei Mosi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ambalo nalisema, la kujitegemea, naomba kurejea maneno ya mpendwa wetu Hayati Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ambaye alikuwa ni Rais wa Awamu ya Tatu, alisema maneno yafuatayo, naomba kunukuu: *“Napenda kuwakumbusha kuwa njia ya maendeleo imejaa jasho na vumbi. Tuzingatie utamaduni wa kupenda kufanya kazi kwa bidii, maarifa, ubunifu na kujituma. Lawama ni tamu ikitoka mdomoni, lakini peke yake haitapeleka mkono kinywani; na katika kila mfanyakazi akumbuke kuwa muhimu siyo muda anaoutumia kufanya kazi, bali kiasi cha kazi anayoweza kufanya katika muda aliopewa.”* mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa hapa mimi niseme ni bidii, maarifa, ubunifu na kujituma. Kimsingi tukiyatekeleza haya, jibu la kwanza la kutupeleka kwenye kujitegemea litakuwa ni maendeleo ya viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo *Blueprint* ambayo ipo tayari, ilitengenezwa tangu mwaka 2018. Hii ingetusaidia sana katika uwekezaji kwenye sekta mbalimbali. Inazungumzia hasa taratibu za kuwezesha kuharakisha uwekezaji ili kufikia Tanzania ya Viwanda. Hata hivyo, ukiangalia utaona tunasuasua na ninyi ni mashahidi. Hata wale wawezeshaji waliokuja Jumamosi wakatupa semina walisema kwenye viwanda tunakwenda katika *pace* ndogo sana. Sasa naomba tujiulize, tumekwama wapi? Nami naomba tu sasa tuombe Mungu wetu atusaidie ili tutoke hapo na kazi iendelee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina viwanda 35 vya korosho vyenye *capacity* ya kubangua tani 50,000 kwa mwaka. Pamoja na kupewa fursa ya kununua malighafi katika minada ile ya awali, wenye viwanda hivi wamekuwa wakibangua chini ya asilimia 10 tu ya korosho yote ambayo inazalishwa katika nchi yetu. Tuseme kwa mfano kama

mwaka 2020 korosho iliyozalishwa ilikuwa zaidi ya tani 200,000, ilikuwa ni tani kama 210,000 hivi, lakini ubanguaji haukufikia hata tani 20,000. Kwa hiyo, hii ni *below 10%*. (Makofi)

Mheshimwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia tena utaona kwamba kuna baadhi ya wenye viwanda walinunua korosho ghafi na wakaiuza nje korosho ghafi badala ya kupeleka kubangua; na kuna baadhi ya viwanda havikubangua hata kilo moja ya korosho. Sasa nashauri tu tuongeze viwanda vya korosho hapa nchini viende sambamba na ongezeko la uzalishaji; tusiache ikawa ongezeko la uzalishaji wa korosho ni kwa ajili tu ya kusafirisha nje. Hata hivyo, tuondoe vikwazo ambavyo vipo katika ubanguaji wa korosho na kazi iendelee. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna gesi asilia. Sasa sina hakika kama kweli haina *sulphur* hii gesi asilia. Nashauri kama kweli kuna *sulphur* ya kutosha, basi tuitumie hii viwandani ili iweze kuzalisha *sulphur* kwa ajili ya mbolea na viuatilifu. Kwa sababu mwaka huu tumenunua *sulphur* ambayo ni takribani shilingi bilioni 25,000/= na kila mwaka tunanunua *sulphur* kutoka nje. Kwa hiyo, inaweza ikatusaidia, tukianzisha viwanda vitatumia hii *sulphur* kutokana na gesi asilia tuweze kusonga mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo fursa nyingi sana. Kwa mfano, mikoa hii ya Dodoma na Singida tuna ubuyu ambao uko porini. Hatuupalilii, hatupulizi dawa; tuna ukwaju, hatuupalii, hatupulizi dawa; lakini tunaona wenzetu wa Uarabuni wanatumia hapa tende zimekuwa *packed* vizuri sana. Niseme tu, ubuyu una matumizi mengi zaidi ya 300 na kikubwa katika afya. Una vitamini C nyingi sana. Tunapoenda hospitali wagonjwa wa *Corona* tunapewa Vitamic C tunamung'unya, lakini hata ukimung'unya ubuyu, *gram* 20 ambayo ni vijiko viwili tu vya unga wa ubuyu, tayari ni zaidi ya 58% ya *daily recommended allowance* ya *vitamin C*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubuyu na ukwaju unasaidia sana kukinga magonjwa ya kansa, inasaidia sana pia

kupunguza *risk* za maradhi ya moyo na matunda haya pia yanasaidia kuimarisha mifupa. Hata kwa wazee ni matunda mazuri sana. Kwa hiyo, kimsingi tufanye tu *value addition*, tuweke viwanda vya kusindika ubuyu na ukwaju kwa sababu kazi yake wala siyo ngumu kiasi kile, ni sawasawa na wanavyofanya wenzetu katika tendeleo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kidogo.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu sasa kwamba tulinde mapori yetu tusichome moto ovyo, tusikate miti ili kusudi huu ubuyu na ukwaju uendeleo kutusaidia. Pia hata watafiti waangalie namna gani ambavyo tunaweza tukaitunza katika kufanya uzalishaji wa kitaalam tuweze kuendelea kuyapata. Kwa kifupi kabla sijamaliza, niseme tu, tukianzisha viwanda vingi tutaongeza ajira na hasa kwa akina mama na vijana ambazo zitatupunguzia umasikini wa mtu mmoja mmoja lakini pia zitaongeza pato la Taifa kwa sababu viwanda vitalipa kodi ya mapato na VAT. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nimeshamaliza. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu kwa siku ya leo ndiyo umefikia hapo na huyo alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Nawapongeza wote ambao wamepata fursa leo ya kuchangia, naamini wengine wataendelea kuchangia kesho.

Kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge nina tangazo moja. Uongozi wa Yanga Bungeni unatangaza kuwa kesho tarehe 16 Juni, 2021 baada ya Bunge la jioni saa 2.00 usiku tunaombwa wanachama na wapenzi wote tukutane *Morena Hotel* kupokea Rasimu ya Mabadiliko ya Uendeshaji wa Klabu. Viongozi watakaowasilisha hiyo kesho ni Katibu wa Timu, Mjumbe wa Kamati Tendaji Eng. Hersi pamoja na Senzo Mbatha. Kwa hiyo, wapendwa wote, washabiki wa Bunge wote mnaombwa kesho mwende kwa ajili ya kazi hiyo maalum. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho tarehe 16 Juni, 2021 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 16 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*